**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 3 Julai, 2007**

*(Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:-**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia *Order Paper* yetu ya leo, hati za kuwasilisha Mezani iko, Ofisi ya Makamu wa Rais, yuko Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, tumemruka Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala, halafu atakuja Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Hotuba ya Bajeti ya Wizari wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA (MHE. RAMADHAN A. MANENO):**

Tarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. RIZIKI OMARI JUMA (k.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 126

**Barabara Toka Sanya Juu – Mowo**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MHE. AGGREY D. J. MWANRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Hai kwa kushirikiana na Serikali imeanza kujenga daraja la Lima na Siki na lile la Mese kwa kushirikiana na *TANAPA*; na kwa kuwa barabara itokayo Sanya Juu kwenda katika vijiji vya Mowo – Njamu, na Nshere – Hehe na Ngaronyi ina hali mbaya sana na hivyo kutopitika wakati wa mvua:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi wa barabara hiyo hasa ikizingatiwa kuwa wananchi wa vijiji nilivyovitaja ni wakulima wa mazao kama Kahawa, Ndizi, Maharage na kadhalika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara mbayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia yenye urefu wa kilomita 8 ni mojawapo ya barabara ambazo zipo chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Barabara hii inahudumia vijiji vya Mowo-Njamu, Nshere-Hehe na Ngaronyi. Kijamii barabara hii ni muhimu kwa kuhudumia taasisi mbali mbali zikiwemo shule za msingi 4, zahanati 2 na shule za sekondari 2. Kiuchumi barabara hii inatumika kwa kusafirisha mazao ya biashara na chakula yakiwemo mahindi, maharage, ndizi na kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya barabara hii si ya kuridhisha na inahitaji matengenezo. Matengenezo yanayohitajika ili kuifanya ipitike ni ukarabati mkubwa. Gharama ya kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe ni shilingi milioni 208. Kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa Serikali na Halmashauri kwa ujumla barabara hii haijaweza kufanyiwa matengenezo kwa kiwango kinachohitajika. Hata hivyo, ujenzi wa madaraja ya Lima na Siki umekamilika. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Hai katika mwaka wa fedha uliopita (2006/2007) ilitenga kiasi cha shilingi milioni 3.2 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi yenye urefu wa kilomita 3.2. Mkandarasi atakayefanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wananchi amekwishapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itajitahidi kuendeleza kuzifanyia matengenezo barabara zake kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Hai inashauriwa kuendelea kushirikiana na wananchi wake kuifanyia matengenezo madogo madogo ili barabara hiyo iweze kupitika. Katika Bajeti ya 2007/2008, kwa Wilaya ya Siha, barabarA hiyo imeombewa shilingi milioni 14.6 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi ya kilomita 7.3 na sehemu ya Nasai –Ngaronyi imetengewa shilingi milioni 4 kwa ajili ya sehemu korofi eneo la Samakimaini – Ngoronyi kilomita 2. Na shilingi milioni 5.4 kwa ajili ya matengeneo ya kawaida eneo la Nasai – Samakimaini kilomita 6.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa. Vile vile naomba kuipongeza *TANAPA* kwa kushirikiana na Halmashauri ya Hai katika kusaidia ujenzi wa madaraja hayo ya Siki, Lima na Mese. Pamoja na hayo, ninaomba kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa sehemu kubwa ya barabara hii iliharibika pia kutokana na mvua kubwa zilizonyesha. Je, Serikali inatoa kipaumbele gani hasa kwa Mikoa au Wilaya zile ambazo ziliathirika sana na mvua na mafuriko na barabara zake zikawa katika hali mbaya ikiwemo Wilaya hii ya Hai pamoja na Wilaya ya Muheza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyokwisha kulezwa, kwa upande wa barabara zile za Mikoa na *Trunk Roads*, Serikali ilijitahidi kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kurekebisha barabara zote ambazo zilikuwa katika hali mbaya. Kwa upande wa Barabara za Halmashauri, tulifanya zoezi hilo, lakini kwa kweli kiwango cha fedha kinachohitajika ni kikubwa kuliko uwezo ambao tulikuwa tumeufikiria. Kwa hiyo, tulichofanya tumeziomba Halmashauri zote katika programu ya mwaka huu ya matengenezo ya barabara, wajitahidi kuzingatia maeneo yale korofi na watoe kipaumbele kwa maeneo hayo. Lakini, pili tumejaribu vile vile kupitia *Local Government Transport Porgramme* kwa maeneo yote nchini kutenga kiasi cha fedha ambacho kikitumiwa vizuri, kinaweza vile vile kusaidia sana kupunguza kero katika eneo hilo. Kwa hiyo, kwa upande wa Mkoa wa Kilimanjaro peke yake, tumewatengea shilingi 412,997,763 ambazo zitagawanywa katika Wilaya zake zote kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Kwa upande wa Tanga, bahati mbaya sikuja na takwimu za huko, lakini kama nilivyosema fedha hizi ni kwa kila Mkoa. Kwa hiyo, nitajitahidi nimtafutie kwa upande wa Tanga aone ni kiasi cha fedha chini ya programu hii, ambacho vile vile wangeweza wakakitumia kwa Wilaya yake kuona kiasi gani wanaweza kutumia kwa matengenezo katika maeneo yaliyoharibika sana.

**NAIBU SPIKA:** Labda ingekuwa na kwa Wabunge wote kama ziko namna hiyo! *(Kicheko)*

Na. 127

**Kiwanda cha Chumvi cha Ngaresero**

**MHE. KAIKA S. TELELE;** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba ni-*withdraw* swali hili kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu jana alipokuwa anahitimisha hotuba yake ya bajeti, alijibu kikamilifu sana suala hili na alisisitiza kwamba hicho kiwanda cha chumvi kule *Lake Natron* kitajengwa, kwa hiyo, sina sababu ya kuendelea na swali hili. Ahsante! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana kwa kutupa muda!

Na. 128

**Ukosefu wa Umeme – Mninga na Khanga**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE.BENITO W. MALANGALILA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika vijiji vya Mninga na Khanga ndipo kilipo kiwanda cha kuzalisha nguzo zinazotumika kusambaza umeme nchini; na kwa kuwa ni zaidi ya miaka kumi tangu nyaya za umeme zimepita katikati ya vijiji hivyo; na kwa kuwa vijiji hivyo vina nyumba nyingi nzuri na za kisasa:-

(a) Je, ni lini Serikali itasikia kilio cha wananchi wa vijiji hivyo kuwapatia umeme?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa wananchi hao kwa sehemu kubwa ndio waliopanda msitu huo na wamekuwa wakijitoea kuzima moto kila unapotokea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kuungana na Watanzania wote kwa ujumla wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kutoa pole kwa familia ya marahemu Amina Chifupa Mpakanjia na tunazidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili roho yake ilazwe mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukipatia umeme kijiji cha Mninga, shilingi milioni 44 zinahitajika kukamilisha kazi zifuatazo:-

§ Ufungaji wa Taransfoma mbli zenye ukubwa wa *Kva 100* na *Kva 50*, sawia.
§ Ujenzi wa Volti 400 umbali wa kilomita 4.

Aidha, shilingi milioni 24 zinahitajika ili kukamilisha kazi ya kukipatia umeme kijiji cha Khanga kwa kufanya kazi zifuatazo:-

- Ufungaji wa transfoma moja yenye ukubwa wa *Kva 100*.
- Ujenzi wa laini ya volti 400 umbali wa kilomita 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumla ya gharama ya kutekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo viwili vya Mninga na Khanga ni shilingi milioni 68.0.Baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Mninga na Khanga ni kati ya vijiji ambavyo vimeishafanyiwa makadirio kwa lengo la kuwekewa umeme kama nilivyoeleza kwenye maelezo ya utangulizi. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali na pia hali mbaya ya kifedha ya Shirika letu la *TANESCO*, vijiji hivyo havikuweza kupatiwa umeme. Serikali inatafuta fedha zinazohitajika kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini michango mbali mbali ya wananchi wake ikiwa ni pamoja na kutambua jitihada zilizofanywa na wananchi wa vijiji vya Mninga na Khanga katika kupanda miti na kulinda msitu huo dhidi ya majanga mbali mbali yakiwemo majanga ya moto.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni shahidi toka mwaka 1995, Mheshimiwa Malangalila alikuwa akiulizia suala hili la kupeleka umeme katika vijiji vya Mninga na Khanga. Kwa kweli ni muda mrefu umepita na hakuna sababu za ziada ambazo Serikali inaweza ikatoa wananchi hawa wasipatiwe umeme kwa maana ya kuweka transfoma ya *Kva 100* na kupeleka *service line* ya kilomita 2. Je, Serikali kwa Bajeti hii ambayo itapitisha mwaka huu, watakuwa tayari kuwawekea transfoma hiyo na kujenga *line* ya kilomita 2 ili tuondokane na tatizo la umeme katika vijiji hivi? pili; karibu katika Majimbo yote, kuna matatizo kama haya ya kuweka transfoma katika maeneo ambayo miradi imekwishakamilika. Je, Serikali inasema nini katika kuandaa utaratibu wa kuweka transfoma za ziada ili kukamilisha miradi ambayo haijakamilika kwa ajili ya transfoma?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika jibu la msingi, gharama zinazohitajika katika kupeleka umeme katika vijiji hivyo viwili ni milioni 68. Nafahamu unyeti wa suala hili na Wizara yetu inatambua kwamba Mheshimiwa Malangalila amekuwa akifuatilia kweli kwa muda mrefu sana kufikishiwa huduma ya umeme katika maeneo haya ya vijiji viwili. Lakini, tatizo linalotukabili, nadhani tunakubaliana wote na hili halina ubishi kwamba sungura wetu ni mdogo, ni mdogo na mahitaji ni makubwa kuliko uwezo tulionao sasa hivi. Na wote tunafahamu pia kwamba juhudi za Serikali zimekuwa zikiendelea kwa hatua mbali mbali. Nazidi tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya muuliza swali kwamba Serikali ina nia ya dhati kuhakikisha kwamba inafikisha huduma hii sehemu mbali mbali. Lakini tutakwenda kwa hatua kutokana na jinsi tunavyokuwa na uwezo wa rasilimali ya kifedha kufikisha huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha pili, tunatambua kweli kwamba mahitaji ya umeme katika nchi yetu ni makubwa sana na ni dhahiri kwamba Wizara yetu inalitambua hili kwa sababu kumbukumbu zetu zinaonyesha naweza nikasema kwa ufupi kwamba kila Mbunge ana ombi la kuhudumiwa katika maeneo yake katika Ofisi yetu. Lakini, jibu linabaki kuwa ni lile la msingi kwamba tuna tatizo la kifedha na tunafahamu kwamba kwenye bajeti tutakuwa na miradi ambayo itaonekana ikihudumia baadhi ya maeneo ya Tanzania, lakini si yote. Kwa hiyo, nizidi tu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba mzidi kuamini Serikali inafanya juhudi kadri inavyowezekana kuhakikisha kwamba huduma hizo tunazifikisha mahali pake. Kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah amfikishie salaam Mheshimiwa Benito Malangalila kwamba tuko pamoja, lakini tukubaliane kwamba tutakwenda hatua kwa hatua kutokana na uwezo wa kifedha tulionao nchini.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilituahidi umeme wa Rais Mstaafu wa Marekani, Mheshimiwa Clinton kwenda kwenye zahanati zetu zote; na kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba *World Bank* wataleta umeme wa vijiji vikiwepo vijiji vya Ilamba Mshariki; Ibaga, Nduguti, Mwangeza n.k; Serikali inasemaje juu ya hizi ahadi mbili kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Swali hilo ni kama jipya hivi, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kujaribu maana yake Clinton ni mtu mkubwa kabisa mnaweza kuwa mnakumbuka Wizarani kwenu! Mheshimiwa Waziri Mwenyewe! Naomba muwe *brief!*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba kwa muda mrefu tulikuwa na hili suala la umeme vijijini na ambalo lilikuwa chini ya programu ya *World Bank*. Lakini, bahati mbaya huu mradi ulikuwa ukibadilika badilika kila wakati, maana yake ulianza katika *Energizing Rural Transformation,* sasa umeingia *Rural Expansion Progrmme*. Kila mara ulikuwa unabadilka badilika na mwaka huu bado tuko katika majadiliano na *World Bank* juu ya kutekeleza huu mradi mpana zaidi ya walivyokuwa wamefikiria. Nafikiri ukishakamilika na huu hamtauona kwenye bajeti yetu kwa sababu mawasiliano bado hayajakamilika. Lakini, pindi ambapo yatakuwa yamekamilika, ndipo tutaona kwamba huu mpango unaendelea. Lakini, mbali na hapo tutakapokuwa tunawasilisha bajeti yetu, mtaona kwamba kwa mara ya kwanza tumeona hii miradi ya kutegemea ufadhili kutoka nje mara kwa mara ikikwama, tunachelewesha programu zetu. Kwa hiyo, mwaka huu na sisi tutaanza angalau kidogo tu kuanza kutekeleza hii miradi ya *Rural Energy Transformation*.

Na. 129

**Soko la Uhakika kwa Zao la Korosho**

**MHE. DR. ALI TAARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima wa korosho juu ya zao hilo kutonunuliwa kwa bei iliyowekwa na Serikali:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia wakulima wa korosho soko la uhakika ili isibakie mikononi mwao kama ilivyo sasa?

(b) Je, ni tani ngapi za korosho ambazo zimeishanunuliwa hadi sasa katika msimu huu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali, Mbunge wa Jimbo la Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuwatafutia soko la uhakika wakulima wa zao la korosho, Serikali imejiandaa kutekeleza mipango ifuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa korosho zote zinabanguliwa hapa nchini ili kuondoa ukiritimba wa kuuza korosho katika soko moja tu la India ambalo hununua korosho ghafi. Serikali imekwishaelewana na Chama cha Wenye Viwanda binafsi vya kubangua korosho ili wawezeshwe kubangua korosho zote zinazozalishwa hapa nchini. Maamuzi rasmi ya Serikali juu ya namna ya kuviwezesha viwanda hivyo yatafanywa muda wowote kuanzia sasa.

(ii) Kuanzisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za mazao maghalani kwenye zao la korosho kuanzia msimu wa 2007/2008. Mfumo huu utawezesha wakulima wa korosho kupata mkopo kutoka vyombo vya fedha wa hadi asilimia 60 ya thamani ya mazao watakayokuwa wamehifadhi katika ghala. Utaratibu huu pia utaviwezesha viwanda vya kubangua korosho kupata malighafi muda wote wa mwaka kwa kuwa wataweza kuhifadhi korosho ghafi watakayopokea toka kwa wakulima. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine imeanza kuhamasisha wakulima juu ya matumizi ya mfumo huu mpya ili uanze kwa mafanikio.

(iii) Kuimarisha vyama vya ushirika nchini kwenye maeneo husika ili viwe vyama imara vyenye uwezo wa kununua mazao ya wakulima. Vyama vya Ushirika vilivyo imara ni ufumbuzi wa matatizo mengi yanayohusiana na masoko ya mazao ya wakulima wa korosho na mazao mengine kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2007, kiasi cha tani 92,342.4 kilikuwa kimenunuliwa, ikiwa ni asilimia 83 ya lengo la tani 110,000 zilizovunwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Naibu Waziri, aliyeuliza swali ni Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali!

**MHE. DR. ALI TAARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kulitaja jina langu kwa usahihi. Pili, mwezi wa Februari mwaka huu nikiwa katika Kata ya Ngorongo, Rufiji, wakulima wengi walilalamika ya kwamba korosho zao zinanunuliwa na mfanyabishara mmoja kupitia wakala wake kwa bei ya shilingi 250/=

kwa kilo (Risiti ninazo). Je, vyombo vya dola vilivyoko chini kwenye vijiji vinaangalia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**MHE. DR. ALI TAARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani! Zinanunuliwa shilingi 250/= kwa kilo. Lakini risiti zinaandikwa shilingi 480/= kwa kilo!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la ukiritimba wa ununuzi korosho ghafi, kusema kweli ndio lililosababisha na hata matatizo mengine ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Mbunge. Kwa ujumla tu niseme kwamba kitendo cha kununua korosho kwa kughushi ni tendo la kosa la jinai ambalo kwa ujumla wake tunatakiwa tushirikiane sote kukabiliana nalo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wale wote walioathirika na tatizo hili kutoa taarifa kwa vyombo vya dola vinavyohusika ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua zinazostahili, kwa sababu kama unanunua korosho kwa bei tofauti na unatoa risiti tofauti, huku ni kughushi na ni kosa la jinai.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mie kuuliza swali moja la nyongeza: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo tu; Kwa kuwa suala la bei ya korosho, inaonekana ndio tatizo kubwa na hapa ilitolewa kauli na Mheshimiwa Kiongozi Mkuu wa Serikali ndani ya Bunge letu, Mheshimiwa Waziri Mkuu alieleza hapa kuwaambia wale wanaonunua korosho wanunue kwa bei ambayo wamekubaliana na wakulima. Lakini inaonekana bado hakuna nidhamu katika manunuzi haya; Je, Serikali inafuatiliaje vitu kama hivi, anaposema Waziri Mkuu jambo kama hili, halafu inaonekana watu wanalipinga, Serikali inafanyaje katika mazingira kama haya?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Naibu Waziri wa Viwanda, Bishara na Masoko maelezo fasaha aliyoyatoa kuhusu tatizo la ununuzi wa korosho. Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo hili. Mwaka jana kulikuwa na matatizo makubwa na Serikali ilishiriki kikamilifu katika kusimamia ununuzi wa zao la korosho ili kuondoa tatizo hilo. Lakini, kusema ukweli tatizo lenyewe ni *complex*. Kwa mfano, alipokuwa anazungumzia Mheshimiwa Mbunge Dr. Taarab pale kwamba watu wananunua 250, wanapewa 480, hii kusema kweli ni *collaboration* kwa sababu ilikuwa kali katika kufuatilia bei gani ambayo mkulima anapewa na kwa hiyo, ikabidi wakulima wachache wawe wana-*collaborate* na wanunuzi katika kufanya ujanja huo alioueleza. Lakini, kutokana na mafunzo tuliyoyapata katika tatizo la mwaka jana, ndiyo maana maelezo aliyoyatoa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko ni hatua madhubuti zinazochukuliwa ili kuondosha tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Vyama vya Ushirika, tumeanzisha na tumesaidia sasa Vyama vya Ushirika vya Korosho katika Wilaya ya Tunduru, Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Pwani Tunachukua hatua ya kuviimarisha Vyama vya Ushirika, ili inapofika mwezi wa kumi mwaka huu 2007 ununuzi wa korosho uwe

unafanywa na vyama vya ushirika, ndiyo vinakutana na Mkulima moja moja. Pamoja na hatua zingine zote ambazo zinaelezwa juu ya kuhifadhi katika maghala na stakabadhi ili kumwepusha mkulima mdogo asikutane na mnunuzi anayetaka kumdhulumu. Hizi ni hatua madhubuti ambazo Serikali inachukua na tunadhani tatizo hili litapungua kwa kiasi kikubwa katika msimu unaokuja. *(Makofi)*

Na. 130

**Huduma ya Mawasiliano ya Treni**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Mikoa ya Pwani, Morogoro, Iringa na Mbeya wanahudumiwa na Shirika la *TAZARA* kwa kiwango kikubwa kama njia muhimu ya usafiri na usafirishaji wa mizigo; na kwa kuwa katika miaka ya nyuma Shirika hilo lilianzisha safari fupi fupi kati ya Stesheni za Mkamba, Mlimba na Makambako, zilisadia kupunguza msongamano wa wasafiri katika treni za abiria:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwarudishia wananchi huduma hizyo ili kuwezesha kusafirisha mali na mizigo yao bila adha ya kwenye treni za abiria kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa wa Kilombero, kama ifutavyo:-

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa wa Kilombero, kama ifutavyo:-

Ni Kweli Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* ilikuwa na huduma ya treni kati ya kituo cha Mkamba na Stesheni ya Mlimba na Makambako, maarufu kwa jina la KIPISI. Huduma hiyo, pamoja na umuhimu uliokuwepo, ilisitishwa kutokana na uhaba mkubwa wa injini za treni ulioifanya *TAZARA* kutumia injini zenye uimara hafifu kiufundi na hivyo kuwa hatari kwa usafiri.

Aidha, suala la uhaba wa injini za treni limeendelea kuwa tatizo hadi sasa na kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za uendeshaji na utendaji wa Mamlaka kwa ujumla ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa huduma hii. Kwa kutambua na kuzingatia umuhimu wa huduma hii, Mamlaka itaangalia uwezekano wa kuanzisha huduma hii tena pindi hali ya *Locomotives* itakapoimarisha kiufundi na kwa idadi. Wananchi wa sehemu hizi wanashauriwa kutumia huduma ya treni ya kawaida *Ordinary Passenger Service* ambayo inatoka Dar es salaam kila siku ya Jumanne na Ijumaa na Tunduma kila Jumatano na Jumamosi.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa miundombinu kwa maana ya barabara kuanzia Kidatu, Ifakara mpaka Laela imeharibika sana katika msimu huu wa mvua kiasi cha kufanya usafiri wa magari kuwa mgumu; na kwa kuwa kuanzia Stesheni ya Mlimba hadi Uchindile hamna njia nyingi za usafiri, isipokuwa kwa treni.

Je, kwa kutumia vichwa vilivyopo, waziri anaweza kuishauri Mamlaka iongeze safari angalau moja ili ziwe nne kwa wiki badala ya tatu?

(b) Kwa kuwa muda wa kushusha abiria na kupakia umekuwa mdogo sana kwa kuzingatia kwamba safari hizo wanafanya watu wa rika zote. Je, Waziri ataishauri mamlaka kuongeza dakika za kupakia na kushusha abiria kila *station* ili kusizue matatizo ya ajali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, najua masuala ya barabara kuwa mbovu kutoka Kidatu, Ifikara na sehemu nyingine na juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuboresha barabara hizo. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hali yetu ya reli ikiwa nzuri tutaweza kuongeza safari hizo. Lakini hivi sasa ni ngumu kwa sababu *locomotive* tulizonazo ni 14 tu haziwezi kuhimili *return around* ya shughuli hizo kwenda na kurudi. Pili, tutaona uwezekano wa kuongeza dakika chache lakini ikumbukwe kwamba treni hizi zinapita katika *station* nyingi sana. Kama kila mahali tutakuwa tunaongeza safari muda wa dakika ina maana hawa wanaokwenda safari zao hawatafika kwa wakati ambao wangeutegemea. Lakini kutokana na ombi lake tutalipeleka tuone uwezekano wa kusaidia.

Na. 131

**Matatizo ya Usafiri Kando Kando ya Ziwa Nyasa**

**MHE. CAPT. JOHN KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya usafiri kwa wananchi waishio kando kando ya Ziwa Nyasa kuanzia Kyela, Ludewa hadi *Mbamba Bay* ni ngumu sana tangu wakati wa uhuru hadi sasa; na kwa kuwa kwa sasa kuna boti moja tu inayoitwa *MV. Iringa* ambayo inasafirisha abiria na mizigo kwa pamoja, hali inayoweza kusababisha ajali ikizingatiwa boti hiyo imechakaa sana.

Je, Serikali ina mipango gani ya muda mfupi wa kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hali ya usafiri kwa wananchi waishio kando kando ya Ziwa Nyasa, kuanzia Ludewa, hadi *Mbamba Bay* ni ngumu. Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi waishio kando kando ya Ziwa Nyasa kwamba pamoja na meli hizo kuwa zimechakaa zinakarabatiwa ipasavyo ili ziendelee kutoa huduma, Serikali kupitia Kampuni ya Hudumza za Meli huzifanyia matengenezo *(Scheduled Maintenance)* meli za *MV. Iringa* na *MV. Songea* kama ifuatavyo:-

*MV. Songea* ambayo ina uwezo wa kubeba abiria 212 na mizigo tani 40, ilifanyiwa matengenezo makubwa mwezi Februari 2005 nchini Malawi na kwa sasa inaendelea kufanya kazi katika hali nzuri. Meli hii inatarajiwa kufanyiwa matengenezo mengine makubwa kuanzia mwezi Agosti, 2007 yanayotarajiwa kugharimu jumla ya Tshs.185 milioni ili kuboresha utendaji wa meli hiyo katika kutoa huduma zake. Aidha, vipuri vyote kwa ajili ya matengenezo ya mitambo vilikwishaagizwa kutoka nje ya nchi na tayari vimewasili nchini. *MV. Iringa;* ambavyo ina uwezo wa kubeba abiria 138 na mzigo tani 5, ilifanyiwa matengenezo makubwa kuanzia Novemba 2006 hadi Januari 2007. Aidha, matengenezo hayo yaliyogharimu kampuni hii kiasi cha Tshs.122 milioni yameshakamilika na tayari meli hiyo imeanza kazi rasmi tangu mwezi Mei, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Meli za *MV. Songea* zimetengenezwa kwa ajili ya kubeba mizigo na abiria kwa wakati mmoja. Mizigo hiyo hupakiwa sehemu maalum *(Cargo Hatch)* na hivyo kutochanganywa kabisa na abiria. Katika kubeba abiria na mizigo tahadhari zinazostahili zinachukuliwa ili kuepusha uwezekano wa ajali kutokea. Aidha, katika safari zote zilizowahi kufanywa na meli hizi, haijawahi kutokea hali ya wingi wa mizigo hadi kufikia ukomo wa uwezo wa meli hizi na hivyo kusababisha meli hizo kupakiwa kwa kuchanganya mizigo na abiria pamoja. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu. kwamba uongozi wa Kampuni ya Huduma za Meli unasimamia kwa karibu uendeshaji wa meli hizi ili kufanikisha uendeshaji salama wa meli zenyewe na abiria kwa ujumla.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali mwaka jana iliahidi kununua meli kubwa ambayo itakidhi mahitaji ya usafiri wa Ziwa Nyasa:-

(a) Je, ile ahadi ya meli kubwa sasa ipo ama imetoweka?

(b) Kwa kuwa kituo cha kushushia watu cha Ndumbi kilifungwa miaka minne iliyopita kwa sababu mchanga na mawe yamejitokeza katika kituo hicho na Serikali iliahidi kukitengeneza. Je, ni lini kituo hicho kitafanya kazi ili kuwapunguzia adha ya usafiri wa wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikumbuki kwamba tuliahidi Bunge hili Tukufu kununua meli

kubwa lakini tulitoa ahadi kwa yeyote ambaye anaye nia ya kuwekeza katika uendeshaji wa meli basi ruhusa inatolewa kwa sababu ni sera ya Serikali kujinasua katika kuendesha shughuli za kibiashara na sekta binafsi inachukua nafasi yake. Napenda nimwombe Mheshimiwa Mbunge, kama yupo mtu yeyote ambaye anayo nia ya kuwekeza katika masuala ya meli kama yanavyofanya katika *Lake Victoria* basi tuko tayari kumpa msaada wa kufanikisha shughuli hiyo.

Pili, nakubaliana naye kwamba kituo cha Ndumbi kimejaa mchanga kama vituo vingine vile vile. Kwa mfano *Itungi Port* na sehemu nyingine. Tatizo kubwa linalotukabili ni kupata fedha kwa ajili ya kutoa mchanga. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha ikipatikana tutaweza kuchimba na kutoa mchanga siyo Ndumbi tu lakini *Tungi Port* na sehemu nyingine. Nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Capt. Komba kwa kufuatilia kwa karibu zaidi matatizo yanayokera wananchi wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea maana tulionyeshwa boti moja sidhani kama ndio meli yenyewe. *(Kicheko)*

Na. 132

**Hitaji la Kituo cha Polisi Mvuha**

**MHE. HAMZA MWENEGOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Morogoro Kusini, ni kubwa sana – Kwani linaanzia Kibungo chini (katika Tarafa ya Matombo) na kupakana na Liwale-Kusini na Kisarawe Kusini Mashariki, pamoja na Mikumi – Magharibi na kwa kuwa, kuna kituo kimoja tu cha polisi cha Matombo:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuweka katika Bajeti yake ya 2007/2008 ujenzi wa Kituo cha Polisi Mvuha?

(b) Je, Serikali iko tayari kuwapa usafiri askari wa Matombo wanaotembea mwendo mrefu kwa miguu wakiwa wamebeba silaha?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua ukubwa wa jimbo la Morogoro Kusini kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kwa sasa haitaweza kuweka katika Bajeti yake ya mwaka 2007/2008 ujenzi wa Kituo cha Mvuha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya vituo vya polisi Serikali kupitia Jeshi la Polisi inafanya tathmini kujua mahitaji halisi ya vituo vya polisi nchini kutokana na vigezo vinakubaliana kipolisi ili iweze kujenga vituo hivyo hatua kwa hatua kadri Serikali itakavyopata uwezo kifedha ili hatimaye kumaliza tatizo la mahitaji ya vituo vya polisi hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufanya tathimini ya mahitaji ya vituo vya polisi zoezi hilo linakwenda sambamba na kujua mahitaji mengine muhimu kwa utendaji wa Jeshi la Polisi yakiwemo magari na pikipiki. Serikali kupitia bajeti yake ya kila mwaka itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kununua magari na pikipiki hatua kwa hatua ili kumaliza matatizo ya usafiri yanayolikabili Jeshi la Polisi. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati tunaendelea kulipatia ufumbuzi tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wakazi wa Mvuha wataendelea kupata huduma ya polisi kutoka Kituo cha Polisi cha Kisaki na Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro na vituo vya polisi vya Matombo. Aidha, Jeshi la Polisi litaendeleao kuimarisha doria, kufanya misako na kutumia mbinu mbalimbali za kiulinzi ili kuhakikisha hali ya usalama katika eneo hilo.

**MHE. HAMZA MWENEGOHA:** Kwa kuwa mwaka jana tuliomba usafiri na bahati nzuri Serikali ikatufikiria kutupa usafiri lakini baadaye ikaonekana Makao Makuu ya Mkoa yalihitaji sana usafiri zaidi. Kwa hiyo, gari ile ikabaki Makao Makuu ya Mkoa, Morogoro Mjini na wao wanatusaidia kuja. lakini kutokana na ukubwa wa jimbo hili, wale *police officers* ambao wako kwenye doria anayozungumza ni doria ya miguu ya kwenda kilomita 70 hadi 80 huku wamebeba silaha.

(a) Je, ili na sisi tuweze kuwasaidia polisi hawa hamuwezi basi angalau kuwapa pikipiki ili na sisi tuweze kutia mafuta mara nyingine?

(b) Mimi ningemwomba Mheshimiwa Naibu Waziri apange safari aone hali halisi ya jimbo hili labda itasaidia vile vile kwa Serikali kuona umuhimu wa kuwasaidia polisi hao. Je, Mheshimiwa Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kuja jimboni Morogoro Kusini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa heshima kubwa kabisa napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mwenegoha mara tutakapopata pikipiki kipaumbele cha kwanza tutapelekwa katika kituo hiki ambacho Mheshimiwa Mwenegoha amesema. (*Makofi*)

Kuhusu suala la pili, kwanza napenda nimshukuru nataka nimhakikishie itakuwa tayari mara tu baada ya kipindi hiki cha Bajeti twende jimboni kwake tukatembelee maeneo yote hayo. (*Makofi*)

Na. 133

**Matatizo yanayowakabili wakulima wa tumbaku**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwanzoni mwa mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa agizo kwamba ifikapo mwaka 2010 uzalishaji wa tumbaku uwe umeongezeka kutoka tani 47,000 Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika aliunda Tume ya kuchunguza mwenendo mzima wa zao hilo hasa baada ya kubaini kuwa, wakulima wa zao hilo wanakabiliwa na matatizo makubwa na mapato kidogo sana jambo linalohatarisha ukuaji na uzalishaji.

Je, tume iliyoundwa imegundua nini?

**NAIBU WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID MATHAYO DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Kwa kufuatilia agizo la Waziri Mkuu, alipotembelea Mkoa wa Tabora mwezi Mei 2006, Wizara yangu iliunda Kamati kwa ajili ya ya kufanya uchambuzi kuhusu malalamiko ya wananchi kuhusiana na mapunjo katika malipo ya tumbaku yao katika maeneo yafuatayo:-

(i) Gharama za uzalishaji na bei za ununuzi wa tumbaku;

(ii) Upatikanaji na matumizi ya mbolea;

(iii) Hali ya soko la tumbaku; na

(iv) Majukumu ya vyama vya ushirika na taasisi zinazoshugulikia zao la tumbaku.

Hadidu za rejea ziliitaka Kamati hiyo itoe mapendekezo ya namna ya kuboresha kilimo cha tumbaku nchini pote hususan Mkoa wa Tabora. Kamati hii katika uchunguzi wake ilibaini yafuatayo:-

(a) Kuna kutoelewana baina ya wakulima na wanunuzi kuhusu gharama za wanunuzi wa tumbaku. Wakati wakulima wanakadiria gharama za uzalishaji kuwa ni wastani wa shilingi 2.27 milioni kwa hekta, makadirio ya wanunuzi ni shilingi 1,504 milioni kwa hekta.

(b) Pembejeo zinatolewa na wanunuzi kwa wakulima, kupitia vyama vya ushirika vya msingi kwa udhamini wa Chama Kikuu (*Union*) hutolewa kwa riba isiyojulikana na hivyo kusababisha makato mengi na hivyo mkulima kubakia na asilimia 40 tu ya bei katika soko la dunia.

(c) Mfumo wa vyama vya ushirika unakuwa ni wa mawakala wa wanunuzi, badala ya kuwa vyama vya kuhudumia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitoa mapendekezo mengi yakiwemo yafuatayo:-

(a) Kuitaka Wizara kutathmini gharama halisi za uzalishaji ili kuondoa utata uliopo baina ya wakulima na wanunuzi.

(b) Mikataba iliyopo ya wanunuzi kuwakopesha wakulima pembejeo bila kueleweka gharama za riba inawabebesha wakulima mzigo mkubwa na kuwakatisha tamaa. Aidha, utaratibu wa kuwaadhibu wakulima waaminifu wanaouza mazao kupitia vyama walivyokopa kufidia deni la waliotorosha tumbaku yao na kuuza mahali pengine unawakatisha tamaa wakulima waaminifu.

(c) Wakulima wa tumbaku walihimizwa kuanzisha *SACCOS* ili wawe na mfumo wa kuweka akiba na kujipatia mikopo nje ya mfumo wa wanunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeanza kuifanyia kazi taarifa hiyo ya Kamati na imekwishakutana na wadau wa tumbaku kupitia vikao vya Halmashauri na kutoa maagizo maalum kwa viongozi na wakulima. Aidha, Wizara yangu imekutana na viongozi wa Chama Kilele cha Wakulima wa Tumbaku na Mameneja wa Vyama vya Mkoa na kukubaliana hatua za kuchukuliwa ili ushirika kupitia mabenki uwe na uwezo wa kuagiza na kusambaza pembejeo za tumbaku ili kuachana na kutegemea makampuni ya wanunuzi wa tumbaku katika kupatiwa pembejeo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha yanayowasibu wakulima wa tumbaku nchini. Pamoja na majibu hayo sahihi nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba tatizo ni kubwa na hasa kwenye pembejeo ambapo makampuni yanawakopesha pembejeo wakulima kwa bei ambazo hazijulikani.

(a) Je, huo utaratibu wa vyama vya ushirika pamoja na Wizara kuweza kukapa hela kwenye mabenki ili kuwanunulia wakulima pembejeo utaanza msimu huu wa 2007/2008?

(b) Kwa kuwa Nchi ya Malawi ilichukua mbegu za tumbaku kutoka Urambo miaka ya 60 sasa hivi nchi ya Malawi inatoa tani 200 za tumbaku, wakati Tanzania inatoa tani karibu 50 za tumbaku na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, jana amesema akitoa mfano kwamba Kenya, Masai Mara ni eneo dogo wana vitanda zaidi ya 4000 na Tanzania ina eneo kubwa vitanda 900 na akahimiza Mheshimiwa Waziri mkuu kwamba lazima na sisi tufikishe vitanda 4000. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuinua uzalishaji wa zao la tumbaku ili tuweze kuipita Malawi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika jibu la msingi tunatambua hilo tatizo tunalifanyia kazi. Kusema kweli mwaka huu tulikuwa tumekusudia kushirikiana na benki ya *CRDB* ili kuanza utaratibu wa kuwakopesha wakulima wa tumbaku mbolea moja kwa moja badala ya kupitia kwa wanunuzi. Lakini kwa sababu benki hiyo ilikuwa haiko tayari kwa mwaka huu tumekubaliana nayo iendelee na mchakato huo, ili tuanze utaratibu huo katika msimu unaokuja wa kilimo. Tunadhani tatizo ni kubwa na tulihitaji muda wa kutosha kuweza kuishughulikia. Kuhusu suala la uzalishaji mdogo tunatambua ya kwamba uzalishaji wa zao la tumbaku na mazao mengine nchini uko chini ukilinganisha na nchi jirani zetu ikiwemo Malawi. Kwa hiyo, hatua tunazozichukua moja ni pamoja na kuhakikisha pembejeo zinafika kwa gharama nafuu ili kuwatia moyo wazalishaji lakini vile vile tunapeleka maafisa wa ugani ili waweze kuwafundisha wakulima wa tumbaku na mazao mengine namna ya kuongeza uzalishaji ili tuweze kushindana na uzalishaji katika nchi hii jirani na kuongeza mapato ya wakulima. *(Makofi)*

Na. 134

**Kiinua Mgongo kwa Askari Wastaafu**

**MHE. BAHATI ALI ABEID** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi hunyanyasika sana wanapostaafu kwa kupata kiinua mgongo chao kwa kuchelewa sana:-

(c) Je, utaratibu gani anatakiwa afuate askari anayestaafu ili apate kiinua mgongo chake mara tu anapostaafu?

(d) Je, kuna sheria yoyote inayomlinda mstaafu kupata kiinua mgongo kwa wakati muafaka?

(e) Je, mstaafu anatakiwa kupata kiinua mgongo chake baada ya muda gani tangu astaafu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge Viti Maalum, lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, askari anayestaafu ili apate kiinua mgongo chake mara tu anapostaafu anatakiwa kutoa taarifa kwa mwajiri wake miezi sita kabla ya kustaafu akimjulisha azima yake ya kustaafu na mwajiri pia anatakiwa awasilishe Hazina majalada ya mstaafu mtarajiwa huyo yakiwa na kumbukumbu zote zinazohitajika, miezi mitatu kabla ya tarehe ya kustaafu kuwapa ili kuwapa Hazina muda wa kuandaa malipo na kukaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (*CAG*). Muda huo ni muafaka

kwa shughuli hizo zote kukamilika na kumwezesha mstaafu kupata malipo yake mara tu anapostaafu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya pensheni inamlinda Mstaafu kupata kiinua mgongo kwa wakati muafaka kama atatimiza taratibu zinazotakiwa ili kulipwa mafao ya pensheni.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu (a), Mstaafu anatakiwa kupata kiinua mgongo chake mara tu baada ya kustaafu. Lakini mara nyingi wastaafu wengi hupata malipo baada ya muda hata wa miezi mitatu au zaidi kutokana na ucheleweshaji wa kuwasilisha majalada ya wahusika na mara nyingi upungufu wa nyaraka katika majalada hayo.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mstaafu anakuwa amefanyiwa taratibu zote zinazompasa kufanyiwa mstaafu, lakini kuna wastaafu wengi ambao mpaka leo ni miaka mingi hawajapata kiinuo mgongo chao na kwa kuwa wao siyo wenye matatizo ya kupeleka majalada hayo panapohusika. Je, ni hatua gani zitachukuliwa kwa wale wafanyakazi ambao wanachelewesha majalada hayo ya wastaafu hawa na wanawapatia matatizo makubwa kwa kuchelewesha kupata viinua mgongo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Watafanyiwa nini hao ndugu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi tatizo kubwa haliko Hazina. Tatizo kubwa liko kwa ama mwajiriwa mwenyewe kwa kutoa taarifa wakati unapotakiwa au mwajiriwa wake yaani pale ambapo alipokuwa polisi kutoleta Hazina majalada yanayotakiwa. Kama hayo yakitimizwa hakuna tatizo kabisa mtu analipwa kwa wakat. Akimaliza tu, akistaafu tu, katika muda wa wiki mbili anaweza akapata *cheque* yake.

**MHE. RAJAB MOHAMED SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa waajiri ndiyo wajibu wao kufanyakazi hiyo si kazi ya mwajiriwa. Sasa Serikali inatoa kauli gani kwa waajiri ili kuharakisha wasisumbuke wastaafu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, nyaraka zinazohitajika baadhi zinatakiwa zitolewe na mwajiriwa kwa mfano barua yake ya awali ya kuajiriwa, cheti chake cha kuzaliwa, barua zake za kupandishwa cheo na kadha wa kadha. Kwa kawaida vitu hivi waajiriwa wengi huwa wamevipoteza. Kwa hiyo, inabidi mwajiri yule ajaribu kutafuta kila namna ya kuvipata hivyo ili aviwasilishe hazina. Kwa kweli tunajitahidi Hazina kwa kadri inavyowezekana pamoja na kutafuta mafaili kwenye *archives* ili kuwasaidia hawa. Lakini maadam matatizo yamejitokeza hazina itaangalia uwezekano wa kuweza kuona jinsi gani tutaweza kuwasaidia waajiriwa. (*Makofi*)

Na. 135

**Kodi kwa mifuko ya pensheni**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (MHE. AMEIR ALI AMEIR)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni kawaida kutopewa ruzuku ya Serikali kwa Mifuko ya Pensheni na kwa kuwa hujienesha kwa michango ya wanachama wake na huwekeza kwa ajili ya kujiongezea kipato:-

(a) Je, ni kwa nini Mifuko ya Penshejni inalazimika kulipa kodi wakati mifuko hiyo haifanyi biashara?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuitoza kodi mifuko hiyo ni kuipunguzia uwezo wa kifedha?

(c) Je, ni sababu gani zilizosababisha kutozwa kodi kwa mifuko hiyo na ni sheria gani ya nchi inaruhusu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Pensheni, kama mwekezaji yoyote hulazimika kulipa kodi kwenye mapato yatokanayo na vitega uchumi vyake kama vile mapato yatokanayo na majumba ya biashara, ofisi za kukodisha kibiashara na mahoteli, gawio *(Dividends)* zinazotokana na hisa kwenye makampuni mbalimbali, faida kutokana na Hati Fungani *(Treasury Bills and Bonds)* pamoja na faida itokanayo na dhamana kwenye mabenki *(Bank deposits).* Aidha, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, kuwa Serikali haitozi kodi, kutoka kwenye michango ya wanachama kama nilivyoeleza. Kodi inayotozwa ni ile ambayo inatokana na mapato ya vitega uchumi husika, na hii inafanyika ili kuleta usawa *(equity)* katika kulipa kodi kwenye mapato yatokanayo na biashara moja.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, haipunguzii uwezo wa kifedha Mifuko hiyo kwa kuitoza kodi Mifuko ya Pensheni, Serikani inaweka mazingira sawa kwa ushindani kwa washiriki wote katika biashara ambazo mifuko hiyo huamua kuwekeza.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazoruhusu kutoza kodi Mifuko ya Pensheni ni sheria zile zile ambazo hutumika katika kutoza kodi kwenye Makampuni na Taasisi nyingine kama vile Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 na Sheria ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) ya Mwaka 1997 pamoja na Sheria nyingine za Kodi ziizopitishwa na Bunge.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri, kwa kujibu vizuri swali hili lililoulizwa hivi karibuni. Sasa kwa kuwa kuanzia

mwaka huu wa fedha Serikali imeamua kwamba wastaafu wote watalipwa mafao yao ya pensheni kupitia *NSSF, PPF, LAPF* na kadhalika.

(a) Je, Serikali imejiandaa namna gani katika kutekeleza utaratibu huu, wastaafu watakwenda kufuata fedha zao kwenye mifuko hii ya pensheni au watakwenda wapi na katika Wilaya au Mikoa ambao Ofisi za mifuko hii haipo. Je, kutakuwa na utaratibu gani wa malipo hayo? (*Makofi*)

(b) Kwa nini mifuko ya *PPF* na *NSSF* wanakuwa wagumu sana kuwakopesha wanachama wao ila inakuwa rahisi kwa mikopo hiyo kupatiwa watu ambao si wanachama na mifano ipo kadhaa. Je, utaratibu huu Serikali itaendelea nao na hasa inasema nini kuhusu hili? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kuhamisha ulipwaji kwa wastaafu wa Serikali kwenda kwenye mifuko ya pensheni, Serikali ilikuwa na mjadala na mashirika haya karibu mwaka mzima. Kwa hiyo, utaratibu umeandaliwa wa jinsi gani, wale wastaafu kwanza ieleweke kwamba fedha za wastaafu hawa bado ni jukumu la Serikali. Mashirika haya yatatumika kama wakala.

Kwa hiyo, waki-*process* yale maombi ya pensheni watapeleka hazina ili hazina iwalipe mashirika yale na mashirika yale yawalipe. Kwa hiyo, siyo mashirika haya yatakayotumia fedha zake. Ni fedha za Serikali Kuu, ila tunatumia mashirika haya yenye uzoefu kama wakala ili kuwapunguzia adha wastaafu wa Serikali.

La pili, mikopo kwa wanachama ni kweli kwamba yako mashirika yanayokopesha wafanyabiashara lakini vile vile yako mashirika ambayo tayari yameanza kuwakopesha wanachama wao.

Kwa mfano, *PPF* imeanza mpango kabambe wa kujenga nyumba za bei nafuu ambazo zitakopeshwa kwa wanachama wao waliomo katika mfumo wa *PPF*. Sasa wanachama wengine tutajaribu kuona kama kuna uwezekano lakini kwa kweli kwa sababu mabenki yako mengi tungeshauri kwa kweli mwenye uwezo wa kukopa ni vizuri akaenda kwenye vyombo vya fedha vinavyoruhusiwa kukopesha akakopa kule.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona. Swali langu nauliza wale walimu wa MEMKWA ambao utaratibu wao ulianzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu, je, wanastahili pensheni au kukopeshwa na kama ni hivyo ni kwa nini wanaendelea kulipwa shilingi 20,000 na hawajalipwa kwa miezi sita hivi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe, ukisoma swali la msingi linazungumzia mifuko ya pensheni, sasa hilo ni nje kabisa. Kwa hiyo, nasikitika sana, labda uliulize kwa maandishi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maswali tuliyokuwanayo tumeyamaliza na muda umemalizika.

Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane. Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 3 kutakuwa na kikao saa 5 asubuhi hii katika chumba namba 227 ghorofa ya pili Jengo la Utawala.

Tunao wageni ambao tungependa kuwatambulisha, kwanza kabisa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Manejiment ya Utumishi, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, anapenda kututambulisha binti zake waliokuja kushuhudia wakati Waziri anatoa hotuba yake, bi. Ina Ali na mdogo wake, wasimame.

Halafu na Ndugu Nasra Yahya. Wamekuja kumsindiza mama. Tuna wageni wengine wa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zabein M. Mhita. Napenda tuwatambulishe wageni wake, Ndugu Godfrey Kilongo, ambaye ndiyo Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Intila iliyoko Kondoa. Ahsante Mwalimu Mkuu, tunaomba uendelee kuwafundisha watoto wetu. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni wengine wanafunzi wa Chuo cha *Assemblies of God,* wasimame wote kama wapo, karibuni sana. Tuna wageni wengine wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Ilunda Kiomboi Singida, kama wapo nao wasimame. Naona watakuja kesho. Ahsante sana naona hawajafika watafika kesho. Baada ya kusema hayo, nadhani tunaendelea na kazi. Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008
### Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

**NAIBU SPIKA:** Jana tulipoahirisha kikao Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, alikuwa amewasilisha hotuba yake. Wenyeviti wanaopaswa kutoa maoni ya Kamati walikuwa bado, sasa tunao Wenyeviti wawili. Kwanza tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala. *(Makofi)*

**MHE. TATU M. NTIMIZI (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha leo salama usalimini, kuendelea na kazi zetu. Kabla sijazungumza lolote kuhusu kuwasilisha taarifa, naomba niungane ...

**NAIBU SPIKA:** Kabla hatujaendelea, naomba niku-*disturb.* Kamati ya Uongozi watakutana katika Ukumbi wa Spika saa 7.00 baada ya kuahirisha kikao hiki. Mheshimiwa tafadhali anza tena.

**MHE. TATU M. NTIMIZI (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Kwa niaba ya wapiga kura wangu wa jimbo la Igalula na mimi mwenyewe naomba niungane na wananchi wote ambao tumefadhaika kwa msiba uliotupata wa kijana wetu, mwanetu, Mbunge mwenzetu, Amina Chifupa. Mwenyezi Mungu, amlaze mahali pema peponi. *Ina-lilahi waina-ilaihi rajiun.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Ikulu, Fungu 30 – Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa Fedha 2007/2008 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili. Aidha, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa kazi zilizofanywa na ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 Juni, 2007 Kamati yangu ilitekeleza kazi ya kujadili Bajeti ya Ofisi ya Rais, kwa kupokea maelekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na utekelezaji wa kazi zilizofanywa kwa mwaka wa fedha uliopita. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, akisaidiwa na Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii.

Kiasi cha fedha kilichotengwa na majukumu yaliyotekelezwa katika Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu katika mwaka wa Fedha 2006/2007, ilitengewa jumla ya shilingi 5,550,756,800 kwa Fungu la 20 kwa Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007, Fungu hilo lilikuwa limepokea na kutumia jumla ya shilingi 4,625,630,600. Aidha, Fungu la 30 lilitengewa jumla ya shilingi 125,863,118,000, kati ya hizo shilingi 91,077,278,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 34,785,840,000 Fedha za Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007 kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumiwa kwa Fungu hilo ni shilingi 75,847,259,132 kwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 32,400,778,336 kwa ajili ya Fedha za Maendeleo na kufanya jumla fedha zilizopokelewa kuwa shilingi 108,248,037,498.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** pamoja na mambo mengine, fedha hizi zilitumika kugharimia utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Majukumu hayo yanahusu siasa na uhusiano wa kijamii, masuala ya utumishi, utawala bora, tuzo za taifa, ajira, rufaa za watumishi wa umma zinazowasilishwa kwa Rais na kwa Katibu Mkuu Kiongozi; kuhudumia Baraza la Mawaziri, pamoja na Kamati zake na Kamati ya Makatibu Wakuu na Kamati zake; kufuatilia utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya Rais na Baraza la Mawaziri pamoja na kuchambua nyaraka na kushauri kuhusu rasimu za miswada mbalimbali ya Serikali; kushughulikia masuala ya Usalama wa Taifa; Ujenzi wa Makazi ya Rais; kuratibu miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* pamoja na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, tarehe 7 Juni, 2007, Kamati yangu ilitembelea Ikulu, Dar es Salaam, kukagua makazi ya Ofisi ya Rais na kujionea utekelezaji wa baadhi ya shughuli zilizotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha uliopita. Kamati imeridhika na kiwango kilichofikiwa cha ujenzi huo na shughuli nyingine zilizopangwa kutekelezwa kulingana na fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 32, ilitengewa jumla ya shilingi 58,430,104,500, kati ya hizo shilingi 9,122,546,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 49,307,558,500 kwa ajili ya Fedha za Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007, Fungu 32 lilikuwa limepokea na kutumia jumla ya shilingi 43,362,701,026, shilingi 10,407,759,026 zikiwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 32,954,942,000 zikiwa Fedha za Maendeleo.

Aidha, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 33, ilitengewa jumla ya shilingi 1,249,076,000 zikiwa Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007 Fungu 33 lilikuwa limepokea na kutumia jumla ya shilingi 824,829,105 zikiwa Matumizi ya Kawaida. Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94, ilitengewa jumla ya shilingi 8,069,314,000, kati ya hizo shilingi 7,929,326,000 Matumizi ya Kawaida na shilingi 139,988,000 Fedha za Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007 Fungu 94 lilikuwa limepokea na kutumia jumla ya shilingi 5,442,265,438, kati ya hizo shilingi 5,392,265,438 Matumizi ya Kawaida na shilingi 50,000,000 Fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, zilitumika pamoja na mambo mengine, kwa ajili ya kutekeleza majukumu na shughuli zifuatao:-

- Kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanafanya kazi kwa uaminifu na uadilifu na kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

- Kuhakikisha kwamba katika kuajiri watumishi wa umma, ujuzi na anuai za jamii vinazingatiwa na kwamba wanaendelezwa ili kukidhi mabadiliko ya hali ya sasa.

- Kuwa na utumishi wa umma unaojali wateja na kuhakikisha wananchi wanaarifiwa vilivyo kuhusu huduma wanazotarajia kuzipatia Serikalini.

- Matayarisho ya kina ya awamu ya pili ya programu ya maboresho katika utumishi wa umma.

- Uchunguzi wa awali wa malalamiko 156 yaliyowasilishwa na wananchi dhidi ya viongozi wa umma waliotuhumiwa kukiuka maadili ya viongozi, kuhakiki mali au rasilimali za viongozi wa umma 195 wa kada mbalimbali nchini kote.

- Walifanya ukaguzi wa rasilimali watu kwa Wizara 23, Idara zinazojitegemea 6, Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa 12 na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 31.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumla ya Fedha zilizotengwa kwenye Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka 2006/2007 ni kama ifuatavyo:-

Kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, Ofisi ya Rai, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na mafungu yaliyo katika Ofisi hiyo, ilitengewa jumla ya shilingi 199,162,369,300, kati ya hizo shilingi 114,928,982,800 zikiwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 84,233,386,500 Fedha za Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007, Ofisi hiyo ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 162,503,463,727, kati ya hizo shilingi 97,097,743,361 zikiwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 65,405,720,366 Fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa ushauri iliuotoa katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007. Ushauri huo ulihusu Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Katika kipindi kilichopita, Kamati ilitoa ushauri kama ifuatavyo: Serikali iendelee kutatua tatizo la upungufu wa watumishi hasa walimu; Serikali itoe vibali vya muda kwa walimu ambao hawajapata ajira; Serikali iongeze pensheni ya wastaafu; Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi; Serikali iwahamasishe wananchi waitumie *TASAF* kikamilifu ili iweze kuwaletea maendeleo kwa kushirikisha nguvu zao na ifanye uchunguzi wa kina ili kujua sababu za kuchelewa kwa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya *TASAF* na kuimarisha TAKURU na kuipa uwezo zaidi ili kuwakabili watuhumiwa wa rushwa inayofanywa na watu wenye nyadhifa kubwa Serikalini na katika Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wetu ulizingatiwa na kutolewa ufafanuzi kipengele kwa kipengele. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Rais kwa kutekeleza ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa juu ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2007/2008 na kuainisha shughuli mbalimbali za kupokea Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007. Kamati ilielezwa juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na kuainishiwa shughuli mbalimbali zinazokusudiwa kufanywa na Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya

Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma na kiasi cha fedha kinachoombwa ili kuziwezesha Ofisi hizo kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2007/2008, Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba jumla ya shilingi 5,891,233,000 kwa ajili ya Fungu 20 kwa Matumizi ya Kawaida na jumla ya shilingi 190,840,960,000 kwa Fungu 30. Kati ya fedha hizo shilingi 121,250,754,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 69,590,206,000 kwa ajili ya Fedha za Maendeleo.

Aidha, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 32 inaomba jumla ya shilingi 37,482,760,300, shilingi 9,857,913,000 zikiwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 27,624,847,300 zikiwa Fedha za Maendeleo. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 33, inaomba jumla ya shilingi 1,500,009,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Tume ya Utumishi wa Umma inaomba jumla ya shilingi 7,818,121,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na mafungu yake yote, inaomba jumla ya shilingi 243,533,083,300, kati ya hizo shilingi 146,318,030,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 97,215,053,300 kwa ajili ya Fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati yangu kupokea maombi ya fedha kwa Mwaka 2007/2008 na shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi hizo kwa mwaka 2007/2008, Kamati inapenda kutoa maoni na kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Nikianza na Ofisi ya Rais, Ikulu, Kamati inashauri kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iisimamie na kuitumia vizuri sheria mpya ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007 ili kudhibiti mianya yote ya rushwa kuanzia kwenye Halmashauri za Wilaya, Serikali Kuu na kwenye sekta nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria hii ulijadiliwa kwa kina na wajumbe na wadau walioalikwa kwenye Kamati yangu katika kikao cha Kamati kilichofanyika katika Ofisi ya Bunge, Dar es Salaam kabla ya Mkutano wa Saba wa Bunge. Nachukua fursa hii, kuipongeza Serikali kwanza, kwa kuzingatia ushauri tulioutoa mwaka uliopita, kuiboresha Taasisi hii muhimu na kuwasilisha Muswada wa Sheria hii katika Mkutano wa Saba wa Bunge na kupitishwa. Pili, kwa jitihada mbalimbali inazofanya katika kupambana na rushwa.

Lakini pia Kamati inaipongeza Taasisi ya Kuzuia Rushwa kwa kujipanga vizuri hadi Wilayani ambako mafanikio yake yameanza kuonekana kwenye baadhi ya Halmashauri kwa namna zinavyopambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia Ofisi ya Rais, Ikulu, sasa napenda kuzungumzia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nikianzia na mageuzi yanayoendelea katika sekta ya utumishi wa umma, Kamati inashauri kuwa

Serikali ifuatilie utendaji kazi wa watumishi wa umma wasiowajibika na kuwapa mafunzo ya mara kwa mara viongozi wanaowasimamia katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali ili waweze kuwafuatilia na kuwasimamia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya maboresho yanayofanyika katika sekta ya Utumishi wa Umma, Bunge lako Tukufu litakiri kuwa bado zipo ofisi nyingi za Serikali ambazo baadhi ya watumishi wake hufanya kazi kwa mazoea bila kuzingatia maadili na masharti ya kazi zao. Mbali ya Serikali kuhimiza na kuwakumbusha watumishi juu ya utendaji bora wa kazi kupitia nyaraka, semina na vikao mbalimbali, bado kuna baadhi ya watumishi wanaofika kazini muda wanaotaka na kutoka katika vituo vyao vya kazi kushughulikia masuala yao binafsi huku viongozi wao wakiwatazama.

Kamati inaamini kuwa tatizo mojawapo linatokana na viongozi kutowadhibiti ipasavyo watumishi walio chini yao ama kwa kuwaonea haya au kwa kukosa mbinu thabiti za kuwasimamia na hivyo kuendelea kulea uzembe na kuwafanya wakose nidhamu na kutowajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa kuwa sifa ya kiongozi wa umma ni kuwa muadilifu na mkweli, Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe kwamba viongozi wenye dhamana ya kujaza fomu kutoa Tamko la Mali na Madeni yao na kuwasilisha Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, wafanye hivyo mapema kwa mujibu wa sheria na kwa wakati uliowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ililitafakari suala hili na kuona kuwa upo uwezekano kwa baadhi ya viongozi wa umma kutojaza fomu inayohusika kwa wakati unaotakiwa, kitendo ambacho Kamati inaamini kuwa kinaweza kuwafanya baadhi yao kuficha taarifa sahihi za mali walizonazo hasa ikizingatiwa kuwa kutokana na mabadiliko ya maisha na hulka za kibinadamu, inawezekana kuwa wakati kiongozi anapoingia madarakani anaweza kuwa na mali chache lakini wakati anapomaliza utumishi wake anaweza kujilimbilizia mali nyingi zinazoweza kupatikana kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho kwa kuhitimisha, Taarifa hii fupi imeelezea Utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa mwaka wa Fedha 2006/2007 kwa kuelezea kiasi cha fedha kilichopangwa kwa Ofisi hiyo, fedha zilizotolewa na kutumika hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007, majukumu yaliyotekelezwa na utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa kipindi hicho. Aidha, inaelezea Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, maombi ya fedha na ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka huu wa Fedha.

Napenda kukuthibitishia kuwa kutokana na ufafanuzi wa kina uliotolewa na Serikali kwenye Kamati, Kamati yangu ilipitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa kauli moja na kupendekeza yawasilishwe katika Bunge lako Tukufu ili yaidhinishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani za mwisho kwamba nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati. Napenda nimshukuru pia Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), Mheshimiwa Philip S. Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Waziri wa Nchi (Siasa na Uhusiano wa Jamii), Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, Taasisi na Vitengo, kwa ushirikiano waliotupatia na kwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza wakati wote tulipokuwa tukijadili Makadirio ya Ofisi hii.

Kipekee kabisa, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi kubwa waliyofanya walipochambua Bajeti ya Ofisi hii. Matokeo ya kazi yao ndiyo yametuwezesha kuwasilishe Taarifa hii leo. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mwenyekiti wangu Mheshimiwa George Malima Lubeleje, mimi mwenyewe nikiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Choka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohammed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa.

Vilevile nawashukuru Makatibu wa Kamati hii ambao ni Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Emanuel Mpanda, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kutayarisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba hotuba yetu hii inukuliwe yote kwenye *Hansard* na hata sehemu ambazo kuwa sitaweza kuzisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43 (5),(b),(c) na 81(1) Toleo la 2004 kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo kujadili mambo muhimu kwa maslahi ya umma wa Watanzania, na kwa mema yote amabayo amekuwa akitujaalia. Ni matumaini yangu kwamba majadiliano yetu yataweka mbele maslahi ya Umma. Mungu atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Grace Kiwelu ambaye ni Msemaji Mkuu wa Menejimenti wa Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Msemaji Mkuu wa Upinzani, Siasa na Mahusiano ya Jamii kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha uwandaaji wa hotuba hii. Kwani na wao ni wasemaji wakuu katika Wizara zinazojumuisha katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa nafasi ya kipekee kabisa kukishukuru chama changu cha CHADEMA kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi walizonikabidhi katika kipindi cha 2005-2010. Nawaahidi kuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitawatumikia wananchi kwa uadilifu mkubwa.

Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Shoka Khamis Juma , Msemaji Mkuu wa upinzani - Utawala Bora na Mheshimiwa Phares Kabuye , Msemaji mkuu wa upinzani - Siasa na Mahusiano ya Jamii, kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha uandaaji wa hotuba hii, kwani na wao ni wasemaji wakuu katika wizara zinazojumuishwa katika hotuba hii. Vile vile, natoa pongezi za dhati kwa viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani Mhe. Hamad Rashid Mohammed na naibu wake Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kutoa muongozo sahihi kwa mujibu wa kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 tumempoteza mwenzetu, Hayati Juma Jamaldin Akukweti na hivi majuzi tu Hayati Amina Chifupa Mpakanjia. Hivyo kwa majonzi makubwa, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kutoa salamu za pole kwa ndugu, rafiki, jamaa na familia za Marehemu. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** napenda pia kuungana na wenzangu kutoa pole kwa wale wote waliofikwa na misiba na ajali katika kipindi hiki chote tukiwa hapa Bungeni. Mungu awafariji katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Menejiment ya Utumishi wa Umma, kambi ya upinzani inatambua kwa kina umuhimu wa Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama sehemu muhimu sana katika kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za serikali, kuweka mfumo wa uendeshaji wa serikali unaoleta tija na ufanisi, kujenga uwezo wa watumishi wa umma, na kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma. Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa hilo ni muhimu sana idara hii iangaliwe kwa umakini kwa sababu Watumishi wa Umma ni moja ya kiini cha maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inayaona mengi ambayo kimsingi yamekuwa yakidhoofisha swala zima la utendaji na uwajibikaji wa Watumishi wa

Umma. Mambo haya yanatokana na kutokuwepo kwa umakini na ufuatiliaji thabiti ambao umepelekea kuporomoka kwa maadili na uwajibikaji wa Watumishi wa Umma, maisha duni, ubinafsi, na urasimu na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la mishahara kwa watumishi wa umma, maboresho ya maslahi ya Watumishi wa Umma ni jukumu muhimu sana la Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Kwa kutambua hilo, Serikali ya Awamu ya nne haikubaki nyuma na ndio maana ikaahidi 'Maisha bora kwa kila Mtanzania'. Tumaini la kila mtumishi lilikuwa ni nyongeza ya mshahara kulingana na kiwango cha kupanda kwa hali ya maisha kiujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na matarajio ya wengi, hususan wale walipwao kima cha chini, hali imeendelea kuwa ngumu kutokana na kutopanda kwa mishahara kwa kiwango kinachoridhisha. Bajeti kuu ya Serikali mwaka huu inaonesha kwamba mshahara utaongezeka kwa 12%. Hili ni ongezeko dogo sana ukizingatia kwamba kima cha chini cha mshahara ni shilingi 75,000 tu.

Hii inamaanisha kwamba kima cha chini kitaongezeka na kufikia shilingi 84,000 tu. Kwa hali hii bado maisha ya Mtanzania yataendelea kuwa magumu sana huku gharama za maisha zikiendelea kupanda kutokana na Bajeti ngumu iliyowasilishwa na Serikali mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa sherehe za Mei Mosi mwaka huu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikisikia kilio cha Wafanyakazi nchini wakiomba nyongeza ya mshahara ifikie Shilingi 315,000 kwa kima cha chini kutokana na kupanda kwa hali ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kunukuu sehemu ya Risala ya Wafanyakazi iliyowasilishwa na Katibu Mkuu wa *TUCTA* , Ndugu Nestory Ngula katika kilele cha maadhimisho ya Mei Mosi kwenye uwanja wa CCM Kirumba Mjini Mwanza mwaka 2007. Wafanyakazi walisema "…. Vyama vya Wafanyakazi viliwasilisha mapendekezo ya kuboresha kima cha chini cha mshahara kwa watumishi wa Umma cha sh. 75,000/= kwa mwezi kinacholipwa sasa hadi kufikia Sh. 315,000/= kwa mwezi. Kima hicho cha tulichopendekeza cha sh. 315,000/= ndicho kiwango cha chini kabisa cha mshahara kitakachomwezesha mfanyakazi wa ngazi ya chini mwenye familia ya watu sita yaani, mume, mke na watoto wanne chini ya umri wa miaka 18 kuweza kumudu mahitaji muhimu ya maisha kwa mwezi. Mshahara huu wa sh. 315,000/= wa kima cha chini unamwezesha mfanyakazi kutumia sh.142,000/= kwa ajili ya kupata mlo asubuhi, mchana na jioni kila mwezi kama kima hiki cha mshahara hakitakatwa kodi yoyote wala michango mingine. Kima hicho kitakidhi pia gharama zingine za sh.173,000/= kwa mwezi mmoja kulipia usafiri wa kwenda kazini, usafiri wa watoto wanne wa shule ya msingi; sare za watoto, kodi ya nyumba (vyumba vitatu); mavazi, matibabu, maji, umeme na akiba ya dharura…" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza ni kwamba kiasi kilichoongezeka hakifikii hata robo ya maombi yao. Hili linasikitisha sana. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inatambua kwamba kutokana na hali ya uchumi, ongezeko hili kwa ghafla lisingeweza kufikiwa. Pamoja na hayo, bado tunaamini kwamba kama Serikali ingepokea ushauri wa kuboresha bajeti uliotolewa na Kambi ya Upinzani, ongezeko hilo lingeweza kufikiwa angalau nusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti mbadala ya fedha ya mwaka 2007/2008 kama ilivyowasilishwa na Waziri Kivuli wa Fedha inaonyesha kwamba kima cha chini cha mshahara kingefikia kiasi cha shilingi 215,000 kutokana na kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani. Kwa ngazi nyingine mshahara ungepanda kwa asilimia ambayo ingeleta uwiano baina ya kipato cha chini na cha juu. Ni wazi kwamba hili limeshindikana kwa Serikali ya Awamu ya Nne kukataa mapendekezo yaliyotolewa ambayo yangeongeza makusanyo ya mapato ya ndani katika sekta mbalimbali kama vile madini, utalii, uvuvi wa bahari kuu, misitu na bandari, bila kusahau kupunguza misamaha ya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kupendekeza kima cha chini kuwa sh. 215,000, hatukubaliani na ushauri wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini kuwa kima cha chini kisilipiwe kodi. Kambi ya Upinzani inasema, kima cha chini kingeongezwa mpaka kufikia kiasi tulichotaja lakini pia lazima kodi ilipwe. Kulipa kodi ni wajibu wa kila raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitakuwa busara kwa Kambi ya Upinzani kusahau kutetea maslahi ya watumishi wasiokuwa wa umma. Sekta binafsi nayo imekuwa chachu ya maendeleo kwa kutoa ajira kwa Watanzania, lakini ubaya wake unaonekana pale sekta hii inapojilimbikizia faida na kuwanyonya watumishi wake. Kwa sasa kima cha chini katika sekta binafsi ni kati ya sh.35,000 na sh. 48,000, kiasi ambacho ni kidogo sana kulingana na hali ya maisha ilivyo hivi sasa. Kiwango hiki cha mshahara kinamwezesha mfanyakazi kugharamia chakula cha asubuhi, mchana na jioni kwa muda wa wiki moja tu bila kulipia gharama zingine. Kambi ya upinzani inaiomba Serikali itangaze kiwango kipya cha kima cha chini kwa watumishi wasio wa umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia Bajeti kuu ilivyo ni wazi kwamba vipengele vingine si vya msingi kiasi cha kutengewa mabilioni ya fedha kila mwaka, huku watumishi wa Umma wakiachwa solemba. Mfano, katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 zimetengwa shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu. Mwaka 2006/2007 zilitengwa shilingi bilioni 6.125 na mwaka 2005/2006 zilitengwa shilingi bilioni 3.2 kwa ukarabati huo huo wa Ikulu. Kambi ya Upinzani inahoji uhalali wa mabilioni haya yanayotengwa kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu. Kuna nini huko? Je, serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kupunguza baadhi ya matumizi ili kujali maslahi ya watumishi wa umma?

Mheshimiwa Naibu Spika, *TUCTA* pia katika risala yao wanahoji juu ya matumizi ya kifahari na yasiyo ya msingi. Naomba ninukuu "…Hatukatai sababu

zinazotolewa na Serikali kuwa uchumi wetu bado ni mchanga, lakini tunashangaa kuona kwamba pamoja na uchumi kuwa mdogo bado matumizi ya Serikali katika baadhi ya maeneo ni makubwa kuliko hata katika nchi ambazo uchumi wake ni mkubwa kuliko wa nchi yetu. Matumizi haya ya Serikali yasiyofanana na hali ya uchumi ni katika manunuzi ya magari makubwa ya kifahari aina ya *VX (Landcruiser*, *Mitsubishi Pajero, Prado, Nissan Patrol* n.k) ambayo yananunuliwa kwa bei kubwa na yenye gharama kubwa katika matumizi ya mafuta na matengenezo. Inashangaza kuona kwamba kuna magari mengi ya aina hiyo katika ofisi nyingi za Serikali kuanzia Wizarani, Mikoani, Wilayani na Taasisi nyingine za Umma.

Takwimu toka Wizara ya Miundombinu zinaonyesha kwamba hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2005/06 jumla ya magari makubwa na ya kifahari yapatayo 6,000 yalikuwa yamenunuliwa na Serikali kwa gharama kubwa inayokadiriwa kufika *T.Shs*. bilioni 160. Miongoni mwa magari hayo ya gharama kubwa na ya kifahari yaliyonunuliwa na Serikali hadi mwaka 2005/2006 ni aina ya *Toyota Landcruiser (VX/GS, STD, Prado)* yapatayo 1,655, *Nissan Patro*l na *Landcruiser* 885, *Mitsubishi Pajero* 400 na mengineyo. Serikali ingekuwa inafanya matumizi yake kwa kuzingatia hali ya uchumi kama inavyofanya kwa wafanyakazi kwa kuwalipa mishahara isiyotosheleza mahitaji muhimu ya maisha, basi ingeweza kubana matumizi kwa kununua magari madogo ya kawaida na kuweza kuokoa mabilioni ya fedha ili kuboresha mishahara ya wafanyakazi au kuimarisha huduma za jamii. Aidha umezuka mtindo wa kununua samani (*furnitures*) za ofisi za Serikali toka nchi za nje kwa gharama kubwa badala ya kununua kwa watengenezaji wa samani hizo toka hapa nchini ili kubana matumizi, kuongeza ajira, na kuinua uchumi wa nchi yetu."

"Wakati vyama vya Wafanyakazi vilipokutana na Tume ya Rais ya kuboresha Mishahara ya Watumishi wa Umma wakati inakusanya maoni, tulishauri mambo mengi ambayo yangesaidia kupatikana kwa fedha kwa ajili ya kuboresha mishahara ya wafanyakazi. Ushauri tuliotoa ni pamoja na kupunguza magari ya kifahari, kupunguza misafara mikubwa ya viongozi ndani ya nchi wakati wanatembelea mikoani na wilayani. Misafara hiyo hutumia gharama kubwa kugharamia mafuta na matengenezo kwa ajili ya misururu mikubwa ya magari yanayotumika kwenye ziara hizo ikiwa ni pamoja na kuwalipa posho za kujikimu viongozi na watendaji. Matumizi ya aina hii huwafanya wafanyakazi wasielewe kabisa wanapoelezwa kuwa uchumi wetu ni mdogo na hauwezi kubeba gharama kubwa za mishahara wakati wanaona matumizi ya Serikali hayalingani na hali ya uchumi mdogo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kumbukumbu zetu zitakuwa sawa, wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani na kulihutubia Bunge, pamoja na mambo mengine aliunda Tume ya kurekebisha mishahara ya watumishi wa umma ambayo ilikuwa chini ya Mwenyekiti Ndugu Deogratias Ntukamazima, na kwa sasa ni dhahiri kuwa Tume hiyo itakuwa imemaliza kazi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iiweke bayana ripoti hiyo ili wabunge na wawakilishi wa wafanyakazi waweze kuona kama yaliyopendekezwa yanalingana na mapendekezo ya maoni ya vyama vyao vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchelewa kulipwa kwa nyongeza ya mshahara kwa Watumishi wanaopandishwa cheo ni kero nyengine miongoni mwa kero

zinazowasumbua watumishi wa umma. Kambi ya Upinzani inaomba kuelezwa sababu zinazopelekea kucheleweshwa kwa malipo ya nyongeza ya mshahara kwa baadhi ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Utawala Bora ni pamoja na kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa umma. Utawala bora pia ni pamoja na kutoa majibu kwa wakati kulingana na masuala yanayoulizwa na muulizaji. Katika kipindi hiki cha uongozi, Serikali inashindwa kuwapatia majibu wananchi ambao wanaandika barua zao kwa misingi ya kupata ufafanuzi kulingana na masuala mbalimbali. Jambo hili kwa ujumla wake linadhalilisha nchi inayojiita kuwa inafuata sheria na utawala bora. Mfano mzuri ni Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Utawala Bora alipoandika barua kupitia Kiongozi wa Upinzani alipomwandikia Mheshimiwa Rais kuhusu maafa Jimboni kwake, alipata majibu baada ya miezi mitatu. Je, Watanzania wa kawaida inawachukua miaka mingapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia haya ni lazima Ofisi hii itupiwe jicho makini na pembuzi zaidi ili kugundua mianya yenye kudhoofisha utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora unahusu pia utawala wa sheria na kuheshimiwa kwa misingi ya haki za binadamu. Hivi karibuni jumuiya mbili za kiraia, *Legal and Human Rights Centre (LHRC)* na Zanzibar *Legal Service Centre (ZLSC*), kwa pamoja zilishirikiana kutoa Ripoti ya Haki za Binadamu nchini Tanzania kwa mwaka 2006.

Ripoti hiyo imeonyesha kukithiri kwa matukio ya uvunjwaji wa haki za binadamu yanayofanywa na raia na pia vyombo vya dola. Inataja matukio ya kuendelea kutumika kwa adhabu ya kifo, kutozingatiwa kwa haki za wafungwa na mahabusu, matukio ya vikosi vya ulinzi na usalama vya Muungano na vikosi vya SMZ kutumia nguvu za ziada na kuvunja haki za binadamu yakiwemo kuua, kuuawa kwa vikongwe kwa kudhaniwa kuwa wachawi, uhuru wa vyombo vya habari kufinywa, kutoheshimiwa kwa haki na uhuru wa kisiasa wa kujikusanya na kujumuika, kutozingatiwa haki za wafanyakazi, haki za makundi maalumu yakiwemo wanawake na watu wenye ulemavu, wazee, wakimbizi, wagonjwa wa UKIMWI, rushwa na utumiaji mbaya wa madaraka.
Hali inayoelezwa katika Ripoti hii inatisha na haiendani na majigambo ya Serikali kwamba Tanzania inafuata na kuongozwa na misingi ya utawala wa sheria na haki za binadamu. Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo juu ya hatua zinazochukuliwa na Ofisi ya Rais, Utawala Bora katika kufanyia kazi yale yaliyomo katika ripoti hii ili matukio ya aina zilizotajwa yasijirejee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezwaji wa hukumu za Mahakama, tunategemea utawala bora katika nchi unaendelezwa kupitia mihimili mitatu ya dola ambayo ni Bunge, Mahakama, na Tawi la Utendaji kwa kutengana kimamlaka (*Separation of Powers*) kwa mujibu wa Katiba. Kila muhimili kati ya hiyo mitatu unapaswa kuwa huru na kuwa na mamlaka ya kuangalia utendaji wa muhimili mwingine (*Checks and Balances*). Hivyo basi, maamuzi ya kila muhimili yanapaswa kuheshimiwa kikatiba na muhimili mwingine. Kwa mfano, uamuzi unaopitishwa na Bunge juu ya sera

na sheria unapaswa kutekelezwa na Tawi la Utendaji (*Executive*) huku Mahakama ikiwa na jukumu la kutafsiri na kusimamia sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili maamuzi ya Mahakama yatekelezwe ni lazima Bunge lipitishe sheria inayohusu kadhia hiyo. Cha kushangaza ni kwamba tangu Mahakama Kuu ya Tanzania ilipotoa hukumu ya kufuta sheria ya takrima Serikali haijaleta Bungeni Muswada unaohusu hukumu hiyo. Aidha, tangu Mahakama Kuu ilipotoa hukumu juu ya mgombea binafsi Serikali haijaleta Bungeni muswada wa kutekeleza hukumu hiyo? Je, kisheria ni muda gani tangu Mahakama Kuu inapotoa hukumu juu ya jambo fulani na Serikali au chombo kingine cha dola kinatakiwa kutekeleza hukumu hiyo? Kambi ya Upinzani inaitaka mihimili hii mitatu kuheshimiana na kuangaliana kiutendaji kama Katiba inavyotaka ili dhana ya utawala bora ionekane, maamuzi ya kila muhimili yaendanayo na Katiba, lazima yatekelezwe katika muda wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Idara ya Usalama wa Taifa kumekuwepo na ongezeko kubwa la fedha. Kutokana na unyeti wa kitengo hiki tunaweza kuona hata bajeti yake inakuwa kubwa kuliko bajeti ya mihimili miwili ya dola kwa pamoja, yaani bajeti ya Ofisi ya Spika ambayo ni shilingi bilioni 42, na Mahakama ambayo imetengewa shilingi bilioni 37. Kwa ujumla mihimili hii imetengewa shilingi bilioni 79 ikilinganishwa na kitengo cha Usalama wa Taifa ambacho kimetengewa shilingi milioni 110 kama inavyoonyesha kwenye *vote 30,* Programu ya Kumi, Utawala. Pamoja na kuwa kufuatana na Sheria ya Usalama wa Taifa, kitengo hiki shughuli zake nyingi huwa hazizungumzwi wazi wazi, ndio maana hata waheshimiwa Wabunge huwa hatuulizi maswali mengi juu ya kitengo hiki lakini pamoja na utamaduni huo wa usiri, Kambi ya Upinzani inaomba ielezwe sababu za kitengo hiki kuongezewa mabilioni ya fedha kadiri siku zinavyoongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maadili ya Viongozi wa Umma, Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa fomu za maadili kwa madiwani. Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia masuala ya Utawala Bora, asilimia 70 ya madiwani hawakujaza fomu hizo. Kwa kuwa sheria zinamlazimisha kiongozi wa umma kufanya hivyo, Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini nafasi hizo zisitangazwe kuwa ziko wazi kutokana na wahusika kushindwa kutekeleza matakwa muhimu kisheria kama hayo. Pia Waziri alikiri kwamba sio fomu zote zinazokaguliwa, bali mtindo wa *sampling* hutumika akitoa sababu kuwa viongozi ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa mtindo huu wa ukaguzi kwa njia ya *sampling* (yaani kupitia fomu chache tu) unaua dhana nzima ya sheria husika ambayo lengo lake ni kuhakikisha kwamba Watumishi wa Umma wakiwa kwenye madaraka hawatumii madaraka yao kujilimbikizia mali. Suala hili la uzembe wa kuwawajibisha viongozi wanaoshindwa kujaza fomu za maadili inathibitisha jinsi ambavyo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ama imeshindwa kufanya kazi yake kwa makini kwa kuwa ipo juu) au imezidiwa na kazi hivyo kuwa na haja ya kupanuliwa zaidi kufikia ngazi ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni vyombo vya habari vimeandika juu ya madai kwamba Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, alitumia Ikulu ya Watanzania kufanya biashara kwa manufaa binafsi. Je, Serikali inaweza kuweka utaratibu utakaomruhusu raia wa nchi hii kupekua nyaraka za matamko ya Mali na Madeni ya Mheshimiwa Mkapa ili kujiridhisha kuwa biashara yake iliendeshwa sawasawa kwa kufuata sheria za nchi? Kama Rais anaruhusiwa kufanya biashara akiwa Ikulu kwa ajili ya kujitafutia maisha yake ya baadae akitoka katika Ofisi hiyo, Kambi ya Upinzani ingependa kujua nini ulikuwa msingi wa Bunge hili Tukufu kupitisha Sheria Na. 3 ya 1999 *(Political Leaders Retirement Benefit Act,* 1999) pamoja na marekebisho yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ubadhirifu mkubwa wa mali za Umma kutokana na rushwa na ufisadi ambapo kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali anatoa taarifa Bungeni akionyesha fedha nyingi ambazo zimepotea na hazina maelezo ya kutosha kwenye Wizara na idara husika za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2002/2003 Shilingi bilioni 63 ziliripotiwa kupotea, mwaka 2003/2004 shilingi bilioni 82, mwaka 2004/2005 shilingi bilioni 203, na mwaka 2005/2006 shilingi bilioni 273. Kati ya hizo shilingi bilioni 242 ni za Serikali kuu. Ni dhahiri kuwa hakuna hatua zinazochukuliwa kwani kama si hivyo tunaelezaje ongezeko hilo la fedha zinazokosa maelezo kila mwaka? Kambi ya Upinzani inahoji ni hatua gani zimechukuliwa kwa upotevu huu mkubwa wa fedha kwa maana ya kuwawajibisha wahusika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia ikaeleweka kwamba kiasi cha bilioni shilingi 242 ambazo zilifanyiwa ubadhirifu na idara mbalimbali za Serikali Kuu, zingeweza kufanya kimoja kati ya yafuatayo kwa ukamilifu wake:- (i) Kulipa mishahara ya mwaka mzima ya walimu zaidi ya 160,000 wa shule za msingi; ( ii) Kununua vitabu zaidi ya milioni 100 na (iii) Kujenga ofisi za serikali na maktaba ya kila kijiji Tanzania. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Haki Elimu.

Katika kupambana na ubadhirifu mkubwa wa mali za serikali, mara baada ya kuchaguliwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza kwamba *CAG* atapewa mamlaka ya kisheria ya kufuatilia taarifa mbaya za fedha. Vilevile alisema kwamba watumishi watakaohusika na makosa ya matumizi mabovu ya fedha za umma watafikishwa mbele ya vyombo vya dola washitakiwe na si kupitia mabaraza ya kiutawala ambayo huchukua hatua za kinidhamu zaidi. Kambi ya Upinzani si tu inaomba ielezwe kauli hii ya Rais imetekelezwa kiasi gani, bali pia inataka wahusika katika ubadhirifu wa mali za Serikali wawajibishwe kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi bila kujali cheo au madaraka ya mhusika. Kwa ujumla dhana ya Utawala Bora imeendelea kudhoofika kwa kuwepo ubadhirifu mkubwa wa mali za umma, matumizi mabovu ya fedha za umma na upotevu wa fedha za umma usiotolewa maelezo ya kutosha.

Mambo mengi ambayo yanaweza kutajwa katika kadhia hii ni kama vile: masuala yanayohusu mijadala ya mikataba ya *Richmond*, ununuzi wa Rada, ununuzi wa Ndege ya

Rais, mikataba mibovu ya madini, ujenzi wa majengo marefu ya Benki Kuu kwa thamani kubwa mno kuliko hata gharama za kujenga *New York, London* na *Tokyo*, na matumizi mabaya ya nyadhifa za Serikali kwa kujipatia maslahi binafsi. Kama Serikali itafumbia macho uoza kama huu Tanzania kamwe haitaweza kujigamba kuwa na Utawala Bora ambao utaleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingiliano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, ili kuboresha ushirikishwaji wa wananchi katika masuala ya kimaendeleo, Serikali za Mitaa zinapaswa kupewa kiasi kikubwa cha uhuru ambacho kitaziwezesha kusimamia shughuli za kimaendeleo. Shughuli hizi pamoja na kushirikisha wananchi kwa karibu zaidi, pia huhitaji fungu maalumu lenye kutosheleza utendaji wa shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Programu ya kurekebisha mfumo wa serikali za mitaa ulioanza mwaka 1996 (*Local Government Reforms Programme)* Serikali za Mitaa zimepewa uhuru fulani wa kiutendaji (*Devolution*). Lakini pamoja na juhudi hizo zote, Kambi ya Upinzani inaona bado uhuru huo wa serikali za mitaa unadunishwa katika maeneo yafuatayo:-

i) Katika uandaaji wa bajeti, imebainika kwamba vipaumbele vya bajeti vinavyopendekezwa na wananchi kupitia Halmashauri zao huwa havizingatiwi katika ngazi za juu za uandaaji wa bajeti kama vile katika ngazi za Wizara. Matokeo yake ni kupangwa kwa fungu la bajeti lisilowiana na matatizo na mahitaji ya halmashauri husika.

ii) Kupitishwa kwa Muswada unaompa mamlaka Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa kuteua madiwani watatu kwa ridhaa yake kunafanya demokrasia ya wananchi kujichagulia viongozi wao wote katika ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona mwingiliano huo si jambo bora hata kidogo katika suala zima la kuziimarisha Serikali za Mitaa na kuleta maendeleo katika halmashauri zake. Hivyo basi, tunapendekeza yafuatayo:- Kwanza, vipaumbele vya bajeti vinavyopendekezwa na wananchi katika ngazi za Serikali za Mitaa vizingatiwe katika uandaaji wa bajeti kuu kwani vipaumbele hivyo huendana na uhalisia wa matatizo na mahitaji ya wananchi. Kambi ya Upinzani ina kila sababu ya kulizungumzia suala hili kwani tunaelewa kuwa Serikali kuu inatumia takriban robo tatu za fedha yote. Fedha hizo hugharamia mlolongo wa huduma kadhaa ambazo husimamiwa kwenye ngazi ya Serikali Kuu, kama vile mishahara ya wafanyakazi, miradi mikuu ya ujenzi, elimu ya sekondari na afya huku Serikali za mitaa zikipewa kiasi kidogo tu cha fedha kisichotosheleza mahitaji. Pili, wananchi wapewe mamlaka kamili katika kujichagulia wawakilishi wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza katika nyakati hizi za kidemokrasia, bado viongozi wanapewa mamlaka ya kuwachagulia wananchi wawakilishi wao!!!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania *Social Action Fund - TASAF*) ni moja ya chachu za maendeleo ya kijamii. Hata hivyo,

yamekuwepo malalamiko mengi yanayohusu urasimu katika *TASAF* hasa baada ya kuhusishwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kama baadhi ya Wabunge wengi walivyoweza kuchangia katika kipindi cha maswali na majibu imebainika kuwepo kwa ucheleweshaji wa fedha za utekelezwaji wa miradi ya maendeleo. Zaidi ni kwamba kuchelewa kwa michakato inayofanywa wilayani kumetajwa kuwa ndiyo moja ya sababu za ucheleweshwaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka mfuko huu utambuliwe kisheria ili kuwezeshwa kuwa endelevu mpaka pale mkopo wa Benki ya Dunia utakapokwisha mwaka 2009 hasa ikizingatiwa kwamba gharama kubwa zimeshatumika kuwajengea uwezo watalaamu mbalimbali wa *TASAF*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara mpya ya Mipango na Sera imeanzishwa katika Ofisi ya Rais. Kambi ya Upinzani inahoji uhalali wa Kitengo husika hasa ikizingatiwa kwamba kuna Wizara inayohusika na Mipango ambayo ina Idara lukuki. Ni muhimu Serikali ikatueleza kama Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wameshindwa kufanya kazi kiasi cha kuhitaji usaidizi wa idara mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuundwa kwa idara nyingi zenye mwingiliano wa majukumu ni matumizi mabovu ya fedha za umma. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kwamba Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji inatosheleza kushughulikia majukumu hayo.

Dhana mpya ya Utumishi wa Umma inatilia mkazo kuipunguzia Serikali shughuli kwa kuachia shughuli zake kufanywa na taasisi mbalimbali kwa niaba yake. Dhana hii kwa kiasi kikubwa inapunguza matumizi ya Serikali na vilevile kuongeza ufanisi katika sekta husika. Hivyo kitendo cha kuanzishwa kwa Idara ya Mipango katika Ofisi ya Rais ni kuongeza ukiritimba na kinapingana na dhana hiyo ambayo ilikwishaanzishwa na ilitakiwa iendelee kwa manufaa ya Serikali na Watanzania kwa ujumla. Tunaitaka Serikali itueleze sababu za msingi za kuwepo kwa idara hiyo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia ingependa kuelezwa sababu za kuanzishwa kwa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Ongezeko la bajeti ndilo linalotajwa kama sababu ya msingi kwa kuanzishwa kwa kitengo hicho. Kambi ya Upinzani inaelewa kwamba taasisi zote nyeti za Serikali zina wakaguzi wa ndani. Je, uundwaji wa Kitengo hiki unamaanisha kwamba wakaguzi wa ndani hawapo kama ambavyo tunafahamu au wameshindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa?

Kambi ya Upinzani inatiwa shaka na uundwaji wa kitengo hiki kwani bado sababu za msingi hazijawekwa bayana na hivyo hatuoni sababu za kitengo hiki kuendelea kuwepo. Lengo la hoja hii ni kuhakikisha kwamba hakuna mwingiliano wa majukumu au uundwaji wa vitengo ama idara zenye majukumu sawa. Hili likizingatiwa litaokoa matumizi holela ya fedha za walipa kodi na kuzielekeza fedha hizi katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halitokuwa jambo la busara kwa Kambi ya Upinzani kutoshukuru kwa uwepo wa Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii. Ofisi hii ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha uwepo wa siasa bora na mahusiano mema ya jamii katika taifa letu.

Ofisi hii inatarajiwa kuhakikisha kuwa migogoro ya kisiasa na ya kijamii inatafutiwa ufumbuzi wa kudumu ili kudumisha taifa lenye umoja na amani ya kweli. Pamoja na umuhimu wa ofisi hii bado yamekuwepo mapungufu ambayo yamedhoofisha ama utendaji wa ofisi hii au kuhatarisha amani ya taifa letu hususan kule visiwani Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mambo ya Siasa, Kambi ya Upinzani inapongeza kuanzishwa kwa mazungumzo kati ya CCM na CUF ya kuupatia ufumbuzi wa kudumu mgogoro wa kisiasa Zanzibar. Hata hivyo, mazungumzo hayo yamechukua muda mrefu hasa ikizingatiwa ni miezi 18 toka Mheshimiwa Rais alipotoa ahadi ndani ya Bunge hili Tukufu ya kulishughulikia suala hili na hadi sasa hakuna maelezo juu ya hatua iliyofikiwa.

Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo juu ya mazungumzo hayo ambayo yakiendelea kuchelewa yanaweza kuiweka nchi yetu katika mtihani mkubwa wa utulivu wa kisiasa. Tunaamini kabisa kuwa Watanzania wengi ambao walipiga kura kwa ujumla wao walimpatia Mheshimiwa Rais ridhaa ya kuongoza nchi yetu bila ya kuangalia kuwa ni wa itikadi gani. Kwa imani yao hiyo kwa Rais wao, ni matarajio yao pia kuwa Rais huyo atakuwa ni wa wote bila ya kubagua.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kuwa Rais Kikwete ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wakati mmoja, hivyo, kutokana na nyadhifa zake hizo mbili, tunategemea kwa kufuata Katiba ya nchi, atatumia kila kofia yake kwa mahali, wakati na rasilimali mwafaka kufanya shughuli inayoendana na kazi mojawapo ya kofia zake hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua kulisema hili ili lieleweke kwa ukweli na Serikali kwamba katika ziara za mikoa ya Kigoma na Rukwa, Mheshimiwa Kikwete alikwenda huko kama Rais wa nchi, na kwa kutumia pesa za walipa kodi wote wa Tanzania. Kitendo chake cha kugeuza mikutano ya hadhara ya kiserikali kuwa uwanja wa kubomoa vyama vya upinzani kinakwenda kinyume na misingi ya utawala bora.

Hili lilikuwa ni msingi wa malalamiko yaliyotolewa na viongozi wa vyama vya siasa nchini kama ilivyolalamikiwa katika Tamko la Wakuu wa Vyama Vilivyoko Kwenye Ushirikiano yaani CHADEMA, CUF, TLP, na NCCR MAGEUZI, lililotolewa kwa wananchi na kwa vyombo vya habari tarehe 7 Juni, 2007 makao makuu ya CHADEMA Kinondoni, lililobeba kichwa cha habari "Tamko la Kulaani Jitihada za Rais Jakaya Kikwete za Kuuvunja Upinzani Nchini Tanzania." *(Makofi).*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. BATILDA S. BURIAN):** Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Naibu Spika! Nazungumzia Kanuni 50(5)

na hasa (6). Mheshimiwa Mtoa hoja kwa upande wa Kambi ya Upinzani anatumia jina la Mheshimiwa Rais, kutaka kulishawishi Bunge hili, lakini zaidi anahoji mwenendo wa Mheshimiwa Rais, na hasa anaposema kwamba "mtu yeyote anayependa demokrasia", basi kwa kitendo kama kile anahoji mwenendo wa Rais hata katika suala la utawala ubora. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa mtoa hoja afute *paragraph* yake hiyo ya 52, aitoe yote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, Kanuni ya 50(6) inasema mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Kanuni hiyo inatamka kuwa, "Isipokuwa tu kama kunatolewa hoja mahususi kuhusu jambo kama hilo, itakuwa ni marufuku kwa Mbunge yeyote katika mjadala wowote Bungeni, kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Wabunge, Majaji, Mahakimu au watu wengine wanaoshughulika na utoaji wa haki..." Kwa hiyo, nafikiri hiyo unaweza kuiondoa katika kuzungumza kwako. (*Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (k.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI YAUPINZANI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, asante naondoa sehemu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Endelea, dakika zako mbili!

**SHOKA KHAMIS JUMA (k.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YAUPINZANI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** lakini dakika zangu, mbili mbili zitanitosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo katika kupitia vitabu vya bajeti kwa Wizara na Idara za Serikali kwa mwaka huu wa fedha, Serikali imetenga kiasi cha sh. 220,000,000/= kwa ajili ya mambo ya siasa. Je, Serikali inataka kufanya siasa gani nje ya siasa zinazofanywa na vyama vya siasa? Ikumbukwe kuwa ahadi ya kuonana na vyama vya siasa iliyowahi kutolewa na Rais haikuwahi kutekelezwa. Je, fedha hizo zitatumiwa na Rais kukutana na viongozi wakuu wa vyama vya siasa?

Kama siyo hivyo, ni kwa nini hasa itajwe kuwa fedha hizo ni kwa ajili ya siasa? Tunamwomba Mheshimiwa Waziri afafanue matumizi halisi ya fedha hizo ili kama ni mkopo kwa vyama vya siasa vielewe ili viweze kwenda kukopa huko kwa ajili ya shughuli zao za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha Bajeti cha mwaka jana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais , Siasa na Uhusiano wa Jamii, alilieleza Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi yake haikuwa imeanza kazi zake rasmi kwa vile ilikuwa ikijijenga kitaasisi na kazi hiyo ilikuwa ndiyo kwanza imekamilika.
Kambi ya Upinzani inapenda kujua baada ya mwaka mzima kupita toka kauli hiyo kutolewa, Ofisi hii imefanya lipi katika kumsaidia Rais kuimarisha mahusiano ya kisiasa na ya kijamii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahadi za Rais, moja ya sifa kuu ya Serikali ya Awamu ya Nne ni jinsi ambavyo iliweza kuwajaza wananchi matumaini kwa ahadi kedekede

wakati wa kampeni na hata baada ya Serikali hiyo kuingia madarakani. Ahadi hizi zililenga kutoa picha ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Cha kusikitisha ni kwamba kadiri siku zinavyokwenda maisha ya Mtanzania yanazidi kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, baya zaidi ni uamuzi wa Serikali kupitia Bajeti kuu mwaka 2007/2008 kupandisha kodi katika mafuta, bidhaa ambayo inagusa na kuathiri maisha ya kila siku ya Mtanzania kwa namna tofauti tofauti. Kinachojidhihirisha ni kuwa ahadi hizi zilitumika kama danganya toto kwa kuwapatia kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ambalo Kambi ya Upinzani inajiuliza ni kama wananchi wamesahaulika au ahadi hizo zimeshindwa kutekelezeka?

Ahadi hizo ni nyingi sana, kama baadhi yake zinavyoorodheshwa katika makala iliyotolewa na HAKIELIMU kwa jina la "*Government Promises"* ya mwaka 2006 na nyinginezo ambazo zimeendelea kutolewa wakati Rais akiwa madarakani.

Kambi ya upinzani inayo shauku ya kujua zimeshatekelezwa ahadi ngapi katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu wa Serikali ya Awamu ya Nne na ngapi zimebaki, hasa ikizingatiwa kauli ya Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati kwamba ahadi zinatolewa katika kipindi cha miaka 5 na hivyo hizo zote zinatakiwa ziwe zimetekelezwa katika kipindi cha miaka 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa mara nyingine natoa shukurani zangu kwako kwa kunipa fursa hii, na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Nasema asanteni sana na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge mpaka sasa tunao wachangiaji wanne lakini tuzingatie pia kwamba kuna Mawaziri watatu pamoja na mtoa hoja.

Kwa hiyo, ni lengo letu kwamba tunaweza kujadili asubuhi hii na baadaye jioni tuingie kwenye Kamati ya Matumizi. Hivyo, msemaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Job Ndugai, atafutiwa na Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Chacha Wangwe.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi katika Bunge hili la bajeti niwe mchangiaji kwa mara ya kwanza katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaanza, kwa niaba ya wananchi wa Kongwa napenda nitoe salamu za rambirambi kwa wazazi, ndugu na jamaa wa Marehemu Amina Chifupa, sote tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Hawa A. Ghasia kwa kuwasilisha vizuri hotuba hii lakini pia Waheshimiwa Mawaziri, Kingunge Ngombale-Mwiru na Mheshimiwa Philip S. Marmo kwa kazi nzuri

wanayoifanya katika Ofisi hii ya Rais na niseme hapa mapema kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatupo tena kwenye bustani ya Edeni wala dunia hii haifuriki tena maziwa na asali kwa urahisi, uchumi ni elimu ya kuchagua ufanye nini na kipi ufanye baadaye na kwa wakati gani. Nimesikitishwa na msemaji aliyemaliza kuzungumza hivi sasa katika maeneo yake mengi lakini hasa alipofika mwisho kwenye ukurasa wa 24 akizungumzia ahadi za Mheshimiwa Rais kwa kusema kwamba ahadi za Mheshimiwa Rais ni kama danganya toto tu kwa wapiga kura.

Ndugu zangu, dunia hii ilivyo watu huheshimiana, ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais ni ahadi za Serikali ya Awamu ya Nne na ahadi alizozitoa ni kwa miaka mitano, miaka mitano imekwisha lini hadi kuanza kutumia maneno ya kejeli? Mbona siyo sifa, kukejeli kejeli kila mtu? Sisi ambao tupo hapa si tukipigana madongo sisi kwa sisi, huyu mwenzetu mnamtafutia nini wenzetu?

Mimi ushauri wangu ni kwamba inatosha sisi tukijibishana hapa. Wakati fulani nilipata nafasi pale mlipotutuma na Mheshimiwa Mwenyekiti mwenzangu kwenda kwenye Bunge la Uingereza, moja ya mambo ambayo tulijifunza ni jinsi wale watu wanavyoheshimiana, wanakosoana lakini wanaheshimiana. Wanamuheshimu sana Kiongozi wa nchi Malkia wao, na sisi tumheshimu Kiongozi wetu wa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wananchi wengi sana walitegemea kwamba atasema moja kwa moja kuhusiana na mishahara. Katika kieneo cha mishahara amezungumza lakini kwa uchache sana kwamba ni 17% tu imepanda, kwa wananchi wa kawaida walitegemea angechambua kidogo zaidi , labda wakati anamaliza hoja yake anaweza akafafanua kidogo ili kutoa matumaini kwa Watanzania kwa sababu wako wengi watakaopotosha nia njema ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wanasema tulikuwa tumependekeza kwamba ipande hivi na kipandishwe hiki ili fedha ziwe nyingi. Mambo haya si rahisi kama nilivyosema, uchumi ni kupanga, ni elimu ya kujua jinsi ya kupanga, yaani kipi ufanye sasa, kipi ufanye baadaye, kipi ulichonacho mkononi na kadhalika.

Iliwahi kutokea katika Serikali moja huko Ireland, katika kupandisha ovyo ovyo wakapandisha bei za viatu vya watoto wa shule. Serikali ile iliangushwa madarakani kwa jambo dogo tu la bei za viatu.

Watu walianza kupiga kelele kwamba mngepandisha kitu fulani. Kwa hiyo, haya mambo yanapandishwa na kushushwa kwa utaratibu maalumu kwa miaka mitano. Hili ni muhimu sana ningependa Serikali ya Awamu ya Nne mwendelee na *pace* kadri mlivyokadiria na kupanga na siyo mpelekeshwe pelekeshwe, hatuko tena kwenye bustani ya Edeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, iko *concept* ya mtumishi wa Serikali kuajiriwa maisha mpaka atakapostaafu yaani *life time employment.* Hili jambo tulitazame, ndiyo

hii hali inafikia mahali watu wanafanya mambo kama kawaida kwa mazoea yaani *business as usual* kwa sababu ana hakika akishapata ajira yupo tu, akiharibu sana atahamishiwa pale na kadhalika.

Kumfukuza kazi mtumishi wa umma Tanzania bado ni kazi kubwa sana hata awe mzembe kwelikweli, ni lazima ujenge hoja tena na tena. Hili tulitazame, kila baada ya muda tuangalie Utumishi wa Umma. Tutoe fursa tuajiri upya.

Zambia waliwahi kufanya hivyo, walifika mahali wakaanza hata na Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote wakatangaza nafasi zote awamu kwa awamu na wakati kwa wakati. Waliokuwa wazuri waliendelea, wasiotosha wakawapisha wenzao na kadhalika, maana kinachobadilika hapa katika nchi yetu sana sana ni sisi Wabunge, Rais na Mawaziri basi lakini wapo wenzetu ambao wapo na siku zote wapo. Mheshimiwa Waziri unaweza ukaja na mawazo mazuri sana unataka kubadili mambo lakini huwezi wanasema hapana! We namna gani bwana walikuwepo wenzako miaka ya 1970 hawakuweza vilevile; alikuwepo Mama Makinda hapo Ofisi ya Waziri Mkuu naye hakuweza vilevile! Sasa tulitazame hili *life time employment* inachangia sana katika kutucheleweha.

Unakuta Katibu Tarafa ni yule yule toka enzi na enzi hata apewe maelekezo keshazoea; unakuna Mtendaji wa Kata ni yule yule tangu enzi mpaka aje astaafu; wakuu wa Idara mbalimbali unakuta Mhandisi wa Maji huyo alianza enzi hizo amezoea yaani hasukumiki pale alipo, ukimweleza anasema sawasawa Mheshimiwa wewe unafikiri ameelewa kumbe hakuna kitu anakutazama, anakuacha anakwambia alikuwepo fulani bwana na hakuweza itakuwa wewe.

Kwa hiyo, hili tulitazame sana kwani wasomi wameanza kuwa wengi, vyuo vingi tumevifungua na tunaendelea kuvifungua tufike mahali nafasi zetu ziwe za muda katika hili hata Ubunge tufike mahali tuseme ndiyo tukatae *life time employment,* tuseme vipindi vinne mwisho au vipindi sita mwisho lakini pawe na mahali pa kusema hapa mwisho hatuwezi kuwaambia wenzetu wawe na muda halafu sisi tuwe na *infinite*, haiwezekani! (*Makofi*)

**MJUMBE FULANI:** Viwili!

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Viwili! Haitoshi, ni kidogo sana hiyo Waheshimiwa tunaweza tukajadili wakati mwingine.

Niende Kongwa kwa wale ninaowawakilisha. Mheshimiwa Waziri Watumishi wa Idara ya Kilimo na Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kwa muda mrefu hawajapandishwa vyeo wala kuongezewa vyeo wanavyostahili na hili ni kwa Watumishi wa Idara ya Kilimo na Mifugo karibu nchi nzima. Ningeomba watumishi hawa waangaliwe kipekee, sijui kumetokea nini mambo yao yamekuwa hayaendi kama wako 10 wanaopata vyeo ni wawili tu wale wanane hakuna kitu, naomba dosari hiyo iangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo ambalo ningependa kulisema hasa ni watumishi wa Idara za Afya katika Halmashauri za Wilaya kwenye Tarafa zetu, Kata zetu na Vijijini. Watumishi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wanafanya kazi wakiwa na upungufu mkubwa sana wa wataalamu, kwa mfano, unakuta nesi mmoja anahudumia wodi nzima peke yake na wakati mwingine hata wa kumpokea baadaye anaweza asiwepo. Vijijini tuna zahanati ambazo hazina hata Mganga, zina Nesi tu kule Kongwa. Nesi huyo anafanya kazi kutwa nzima yeye peke yake, anakwenda kuandika dawa, kutoa dawa, kuchoma sindano, anahudumia wagonjwa wanaopumzika pale na kadhalika na usiku ni nesi huyu huyu anayetoa huduma ambaye labda anakaa nusu kilomita kutoka nyumbani kwake hadi kwenye Zahanati.

Mama anataka kuja kujifungua labda saa mbili usiku, nesi anakuja kuitwa, anatembea kwa miguu mpaka kwenye zahanati. Mama akimaliza kujifungua kwenye saa saba usiku anaingia mwingine na kukicha asubuhi ni nesi huyuhuyu anaingia zamu. Sasa ni malipo na *package* za aina gani tunaweza kuzitengeneza kwa watumishi ambao wako katika mazingira ya kipekee kama hawa?

Ni vizuri wakaangaliwa hawa Watumishi wa Idara za Afya na Kada zote kwani wana malimbikizo ya muda mrefu sana angalau walimu tuliwalipa kidogo lakini Watumishi wa Afya malimbikizo yao hawajawahi kulipwa kwa muda mrefu sana hasa yale ya nyuma madai sugu ya likizo, kuhudumia magonjwa maalumu kwa mfano wakati wa kipindupindu, bonde la ufa na kadhalika. Lakini juu ya yote mishahara yao ni midogo sana.

Naomba sana mishahara ya watumishi hawa iangaliwe kipekee kwa sababu ya hatari wanayoipata katika aina ya kazi wanayoifanya. Kama tunavyojua magonjwa hivi sasa yamekuwa mengi ukiwemo UKIMWI, Bonde la Ufa na magonjwa mengine ya mlipuko kama Kipindupindu na wagonjwa hawa wote wakipatikana tunawakabidhi Watumishi wa Afya na hasa manesi kushughulika nao katika mishahara hii midogo waliyonayo katika mazingira ya kukosa vitendea kazi.

Ninaomba sana tuwaangalie Watumishi wa Idara ya Afya kipekee na nafikiri ndiyo maana baadhi ya Waheshimiwa Wabunge huwa wanasema mara kwa mara kwamba ni bora basi Watumishi wa Afya wangelirudishwa Wizara ya Afya ili mambo yao yaangaliwe vizuri zaidi na kwa karibu zaidi.

Mwisho, niongelee eneo moja la Watumishi. Watumishi wa Idara ya Wanyamapori , mtu anaweza akajiuliza kwa nini Mheshimiwa huyu anazungumzia Watumishi hawa. Hawa ni Watumishi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, mara kadhaa imeletwa hoja Idara Kuu ya Utumishi kuomba Watumishi hawa wapewe posho ya Mazingira magumu ………!

**MHE. NAIBU SPIKA:** Useme na wewe ulikuwa mmojawapo! (*Kicheko*).

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana! Watumishi hawa wanafanya kazi katika maeneo yenye mbung'o, tembo, simba, nyoka na maeneo mengine magumu sana huko porini, *Game Reserve* kuna maeneo yanaitwa Lukwika Lumisule. Nikiwauliza Wabunge hapa eneo hili liko wapi wachache wanaweza kujua lilipo na hata Moyowosi na Kigosi ni porini, ni ndani kweli kweli. Watumishi hawa wako katika mazingira magumu sana.

Mwaka huu analeta bajeti Waziri wa Maliasili, mapato yao ya *Game Reserves* yatapanda, watazalisha hela kuingiza Serikalini kutoka shilingi bilioni 10 z hadi bilioni 48 kwa huu mwaka mmoja peke yake. Lakini tukisema Watumishi hawa nao waangaliwe kidogo Idara ya Kuu ya Utumishi wanakuwa wanaweka roho ngumu kwa nini? (*Makofi*)

Ni lazima tuwatazame Watumishi wa aina hii wanaishi katika mazingira ya kipekee kabisa, nitashangaa kama wako kwenye mazingira magumu kuwazidi. Mwisho kabisa kule akishambuliwa na wanyama kama Simba au Tembo ama apone au asipone, anapambana na majangili kule porini. Mnasikia uvamizi wa Wasomali huko si jambo rahisi ni mapambano makubwa, naomba Serikali iwaunge mkono hawa Watumishi na iwatie moyo kwa kuangalia *package* yao kipekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru sana kwa fursa niliyopata lakini nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri, natumaini atafafanua kidogo kwa Watumishi wa Tanzania *package* ambayo ameitengeneza ili nao waweze kufurahia matunda ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Naomba nisisahau kusema kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana sasa namwita Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi na Mheshimiwa Shally J. Raymond ajiandae.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN ATHUMAN NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi.

Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anawasilisha hoja yake nilipata nafasi ya kuchangia, kwa hiyo, nilikwisha toa rambirambi zangu kwa wale wote ambao walipoteza maisha na vilevile nilizungumza kuhusu ndugu zangu wa Jimbo la Mlalo. Kwa hiyo, leo nakwenda moja kwa moja katika kuchangia Makadirio haya ya Mheshimiwa Waziri wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, amewasilisha hotuba yake vizuri sana, imeeleweka, na pale ambapo hakutugusa tumeelewa ni kwa nini, lakini kabla sijaingia kwenye yale ambayo nataka kuzungumzia napenda kidogo nijikite kwenye hotuba iliyotolewa na Msemaji Mkuu wa Upinzani kuhusu Mawasilisho ya Wizara hii. Mimi siyo msemaji wa Serikali lakini mimi ni Mbunge wa CCM, kwa hiyo, ni lazima niisemee Serikali ambayo tumeiweka madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Upinzania anazungumzia juu ya Utawala Bora na mambo kadha wa kadha katika kuitupia madongo Serikali. Lakini papo hapo anasahau kuwa wanazungumzia kuhusu mihimili mitatu, kuna Utawala, Mahakama na Bunge, wenyewe wanasahau kuheshimu kwamba mhimili huu mmoja unaitwa Serikali nao unatakiwa kuheshimiwa ili ufanye kazi kama inavyotakiwa. (Makofi)

Ninachoweza kusema katika hili ni kwamba Serikali yetu endeleeni kufanya kazi, bajeti tulikwishapitisha pamoja na kwamba wanakuja na bajeti mbadala. Ilikwishaelezwa kwamba hakuna cha bajeti mbadala, bajeti tuliyopitisha ndiyo hiyo tumeshapitisha, hizo hisia zenu ngojeeni mwaka 2010 mkawauzie wananchi, sasa hivi hazina nafasi hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa niingie katika yale ambayo nilitaka kusema. Lakini kabla ya hapo ndugu zangu wa Upinzani walizungumzia suala la Maisha Bora kwa Kila Mtanzania, wanasahau neno moja muhimu sana kwamba "inawezekana". Sasa Kiswahili siyo kigumu kiasi hicho, mbona mnachukua nusu na nusu mnaiacha? Maisha bora kwa kila Mtanzania inawezekana, malizieni na hili. Kwa hiyo, wote tutekeleze wajibu wetu katika kufikia hali hiyo, ni kazi ya Serikali, ni kazi ya Watanzania wote pamoja na Ndugu zangu wa Upinzani wala msijitoe katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze yale ambayo nilikuwa nimejitayarisha nayo. Ningependa kuzungumzia suala la viwango vya mishahara siyo kwa maana ile ambayo ndugu zangu wamezungumzia. Ni kweli mishahara haitoshi na hakuna mtumishi yeyote katika dunia hii ataridhika kwamba mshahara unatosha lakini inategemea na uwezo wetu kitaifa.

Mimi mtazamo wangu unaangalia upande mwingine, mtazamo wangu ni kuwa ipo haja ya kuangalia mwelekeo na dhana nzima ya jinsi gani tunalipa mishahara katika nchi hii. Hakuna ambaye anakataa kwamba mishahara yetu Tanzania ipo chini ukilinganisha na wenzetu wengi wanaotuzunguka. Zipo sababu, lakini mimi ninapohofia ni pale ambapo tunashindwa kuangalia mbali zaidi ya hizi sababu zilizopo hivi sasa. Kwa mfano, katika bajeti hiihii ukiangalia kifungu 250100 *Basic Salaries* na *Pensionable Services* na ukilinganisha na kifungu 250300 *Employment Allowances* katika mafungu yote Wizara zote, utakuta kwa sehemu kubwa *Employment Allowances* ni kubwa zaidi kuliko mishahara.

**MBUNGE FULANI:** Eti Jamani!

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN ATHUMAN NGWILIZI:** Nilikuwa naangalia sehemu moja ya *Environment* kwa mfano, ndugu zangu wa *Environment* mtanisamehe.

Fungu lile la *environment* katika *program 50 sub vote 5001 Basic Salaries* ni 199,774,000 lakini *Employment Allowances* ni 821 milioni, mishahara ni 199, *Employment Allowances* ni 821 na hiyo ndiyo *trend* kifungu baada ya kifungu ukiacha sehemu ndogo sana. Maana ya hii nini?

Maana yake ni kwamba hawa walioko katika taaluma hiyo hawana haja ya kutegemea mishahara, wanategemea posho na katika nchi tukiwa tunafanya kazi watu wanaacha kutegemea mishahara, tunaanza kutegemea posho basi tusishangae tukikuta ajira zetu zinayumba.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN ATHUMAN NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini? Ni kwa sababu kwanza, wanaopata posho hizo ni akina nani? Wote hapa ni wafanyakazi, wote hapa tumekaa katika ofisi. Wanaopata posho hizi *Employment Allowances* ni wale viongozi wachache ambao wana fursa ya kuzipata ndiyo wanaosafiri kwenda kwenye makongamano, kutembelea eneo fulani na kadhalika lakini Watumishi wengi wako pale pale.

Kwa hiyo, mishahara ile midogo ipo pale, maana yake ni kwamba wale wengi hali zao zinazidi kuwa duni na wachache ndiyo wanaonufaika. Ndiyo mfano kama huu na tunasahau kwamba hawa wengi ndiyo watendaji wengi. Nilidhani hili ni lazima tuliangalie kwa sababu hii ni nchi yetu wote na tunataka kuboresha hali za watumishi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni suala la vyeo, mara nyingi tunazungumza hapa kwamba Watumishi wapandishwe vyeo na Watumishi hawapandishwi vyeo. Mimi nataka kusema kwamba cheo ni dhamana na huyu anayekupandisha cheo ni lazima aridhike kwamba nikimpa dhamana hii huyu mtu je, ataiweza? Haiwezekani mtu kakaa tu, mvivu na mzembe lakini anadai cheo, hapana! Hatuishi na hatupandishani vyeo kwa sababu ya kukaa muda mrefu katika cheo kile ukitaka upandishwe cheo onyesha macheche yako katika kufanya kazi ya Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie suala la pensheni. Hili nalo ni kwa ajili ya huko mbele tunakokwenda, bajeti tumeshapitisha. Sasa hivi yapo malalamiko makubwa sana juu ya viwango vya pensheni katika nchi hii hasa kwa wale ambao ni *pensionable*. Tunao watu ambao wametumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa sana na wanaendelea kuishi kwa bahati nzuri mpaka leo lakini dhambi yao kubwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba wameendelea kuishi kwamba, wewe ulipoacha kazi wakati huo mshahara wako ulikuwa huu, kwa hiyo, hatuna nafasi ya kuangalia zaidi. Tunayo mifano mingi katika kila sekta, kwenye wizara tumekuwa na Makatibu Wakuu na hata Wakuu wa Idara pia wamestaafu hasa wale waliostaafu miaka ya 1980 na mapema miaka ya 1990.

Utakuta pensheni zao ni kidogo mno ukilinganisha na ngazi walizokuwa nazo, inawezekana sisi tuliopo kwenye madaraka sasa hivi tukachekelea kwamba shauri yao lakini tusisahau "linalompata ungo na peku naye litampata," na wewe unaelekea huko huko kwenye kustaafu. Tunasahau kwamba wale ambao tunasema kwa sababu mshahara

ulikuwa huo na kwa sababu muda wao umepita lakini wao ndiyo walitufundisha sisi kazi.

Mimi huwa naangalia watu wengine kama Wakuu wa Vyombo vya dola unamkuta mtu analipwa pensheni ya shilingi 60,000/=, alikuwa ni Mkuu wa chombo cha dola na sisi tumekaa tunasema mambo ni sawa kabisa, siyo sahihi! ni lazima tuwaangalie. Mimi nashukuru kwamba tumeanza vizuri kuwaangalia Marais wetu wanaostaafu, Makamu wa Rais, Mawaziri Wakuu na hata Makatibu Wakuu. Sasa utaratibu huo tuuendeleze mpaka chini, hao wote ambao tumewaacha waliofanyia kazi nchi hii siyo sahihi kuwaacha hivihivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la ikama katika Wizara zetu hizi, kila mara ukiangalia unazungumzia kwenye hospitali hakuna waganga wa kutosha, kwenye Wizara nyingine kama Elimu kuna mapengo, yaani shule hazina walimu wa kutosha, kwa nini tumejifikisha hapo? Ni kwa sababu tumejiwekea taratibu ambazo ni ngumu, nakubali.

Kulikuwa na wakati ilikuwa ni lazima kwa sababu kulikuwa na watumishi hewa wengi mno lakini tulikwisha *deal* na hilo tatizo. Sasa hivi mtumishi anakufa *replacement* haipatikani mpaka tuombe kibali cha kuajiri, mtumishi anafukuzwa kazi *replacement* haipatikani, kwa nini kunakuwa na urasimu mkubwa namna hiyo?

Kama zahanati inatakiwa kuwa na watumishi kadhaa ama Kituo cha Afya ni lazima tuhakikishe tunakwenda kwa ikama, kwanza, kwa vyovyote vile fedha za huyu ambaye amekufa ama amefukuzwa tayari zilitengwa, zimeondolewa na nani? Mbona tunajikwamisha wenyewe? Mimi nategemea katika hili Mheshimiwa Mtoa Hoja naamini atalizungumza wakati akifunga mjadala. Kwa nini hatuwezi kujaza nafasi za watu ambao wamekufa kwa magonjwa, wamefukuzwa kazi na hata kustaafu wakati fedha zao zilikwishatengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Shally J. Raymond na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe ajiandae halafu atafuatia Mheshimiwa Kingunge Ngombare-Mwiru.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ni juzi tu nilichangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nikatoa rambirambi zangu kwa familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa lakini kwa vile kutoka Kilimanjaro Vijana, kina Mama na Wazazi wanaendelea kunipigia simu basi wanaomba ndugu zangu tuendelee kumwombea binti yetu huyu aendelee kupata mahali pema atakapokuwa amepumzishwa huko peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyoeleweka ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Niwapongeze pia Waheshimiwa Mawaziri wengine katika Ofisi hiyo, akiwemo Mheshimiwa Kingunge Ngombare-Mwiru na Mheshimiwa Philip S. Marmo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia maeneo machache tu katika hotuba hii, kwanza, naomba nizungumzie suala la ajira mpya ambayo kwenye kitabu chake ameianisha kwenye ukurasa wa 47 na ninaomba kunukuu.

Kwenye hotuba hii ameeleza kwamba kutakuwa na ajira mpya 41,435 ambazo zitakuwe kwenye elimu, afya, usalama wa raia, kilimo na mifugo na ajira nyinginezo ambazo hakuzitamka lakini najua ni katika maeneo mengine mengi na pia kuna ajira mbadala kama 5,321. Hili ni jambo jema na la kutia moyo. Lakini kinachonitatiza mimi na ambacho napenda nizungumzie hapa hawa watakapoajiriwa watapelekwa vijijini nje ya maeneo ambayo watakuwa wamemaliza masomo au watapelekwa kwenye Wilaya nje ya walikozaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wetu wa sasa hivi imewawia vigumu sana kuishi vijijini na jambo hili ni wazi na linaeleweka. Inaonekana dhahiri kwamba siyo kwa sababu hawataki tu kuishi vijijini ila pia mipangilio ile ya kuishi vijijini ni duni. Kwa nini nasema hivyo?

Utakuta mtu amemaliza Chuo Kikuu, anapangiwa akafanye kazi Shinyanga Vijijini, na ni mara yake ya kwanza, na pale anapofika kwenye kijiji anakuta hakuna matayarisho yoyote ya nyumba ya kuishi. Wote tunaelewa kabisa nyumba ni kitu cha msingi, ni mahali pa mtu kuishi, lakini wakati ajira hizi zikitokea au zilivyoainishwa hapa hakuna matayarisho yoyote kwenye vijiji vyetu kwamba haya ni makazi mapya kwa wale watakaoajiriwa.

Wanapofika huko hakuna nyumba, labda pia hakuna hospitali. Kilichopo tu ni kwamba kama ni mwalimu wa hizo shule mpya zilizojengwa anakaa eneo la mji mdogo na anatakiwa kutembea kilomita siyo chini ya 15 kwenda katika shule ambayo amepangiwa, mwalimu huyo atafika asubuhi amechoka.

Mimi najiuliza hivi atafika kufundisha au atafika kukaa na kuanza kusononeka? Nini basi ninachotaka kuzungumzia hapa? Naiomba Serikali wakati inapopanga ajira hizo mpya ipange pia na fungu la hela la kwenda kuandaa makazi mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema kwamba Idara mbalimbali zipange, naona kwamba siyo kitu muafaka. Ni Wizara hii ndiyo naona inatakiwa kuwajibika na labda itatoa ufafanuzi wakati Waziri akihitimisha hoja hii atueleze wana mpango gani wa hao watu ambao wanapangiwa hizo ajira mpya huko wanakokwenda, wataishi namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba nijikite zaidi kuzungumzia mabinti zetu. Mabinti zetu wanamaliza Chuo wakiwa wadogo sana na baada ya chuo ni kuanza kazi au kwenda kuolewa. Anapofika kijijini kule huko atokako ameacha mchumba wake au

hapana, hajawa na mchumba, tunamweka binti huyo katika maeneo yale, hivi kweli atakaa mahali hapo?

Ninachoona ni gharama kubwa zaidi kwa Serikali kwa sababu binti yule ataripoti apate hiyo fedha ya uhamisho aondoke au hatakwenda kabisa kwa sababu yule ambaye anatarajia kumwoa atamwambia baki tuoane nitakufungulia biashara. Sasa unakuta hata elimu na ile fani aliyoipendelea yeye kufanya imekwama na inakuwa ndiyo mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo kweli ambayo labda kuna nyumba ambazo hawaishi watu na wanapopanga kwenye maeneo hayo huenda mmoja mmoja atapata, lakini je, anapoanza kuwa na familia atakaribisha familia yake kwenye nyumba ya mtu ambayo amepanga? Siyo rahisi!

Jambo lingine pia katika kujenga makazi mapya ya hao waajiriwa, itawasaidia wao katika fani mbalimbali au katika sekta mbalimbali kufahamiana na wenzao endapo watakuwa wamewekwa mahali pamoja; na siyo hivyo tu, hata ulinzi utakuwa rahisi. Lakini nimefikiria sana nikaona huenda mzigo huu ukawa mkubwa sana kwa Serikali yenyewe. Hivyo niiombe Serikali basi ikaribishe wadau mbalimbali kama *NSSF, PPF* na wote wale ambao wanajenga nyumba za kukaa hata *National Housing* kwa sababu inapokuwa ni kuchangia mifuko hiyo, hawaulizi kama wewe unayechangia unafanya kazi kijijini au kwingineko.

Wewe unatakiwa kuchangia *NSSF* utachangia tu. Lakini Taasisi hizo zinapokuja kuwekeza vitega uchumi wote wanapenda kuwekeza katika miji mikubwa ambapo wanapata faida kubwa. Je, kule vijijini nani agharamie? Basi tamko litoke Taasisi hizo zikajenge nyumba pia vijijini ili kuisaidia Serikali katika kufanya mambo hayo yawe rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hilo la makazi kwa hao waajiriwa wapya na jinsi labda wadau mbalimbali wanavyoweza kushiriki, naona sasa nizungumzie kuhusu suala la nafasi ambazo zinatokea Serikalini; watu wamemaliza au wanakuwa wamekwenda masomoni kwa kipindi kirefu na nafasi hizo zinakuwa nafasi za kukaimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la kukaimu ni zuri, lakini sasa kuwepo na ukomo wa kukaimu na siyo isahaulike kabisa. Inakuwa shida pale ambapo anayekaimu hana uhakika wa kupata nafasi hiyo na wale wanaomsikiliza wanajua kwamba huyo anakaimu tu, mwenye nafasi yake yuko njiani anakuja. Kwa kweli hili linashusha ufanisi. Sasa tufanye namna gani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie kwa makini nafasi hizi. Unapokaimu unapewa marupurupu fulani, lakini pia unaweza wakati mwingine ukamudu au usimudu.

Sasa basi kuna nafasi za kukaimu ambazo unatarajia upate wewe kuthibitishwa kwenye hiyo nafasi. Lakini inakupasa ufanye mchakamchaka mkubwa tu, na huenda nafasi hizo zikashawishi rushwa. Ni vyema basi hizo nafasi zikawa na muda ambao unaeleweka kabisa.

Nasema hivyo nikiwa na maana kwamba tujue kabisa kwamba mtu huyo atakaimu kwa muda wa miezi mitatu au sita na anapokidhi apewe, siyo tena mtu huyo huyo anakaimu halafu mnakuja kufanya usaili na yeye anafanya usaili mnamwambia hakuweza kupata hiyo nafasi. Ina maana kwa muda wote huo wa kukaimu yeye alikuwa anafanya kazi gani pale na kwa nini hamkusitisha hiyo ajira mapema kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ikiwezekana itamkwe bayana wakati Waziri anahitimisha hoja yake ili hata wale waliopo katika nafasi za kukaimu wajue. Si hivyo tu, huku kukaimu kwa muda mrefu kunazuia pia ajira nyingine kufunguka chini ya yule ambaye anakaimu. Kwa sababu akithibitishwa yeye ina maana pale alipokuwa yeye pia mwingine anapata ajira mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naona kwamba ni vyema sasa tufikie mahali tuwe na *database.* Wale ambao nafasi zitafunguka tujue tunawachukua wapi na kuwaweka na kuwathibitisha mara moja na siyo kwamba wale ambao wanakaimu inatokea tu hata mtu siyo fani yake, lakini kwa vile ni mtu aliyekaa pale mahali kwa muda mrefu akapatiwa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii nzuri sikuona mahali popote ambapo pamezungumzia sasa jinsi gani tutafikia katika kuchukua nafasi 50 kwa 50 za wanaume na wanawake. Najua Wizara hii ni nyeti na hata uteuzi wa Bodi unatokea kwenye Wizara hii.

Lakini kwa kweli pamoja na kwamba tunasema sana sasa tufikie 50 kwa 50, hatujaanza kuweka bayana kwamba hata Bodi zinapoteuliwa wawekwe wanawake asilimia 50 na wanaume asilimia 50.

Hata Wenyeviti wa Bodi hizo basi tujue kwamba zikishateuliwa kadhaa wawepo wanawake na wanaume na siyo kweli kwamba wanawake hawana uwezo. Wanawake wana uwezo mkubwa tu na wenzetu wanawakubali kwamba wapo tayari kufanya kazi na sisi kwa kushirikiana na kupeana mawazo.

Niiombe basi Wizara hii katika shughuli zake iweze kuona kwamba imefika wakati, kwa sababu iko juu, ionyeshe mfano kwamba inaweza kutekeleza hilo kila uteuzi wa Bodi unapotokea basi wanawake wawe asilimia 50 na wanaume nao asilimia 50 ili twende pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru walionisikiliza. Naomba sasa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa kweli nadhani tumweke Mungu mbele kwa kila jambo kwa sababu ndiye anayetuwezesha kuja hapa na kukalia viti hivi kwa kuwawakilisha wananchi wa Tanzania. Kwa sababu sisi wenyewe tusingekuwa na uwezo wa kuja hapa ila kwa sababu ya wananchi wa Tanzania waliamua kwamba tuje hapa; na naamini kwamba hili Bunge siyo Bunge la Chama chochote, hili Bunge ni la wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Vyama vyote ni vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningependa kusema kwamba tusiwe tunaogopa ukweli hadi kufikia hatua ya kuanza kutishiana humu Bungeni kwa sababu idadi yetu ni ndogo. Sisi ni wawakilishi tu. kuna wananchi milioni 36 na hao wanatarajia kwamba sisi tuwawakilishe; na mambo tunayokuja kuzungumza hapa ni mambo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tuendelee kumkumbuka Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Mwalimu hatasahaulika katika nchi hii kwa sababu aliupenda ukweli na katika ule ukweli yale aliyotuagiza bado yanabaki na tunaendelea kumwona kama yuko hai kwa sababu alikuwa hana makuu na alipenda kwamba hii nchi iende mbele.

Moja ya mambo ambayo marehemu Mwalimu Julius Kambarage aliyazungumza, alipenda kuzungumzia kwamba ubaguzi ni jambo baya na alisema kwamba ule ubaguzi unazaa ubaguzi, kama leo utanibagua kwa sababu ya Chama changu na nyie wenyewe mtarudi mtabaguana kwa sababu ya makundi.

Hiyo ndiyo dhambi ya ubaguzi. Yote ambayo Marehemu Julius Nyerere aliyokuwa anayasema tunayaona hai yanavyoendelea kuibuka katika nchi yetu.

Ndiyo maana napenda wote tukumbuke kwamba wananchi wa Tanzania wanaishi katika shida kubwa na hii Wizara ni Wizara ambayo ina watu ambao wana uzoefu mkubwa.

Kuna kitu kinachoitwa *tools of analysis* yaani uwezo wa kuchambua jamii na kuifahamu jinsi ilivyo na hii jamii ya Tanzania imechambuliwa na wasomi na viongozi na tuchukulie kwa mfano suala la Ujamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuliopo upande huu siyo kwamba hatujui Ujamaa ni nini? Tumepitia vitabu mpaka vya *Maxism, Leninism*, tunafahamu Ujamaa ni kitu gani?

Kwa hiyo, unaposema kwamba hii ni nchi ya kijamaa ujiulize, kwa sababu vipo vitabu vinaonyesha kwamba Ujamaa ni nini?

Mwalimu alizungumzia tabaka, nchi hii imeingia katika masuala ya tabaka na kuna tabaka fulani dogo ambalo sasa ndilo linaloendesha nchi hii kwa jinsi linavyotaka na kwa vitisho na kwa ubaguzi mkubwa.

Marehemu Mwalimu Julius alisema kwamba nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, tabaka gani hilo linaloongoza Serikali kwa vitisho? Kwa sababu tukiangalia Katiba yetu namna gani Serikali ilivyopatikana, nadhani tuna utaratibu.

Tunaomba usitumie maneno ambayo yanatufikisha mahali hakuna *sense* yoyote pale kusema kwamba inatawaliwa na kikundi kidogo chenye tabaka. Mbona viongozi wamechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya Nchi! Tafadhali tumia Katiba!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naelekea kusema kwamba hicho kikundi ambacho ninaenda kukitaja hapa ni kikundi ambacho cha utawala kwa sababu watawala lazima ni wachache.

Siyo Watanzania wote wanaokuja hapa; na nitaendelea kusema vitisho ambavyo ninaviimaanisha kwa sababu ukiangalia hata suala la wale vijana wanaoitwa *wapiga debe*, sasa hivi wanahangaishwa.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Kuhusu Mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haroub Masoud, kuhusu utaratibu!

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 43, Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zinazoongelewa Bungeni, Mheshimiwa Mbunge naona anatuweka nje ya mstari leo.

Kwa sababu Kanuni ya 43(1) inazungumzia "isipokuwa kama Kanuni hizi zimeagiza vinginevyo hakuna mjadala wowote utakaoendeshwa Bungeni ila tu kuhusu iliyoingizwa katika Kitabu cha Shughuli za Bunge na kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge, alikuwa hazungumzii lolote ambalo limo ndani ya *Order Paper* ya leo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aendelee na lile ambalo yeye anatakiwa kulizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, umetolewa utaratibu na mimi nasikiliza utaratibu na ninatoa uamuzi.

Sasa Wizara tunayozungumza hii ni Wizara ya Rais, *Good Governance,* na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, hayuko mbali, lakini kitu alichokuwa anaenda

mbali kusema ni kwamba kuna kikundi kama vile kimeanguka kutoka Mbinguni kimewekwa hapo.

Tunasema hapana, kama ni Serikali hii tuliyonayo sisi imeundwa kwa mujibu wa Katiba.

Ndiyo maana nikamwambia maneno ya vikundi siyapendi, kwa sababu Serikali iliyopo madarakani imeundwa kwa Mujibu wa Katiba. Sasa endelea.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi nilichokuwa nataka kuzungumzia vilevile ni ku-*point out* katika Kanuni ya 50(6) inayosema kwamba "Wabunge au Mbunge asiwe mwepesi kuwazungumzia Wabunge wengine." Mimi ninavyoona ni kwamba sisi Wabunge wa Upinzani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge umesema kifungu cha 50 cha Katiba au Kanuni?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Kanuni. Katika hiyo Kanuni imezungumziwa kwamba Wabunge pia wasiwaseme Wabunge wenzao. Ninamaanisha Kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, usipoteze muda hatutakulipa muda huo!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ngoja nirudi kwenye mada kwa sababu ninachosema kinaeleweka kwamba hapa watu wasifikirie kwamba wao ni bora sana, sisi wote ni Wabunge na tunachokisema hapa ni kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi katika Katiba sehemu ya Tatu inayozungumzia kuhusu Haki sawa kwamba watu wasibaguane. Nasema kwamba vijana kama wale wanaobaguliwa wanaoitwa *Wamachinga* au *wapiga debe* kwa sababu ya jinsi walivyo wakati tunasahau kwamba tumewazaa sisi, tumewakosesha elimu, tumewakosesha ajira na tumewasababishia watoke vijijini waje mijini na sasa mijini hatuwataki kuwaona. Kazi kubwa ya Serikali ni kukimbizana na vijana hao mijini kuwanyima riziki zao wasiwe hata na uwezo wa kuvuta hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kama hilo lazima Waheshimiwa Wabunge tulikemee, kwa nini wao wanabaguliwa kwamba wao ni watu ambao hawafai hata kuwa mijini, hawafai kujiajiri, hawafai kuendesha maisha yao katika nchi hii? Hilo jambo tuliangalie litatuletea matatizo; na sisi tunachofanya hapa ni kutoa *warning* tu kama manabii. Msiposikia sawa. Lakini kama wananchi wa Tanzania ambao wengi wao ni vijana asilimia 80 hatutawatafutia njia ya namna ya kuishi hata huko vijijini na namna ya kuwapatia elimu nzuri na ajira, itatuletea matatizo. Kwa sababu hata wale wanaotafuta elimu nao pia wanabaguliwa. Tumeona suala la wanafunzi hapa jinsi ambavyo wanabaguliwa. Serikali inachukua msimamo wa ukatili ambao hauna huruma kwa

wananchi wa Tanzania. Hiki ni kinyume na Marehemu Mwalimu Julius Nyerere alivyofundisha. Kwamba wapiga debe hawatakiwi, wamachinga hawatakiwi, Changundoa hawatakiwi, watoto wa mitaani hawatakiwi, wanafunzi hawatakiwi, wakulima hawatakiwi na wafanyakazi pia hawatakiwi kwa sababu hata mshahara wanaopata sasa hata haukutajwa hapa. Sasa wafanyakazi wamepewa mzigo mkubwa hata Daktari ambaye amehitimu anakatwa kodi kubwa sana, shilingi 300,000. Lakini pia fedha ile haitoshi, inabidi atafute njia nyingine ya kuishi. Kwa hiyo, Katiba hii inatuchongea kwamba hili suala la ubaguzi litatupeleka pabaya. Tuangalie kwamba watanzania wote wana haki sawa na Serikali ijitahidi kuboresha Sekta ya Kilimo kusudi watu wajiajiri kule vijijini. Serikali iweze kukusanya kodi kubwa zaidi ili hatimaye iongeze mapato yake na vilevile iongeze bidhaa tunazouza nchi za nje ili tuweze kupata fedha za kigeni zaidi kuliko tunazopata sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudi kuzungumzia suala la Utawala Bora. Katika nchi hii wale wanaokaa vijijini ni mashahidi, kuendeshwa udikteta mbaya sana kule vijijini wa kuwakandamiza watu kwa kutumia vyombo ambavyo haviko Kikatiba. Kwa mfano, unapozungumzia kwamba watu wanafuata mila na desturi katika utawala, unakwenda kinyume na makubaliano yetu kwa sababu sisi tumekubaliana kwamba tutafuata Katiba na hiyo Katiba ni pamoja na Sheria. Hii ni Serikali ambayo inatakiwa ifuate Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watu wanapojikusanya pengine kwa sababu ya kukosa ajira na wanateuliwa viongozi ambao wameteuliwa na *ma-DC*, na *ma-RC* , wanajiita kwamba wao ni Mabaraza ya Jadi na hayo Mabaraza ya Jadi yanateua askari wa jadi sungusungu wanazunguka kwenye nyumba za watu wakikamata vitu na kuwapiga watu na kusababisha uvunjaji mkubwa wa Haki za Binadamu. Hili jambo haliwezi kukubalika kwa sababu haliko katika Katiba na haliko katika sheria za nchi. Hayo siyo mambo ambayo tulikubaliana; na katika hiyo hali wanawalazimisha wananchi kufanya chochote. Kwa mfano, hili suala la kujenga shule kwa nguvu pamoja na kwamba shule zinahitajika. Lakini kwa nini watu walazimishwe? Hicho ni kinyume cha Katiba na sheria za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuseme hatuwezi kuogopa vitisho kwa sababu tumekwishajitolea kwamba tutasema ukweli daima na tumeapa hapa Bungeni kwa Katiba hii hii. Kwa hiyo, hata mnapokuwa mnaona sisi ni tatizo hapa, tutaendelea kuwa tatizo mpaka watanzania wote wazibuke masikio na kuelewa kwamba hakuna Utawala Bora katika nchi hii, na Utawala Bora ndiyo unaozungumziwa na hii hotuba. Vilevile hakuna demokrasia ambayo inazungumziwa hapa kwa sababu kungekuwa na demokrasia ingeonekana kuanzia hapa Bungeni. Tunapokuwa tunaanza tu kuzungumza upande wa Upinzani tayari watu wengine wanaona kwamba wao ndio Mawakili wa Serikali, wamekuja hapa Bungeni kuwa Mawakili wa Serikali. Hakuna Mbunge ambaye amekuja kuwa Wakili wa Serikali hapa, sisi tumekuja kuwakilisha wananchi! Wewe zungumza mambo ya wananchi wako waliokuchagua na kama wewe ni Mbunge wa Viti Maalum, uelewe kwamba hili suala itabidi tulirudishe kwa wananchi walitafakari. Inaonekana kwamba wanakuja hapa Viti Maalum kuja kufanya ushabiki wa Vyama hapa ndani ya Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge na wewe zungumza habari za Jimboni kwako, acha Waheshimiwa Wabunge peke yao. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante**.** Mimi nilichokuwa najaribu kupendekeza ni kwamba sasa Waheshimiwa Wabunge wote tupite kwenye tanuru, wawe wanawake, wanaume tupite kwenye tanuru la uchaguzi kusudi anayekuja hapa ajue kwamba amekuja kuwawakilisha wananchi. Lakini watu kama wanataka kuwa asilimia 50 ili kusudi waje kufanya ushabiki wa Vyama hapa Bungeni hilo halitakubalika na wananchi.

Tumekwenda hata Uingereza, tukakuta kwamba tunapata hali ngumu sana kuelezea manaa ya Viti Maalum ni nini. Wako wanawake kwenye Bunge la Uingereza, *House of Commons,* asilimia 20, lakini wote wamepita kwenye tanuru. Sasa kwa sababu hao wanapendelewa, wanapokuja humu sasa wao wanachofikiri ni Chama tu, kwamba wao wapigepige makofi hapa kwa sababu ya Chama.

Halafu wakirudi huko Majimboni wanaenda kutuvuruga sisi watu ambao tulichaguliwa kihalali, hatuwezi kukubali. Hilo lazima tu- *expose* kwamba hawana *mandate* na pia ni kuwadhalilisha kwamba wanawake kama wanawake hawawezi kusimama kama Wabunge wengine wakachaguliwa. Lazima waonekane kwamba wamesimama kama Wabunge, lakini kama wanateuliwa basi ni kuonyesha kwamba wanawake bado ni dhaifu na hiyo pia kijinsia inawanyanyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba hii hotuba haijatueleza ambavyo Serikali inafikiria kuboresha suala la Katiba ya nchi hii pamoja na Utawala Bora. Nina uhakika kwamba masuala ambayo yamezungumzwa hata na wananchi kuhusiana na uvunjwaji wa Utawala Bora katika Vijiji, hii haionyeshi kwamba yale mambo yatafanyika namna gani. Tumezungumzia suala la kulipa kodi, kwamba mwananchi analazimika kulipa kodi na kila mwananchi ambaye amefikisha miaka 18 lazima alipe kodi na hiyo kodi ndiyo inayotumika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la kuwatoza wananchi kwa mara ya pili, kwamba hao wananchi waendelee tena kutoa fedha mifukoni mwao ambazo zimekwishalipwa kodi ili kuchangia maendeleo ya nchi hii, halipo Kikatiba, ni wajibu wa Serikali kukusanya kodi na ni wajibu wa kila mwananchi kulipa kodi. Baada ya kulipa kodi basi huyo mwananchi atulie. Serikali sasa itumie ile kodi kuleta maendeleo, kujenga barabara, kujenga shule, kujenga hospitali. Hayo ndiyo makubaliano ambayo tulikubaliana. Lakini hili sasa la kuweka pembeni majukumu ya Serikali wakati Serikali inakusanya kodi, hizo fedha hazitumiki katika kutengeneza miundombinu au vitu kama hivyo badala yake inawalazimisha wananchi wabebe mzigo ambao ni wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni mambo ya Harambee yameanzia Kenya. Sisi tupo jirani pale, wamechangishwa Harambee, lakini ikafika mahali wakagundua kwamba ni ujanja wa baadhi ya watu ndani ya Serikali kukwepa majukumu ya Serikali. Wameipigia marufuku. Hakuna harambee Kenya siku hizi. Sasa ndiyo tunaikumbatia

sisi hapa. Kule hata akija Mbunge kutokana na ile *CDF* anasema fedha ambazo ametoa Serikalini kuleta kwenye Jimbo, na wanamwaga fedha nyingi, wanajenga miundombinu. Tunawaona pale, hakuna mtu anayeenda kukamatiwa kitu chake wala hakuna hiyo *story* ya harambee tena. Kwa hiyo, hili suala la harambee halipo katika Katiba ndiyo maana nasema hata mimi kama Mbunge, kazi yangu ni kuhamasisha maendeleo na kuwawakilisha wananchi wangu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi siwajibiki kutoa hata shilingi moja kwa ajili ya mchango wa kitu chochote, na wewe kama unatoa sasa tunataka tujue hizo milioni ambazo unaenda kuchangia kule unazitoa wapi? Maana kwenye mshahara wako hazipo. Ina maana mnakusanya fedha kutoka Hazina, mnakwenda kutafuatia kura kule kwa wananchi.

Hiyo ndiyo Wakenya waliikataa. Kwa hiyo, tunataka Serikali itumie fedha zake ambazo inakusanya kutoka kwa wananchi kwa mfano, katika Jimbo langu wanachukua fedha nyingi sana kutoka mpakani, mbuga za wanyama, samaki, migodi, na kadhalika.

Wananchi wa Jimbo langu hawaoni umuhimu wa kuchangia na hata mimi nimewashauri hivyo kwamba hakuna umuhimu wa kuchangia kitu chochote kwa sababu hatujapata haki yetu. Tupate haki yetu kwanza halafu kama ni kuchangia itakuwa ni hiari.

Kwa hiyo, nadhani Serikali katika Utawala Bora ni bora Waziri mhusika apige marufuku mambo ya harambee za nguvu na pia kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki yao kama Katiba inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi sitasubiri nigongewe kengele ila nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii *"message sent and delivered*." Wananchi wamesikia. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Jamani haya sawa? Waheshimiwa Wabunge wapo tofauti na Majimbo yapo tofauti na maendeleo ndiyo maana yapo tofauti. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tunao Mawaziri watatu.

Kwa mujibu wa taratibu zetu mtoa hoja ni mmoja. Kwa hiyo, tumeamua kwamba Mheshimiwa Waziri Kingunge Ngombale-Mwiru ataingia kama mchangiaji lakini wakati huo atakuwa anatoa *input* katika hoja zilizotolewa.

Lakini pia tutampa nafasi Mheshimiwa Waziri Philip Marmo atachukua dakika 15 za mtoa hoja. Hivyo, mtoa hoja atakuwa na dakika 45 na Mheshimiwa Philip Marmo atakuwa na dakika 30. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru unakaribishwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, SIASA NA UHUSIANO WA JAMII (MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU):** Mheshimiwa Naibu Spika,

nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuunga mkono hoja ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, kwa hotuba yake nzuri ambayo imewasilisha vizuri shughuli zilizopita na za mwaka mpya ujao za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kifupi kwa kutoa salamu za rambirambi. Katika kipindi hiki tumepoteza ndugu zetu, Marehemu Waheshimiwa Wabunge wawili. Kwanza, marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti aliyekuwa Mbunge wa Tunduru, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge. Hivi karibuni tumempoteza kijana wetu, marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum.

Halafu ningependa kutoa salamu za rambirambi zangu kwa ndugu wa marehemu waliopata ajali Arusha, Singida na Mbeya. Vilevile nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya viongozi wa Nyanza *Cooperative Union* waliopata ajali Singida, marehemu Ndonyo Hezroni, marehemu Stephen Kazi, Mbunge mstaafu na marehemu William Kasubi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa katika kuchangia kuwashukuru na kuwapongeza wote ambao wamechangia katika mjadala huu. Lakini nitakuwa na mambo kadhaa yafuatayo ya kuyatolea maoni na maelezo.

Kambi ya Upinzani imekuwa na maneno mengi kidogo kuhusiana na masuala ya kisiasa. Ningependa nianze kwa kusema kwamba dhamira ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya kutaka kulishughulikia suala linalohusu migogoro ya kisiasa nchini na hasa kuhusiana na mpasuko wa Kisiasa Zanzibar, dhamira yake inabaki pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada kubwa zimekwishafanyika kulishughulikia suala hilo, halikuwa jambo jepesi sana kwa sababu mpasuko wa kisiasa Zanzibar wote tunaujua kwamba ni hali ambayo imekuwepo kwa muda mrefu. Lakini baada ya jitihada zake sasa uongozi wote kabisa wa Chama cha Mapinduzi umekubaliana kwamba suala hili lazima lipatiwe ufumbuzi. *(Makofi)*

Msemaji wa Kambi ya Upinzani anasema mazungumzo yanakwenda polepole. Kumekuwa na kauli hizi kwa wiki mbili tatu hivi, lakini karibu zote zinatoka upande mmoja, zinatoka ama kwa wafuasi ama kwa viongozi wa Vyama vya Upinzani kama hapa Bungeni. Ningependa niseme tu kwamba hivi wao walikuwa wanategemea mazungumzo yaishe lini? Sasa haya ni mazungumzo ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mpasuko wa kisiasa Zanzibar. Wenzetu walishakuwa na muda ambao waliupanga kabisa kumaliza mazungumzo.

Mimi nadhani katika mazungumzo haya ni lazima watu wakubali ukweli. Ninavyoelewa, mazungumzo yanaendelea vizuri. Chama cha Mapinduzi na Chama cha

*CUF* wameunda Kamati zinazoendesha mazungumzo. Najua yanakwenda vizuri, *inshallah* tutafika huko tunakotaka kufika, subira ni suala la msingi. Wale wanaofikiria wanaweza wakalipua katika matatizo makubwa ya jamii, nadhani wangefikiri mara mbili kama wanataka ufumbuzi wa kudumu ama wanalo lao wanalolitafuta. Kwa sababu kama wanataka ufumbuzi, lazima wawe na subira. Ndio maana kwa upande wa Chama cha Mapinduzi mimi nawapongeza sana wanachama wa Chama cha Mapinduzi na viongozi wao, wamekuwa imara wanasubiri mazungumzo yafikie kule ambako tunataka yafike.

La pili katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani wametoa wito Rais wa Jamhuri atenganishe kofia zake mbili anavyofanya kazi. Sasa nasema, sijui kinachotafutwa ni nini, kwa sababu huyu ni Rais kamili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hata anapokuwa Mwenyekiti kwenye vikao wa Halmashauri Kuu ya Taifa, havui kofia ya Urais na haivuliki. Lakini vile vile yeye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Hata anapokuwa Ikulu hajiuzulu kwanza Uenyekiti, anabaki Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Sasa akiwa kwenye mkutano wa hadhara wanataka avue kofia ipi sasa? Ule utaratibu wa kumvua ile kofia ukoje na hayo yanafanyika katika nchi gani? Kwa sababu Ma-*comrade* wa upande mwingine wakati mwingine mambo mnayoyaleta ya ajabu kidogo, wapi huko ambako viongozi wa vyama ambao vile vile ni Wakuu wa Nchi au viongozi wa nje huwa wanavuavua kofia zao? Hakuna!

Halafu wanasema humu ndani aache siasa! Urais ni siasa tupu! Sasa atawezaje kuacha siasa? Ama katika ile maana ya kejeli ya siasa na nyinyi mnafanya siasa ile ya kejeli! Mimi najua upande wa Chama cha Mapinduzi na tayari upande huu wa CCM sisi tunafanya siasa kweli kweli! Sio ubabaishaji! Ni siasa, yaani kushughulikia mwenendo wa mambo ya kuongoza shughuli za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Rais, nalo hili linarudiwa rudiwa. Kuna ahadi za aina tatu. Kwanza, ahadi kutokana na Ilani ya Uchaguzi. Mgombea wa Urais wa CCM alikwenda kwa wananchi akiwa na Ilani ya Uchaguzi. Alipokuwa huko alikuta hali iliyomtaka vile vile atoe ahadi, akatoa. Aina ya pili ya ahadi, akasema mkinichagua hapa nitashughulikia daraja hili moja la Bariadi. Ziko hizo aina mbili. Lakini iko aina ya tatu ya ahadi ya Rais isipokuwa yeye yuko madarakani, hivi akifanya ziara akiona shughuli akifika mahali kwamba hapa panahitaji Serikali ifanye jambo atatoa tamko la ahadi, nayo ni ahadi halali. Sasa zote hizi zimeratibiwa na zitaratibiwa na kipindi chake cha kutekelezwa ni miaka mitano. Kwa hiyo, hii habari ya kusema tunataka kujua, sasa miezi minane hii, tumechaguliwa miaka mitano, miaka mitano wananchi watatuhoji tumefanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, siasa ina wadau na jamii ina wadau. Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii inashughulika na wadau. Wadau hao sio vyama vya siasa peke yake, siasa inafanywa na makundi mengi sana na jamii vile vile ni makundi mbalimbali kutoka ya dini, walemavu, wanawake, vijana na kadhalika. Kwa kuzingatia muda, nakushukuru sana kupata nafasi na naunga mkono hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mimi kuja hapa kujiunga na

mjadala huu wa bajeti ya Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zilizoko chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba uniruhusu na mimi nitoe salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge mwenzetu Hayati Amina Chifupa Mpakanjia na pia ndugu na jamaa waliopoteza maisha katika ajali zilizotokea hivi karibuni katika Mikoa ya Singida, Arusha, Mbeya na kwingineko. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema Peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba za Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika Mkutano huu wa bajeti kwa mwaka 2007/2008, zimetoa maelezo ya kina na dira kuhusu mwelekeo wa bajeti kwa ujumla na hivyo hotuba za bajeti za Wizara moja moja zinazofuatia ikiwa ni pamoja na hii ya Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma inajazia na kutoa picha halisi ya maelezo mahsusi katika Wizara husika.

Hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2007/2008 iliyosomwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imechangiwa kwa kuzungumza hapa na kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge wengi sana. Hapo baadaye Mheshimiwa Waziri atawataja kwa majina. Mimi naona hapa itoshe tu kwa kusema kwamba maoni yote tumeyachukua, tunayafanyia kazi na kwa ajili ya utekelezaji tutaandaa majibu ya maandishi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumefarijika sana na maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala yaliyowasilishwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati - Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula kwamba Kamati yake imeridhika na utendaji wa kazi na utekelezaji wa miradi yote iliyoko chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu. Maoni kwa wahusika katika Ofisi ya Rais Ikulu ni changamoto ya kufanya kazi vizuri zaidi katika kutekeleza majukumu tuliyojipangia sasa kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Shoka alitoa kauli kadhaa nzito sana na mimi nimeona kwamba lazima tuzitolee maelezo katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo: Eneo la kwanza alilosemea kwa nguvu sana ilikuwa ni eneo la bajeti ya ukarabati wa Ikulu; pili, ameongelea matumizi ya magari ya kifahari; tatu, ameongelea sehemu ya utawala bora ikiwa ni pamoja na haki za binadamu na utekelezaji wa hukumu mbalimbali za Mahakama zetu. Pia Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani amesemea kuhusu malumbano ya sasa yanayoendelea kuhusu shughuli za Rais Mstaafu. Ameongelea pia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, uanzishaji wa Idara ya Mipango na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Ofisi ya Rais Ikulu, matumizi ya Idara ya Usalama na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ya ukarabati wa Ikulu. Kama alivyosema Makamu Mwenyekiti wa Kamati wakati alipowasilisha hoja ya Kamati ni kwamba kazi iliyofanyika kwa kweli ni nzuri sana na Kamati iliridhika. Msemaji wa

Kambi ya Upinzani kwa eneo la utawala bora ni Mjumbe wa Kamati hii. Nashangaa sasa na yeye ameleta maoni tofauti na yale ya Kamati. Kwa wale waliotembelea maeneo yote kwa kweli tatizo ni uhaba wa fedha. Fedha zinahitajika kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu ni nyingi sana. Ninachoongelea suala hili sio ukarabati wa Ikulu Dar es Salaam pekee. Tunahusisha pia Ikulu ya Chamwino na Ikulu Ndogo mbalimbali zilizoko nchini kote.

Alisema angependa kupata mchanganuo wa fedha ambazo zinaombewa kwa kazi ya ukarabati wa mwaka huu. Napenda kumhakikishia kwamba fedha hizi zitatumika katika maeneo nane muhimu ambayo ni ununuzi wa samani kwa nyumba ya makazi ya Rais, ukarabati wa mfumo wa usalama Ikulu, kuboresha mazingira Ikulu, ukarabati wa Zahanati Ikulu, *video teleconference* kwa matumizi ya Mheshimiwa Rais, ukarabati wa nyumba za watumishi Ikulu, ukarabati wa Ikulu Ndogo Dodoma, ukarabati wa Ikulu Ndogo Lushoto, ukarabati wa Ikulu Ndogo Arusha, ukarabati wa Ikulu ya Chamwino, ukarabati wa lango kuu la Ikulu, ukarabati wa Ikulu Mwanza, kubadilisha mitambo ya kupoozea *(chillers)* za maji pale Ikulu na pia ununuzi wa *generator* mpya utakaogharimia Sh. 5,596,900,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani pia amesemea kuhusu magari ya kifahari yanayotumika sasa. Suala hili linafanyiwa kazi pamoja na kwamba kuna utata magari ya kifahari ni yapi, kwa sababu huwezi kusafiri kati ya Dar es Salaam na Kibondo au Mpanda kwa kutumia *saloon.* Kwa hiyo, kwa sasa Serikali haichukulii magari haya yaliyopo ni ya kifahari. Haya ni magari ya kazi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani wa eneo la utawala bora ametaja kuwa wananchi wanapoandika barua Ikulu huwa hawapati majibu kwa haraka. Napenda niseme kwamba nchi hii ina muundo mzuri sana wa utawala na Serikali kwa ujumla. Kuna Serikali kwenye ngazi ya Kitongoji, Mtaa, Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa. Kila ngazi ina majukumu yake, wananchi wengi huwa hawafuati ngazi husika. Suala ambalo lingetatuliwa ngazi ya Tarafa, Kitongoji, Kata linaletwa kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kinachofanyika ni kutafuta ukweli kwenye ngazi husika na hii huchukua muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki za binadamu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amenukuu Taarifa za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na pia kile cha Haki za Binadamu cha Zanzibar Taarifa ya mwaka 2006, kwamba kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu hapa nchini. Taarifa hii iwapo ni sahihi, inawezekana kuna dosari, lakini tujiulize taarifa hii inalinganisha nini? Kama walitumwa na walipewa fedha kuangalia dosari hizi ni dosari za kawaida katika kila nchi. Vitendo vya uhalifu ni vitendo vya kawaida na Serikali yetu inasifiwa kwa kuwa na vyombo vya kutosha vya kusimamia haki na Utawala Bora. Tuna Bunge huru hapa, tuna Mahakama huru, tuna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na kuna taasisi nyingi za kiraia. Lakini taasisi hizi za kiraia pia ziangalie upande wa pili wa kazi nzuri inayofanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinaheshimiwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii inasifiwa na taasisi za nje kwamba inajitahidi sana na ndiyo maana katika ukanda wetu inaonekana ndiyo nchi ya kwanza ambayo

inajitahidi kwa uwezo wake wote kuzingatia haki za binadamu na kuwa na vyombo timamu na huru vinavyolinda haki za binadamu na haki za raia. Kwa hiyo, wakati mwingine pengine ili kutenda haki, taasisi hizi pia zingeangalia yale mambo mazuri yanayofanyika ili kupima dosari iko wapi na tutafute namna ya kutatua matatizo haya kwa utaratibu ambao unaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani pia ameongelea kuhusu utekelezaji wa hukumu za Mahakama na hapa anataja hukumu kama ile iliyofuta takrima na hukumu inayohusu mgombea binafsi. Mimi nadhani utekelezaji unaendelea kwa sababu sasa Sheria ya Takrima imefutwa na Serikali iko mbioni kutunga sheria nyingine na pia suala la mgombea binafsi pia litaangaliwa wakati muafaka utakapowadia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani pia ameliongelea suala la shughuli binafsi za Rais Mstaafu. Kwa kweli Serikali isingependa kujiingiza katika malumbano haya yaliyoko magazetini. Ni malumbano ya magazeti, nashangaa kwamba yameletwa Bungeni na Kiongozi wa Upinzani. Nataka kumweleza kwamba sheria zetu hasa, ile sheria ya maadili iko wazi imeweka utaratibu wa kukagua mali za viongozi kwa masharti kuwa anayekagua mali hizo awe amewasilisha malalamiko kwa Kamishna wa Maadili dhidi ya Kiongozi husika. Pia alipe ada ya Sh.1,000/= kwa ajili ya ukaguzi husika. Tatu, malalamiko dhidi ya kiongozi yawe ya msingi na yanahusiana na Sheria ya Maadili ya Viongozi ya Mwaka 1995.

Utaratibu upo katika tangazo la Serikali Namba 208 la mwaka 1998, haiko wazi na tunasisitiza sheria izingatiwe. Serikali haitajihusisha na malumbano haya kwa vile sheria iliyopo inajitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani pia aliongelea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Taarifa hii imetolewa maelezo ya kina kabisa hasa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Naamini maelezo yale yanatosheleza na yameeleweka.

Pia Mheshimiwa Shoka ameelezea kuhusu uanzishwaji wa Idara ya Mipango, Sera na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Ofisi ya Rais Ikulu. Kwa kweli Idara hizi ni Idara ambazo ziko katika Wizara zote na umuhimu wake ni mkubwa zaidi katika Ofisi ya Rais Ikulu kwa vile Idara ya Sera na Mipango inasimamia majukumu niliyoyataja awali. Idara hii pia ina jukumu la kumshauri Mheshimiwa Rais, lakini pia Idara inatoa ushauri kwa wataalamu kwa Idara nyingine katika utambuzi wa sera, ufuatiliaji na tathmini na mipango ya bajeti ya Ofisi hii. Idara vile vile inafanya kazi kwa karibu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri katika uandaaji wa sera na utekelezaji wake kwa zile sera zinazohusu Ofisi ya Rais Ikulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Ukaguzi ni Kitengo muhimu katika kila Wizara na Sheria ya Fedha na Manunuzi ya Umma na Kanuni zake zinaeleza kuwepo kwa Kitengo hiki cha Ukaguzi wa Ndani kujitegemea ili kumshauri Afisa Mhasibu husika katika kusimamia na kuzingatia kanuni na taratibu za matumizi ya fedha na kuongeza thamani ya kazi bila kusimamia utunzaji wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani pia aliongelea bajeti ya Idara yetu ya Usalama. Sio kweli kwamba kile kifungu alichokitaja ni kifungu cha bajeti ya Idara ya Usalama pekee. Kifungu hicho kinahusika pia na matumizi ya kawaida ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa na inafahamika kama Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Kwa sasa imeongezewa majukumu ambapo mwaka huu itatekeleza sheria mpya. Pia itafungua vituo vidogo tisa kama ilivyoeleza kwenye hotuba yetu, itajenga Ofisi kadhaa za Wilaya na moja ya Mkoa, itafanya mafunzo ya awali ya watumishi wake wapya. Lakini kwa upande wa Idara, pia fedha hizi zitatumika kwenye gharama za uendeshaji wa Ofisi za Wilaya mpya ambazo ni tisa, tutakuwa na ajira mpya kwa ajili ya Wilaya hizo, lakini pia fedha hizi zitatumika kwa ajili ya Ofisi za Mikoa mitatu na Wilaya nne za Kanda Maalum za Dar es Salaam ambazo tumezianzisha hivi karibuni. Kwa hiyo, kwa ufafanuzi ni kwamba kifungu hiki ni mahsusi kwa ajili ya vitendea kazi na uendeshaji shughuli za kila siku za Taasisi ya Kuzuia Rushwa na pia Idara ya Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusu majukumu ya Sekretarieti yetu ya Maadili ya Viongozi. Kwanza, naomba nikubaliane na Makamu Mwenyekiti wakati akiwasilisha taarifa yake kuwa moja ya wajibu wa msingi kwa kiongozi yoyote wa umma, ni kutoa tamko la maandishi kuhusu mali, raslimali na madeni kila mwisho wa mwaka au katika kipindi cha siku 30 baada ya muda wa wadhifa au mwisho wa kutumikia wadhifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutaja katika kipindi kinachoishia Desemba 31, 2006 jumla ya viongozi wa umma 6,415 walikuwa wametumiwa fomu za tamko la mali na madeni. Hadi kufikia 30 Aprili, 2007 jumla ya viongozi waliorejesha fomu hizo baada ya kuzijaza ni 3,317 tu. Idadi kubwa kati ya viongozi wa umma 3,098 ambao hawakuwa wamerejesha fomu za tamko la mali na madeni 2,084 ni Waheshimiwa Madiwani, 415 ni Waheshimiwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na 599 ni viongozi wa kada mbalimbali. Viongozi hao watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Mali ya Viongozi baada ya taratibu zinazohusika kukamilika.

Pia nitoe taarifa kwamba mwishoni mwa Novemba, 2006 Sekretarieti ya Maadili ilianza zoezi la kuhakiki mali za viongozi na kama nilivyotaja sehemu nyingine kwamba ilikuwa ni *sample* kwa sababu hatungeweza kuwafikia viongozi wote kwa ajili ya hali yetu ya bajeti. Zoezi hili la uhakiki lilifanywa kwa njia ya *sampling* kama nilivyosema na linahusu makundi ya viongozi kama ifuatavyo:

Mawaziri 11, Manaibu Mawaziri 13, Wakuu wa Mikoa 20, Makatibu Wakuu 8, Naibu Makatibu Wakuu 5, Wakuu wa Wilaya 20, Majaji 28, Wakurugenzi wa Halmashauri 38, Mwenyekiti wa Halmashauri 1, Wakuu wa Polisi wa Mikoa 10, Makatibu Tawala wa Mikoa 21 na Wakuu wa Taasisi mbalimbali 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi hufanya kazi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kama vile Taasisi ya Kuzuia Rushwa na kila kiongozi akipatikana na mali isiyo halali, basi hatua zinachukuliwa kwa mujibu wa

Sheria. Zoezi hili litaendelea kwa mwaka 2007/2008 na napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba kwa viongozi hawa ambao mali zao zimehakikiwa, kwa kweli zinafanana na hali halisi. Mali walizotaja ndizo zilivyoonekana katika *sight.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wachache waliongelea kuhusu shughuli za MKURABITA na utekelezaji wake, kwa ajili ya muda napenda kusema tu kwamba utekelezaji wa MKURABITA uko katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ni kufanya utafiti wa ukubwa wa sekta isiyo rasmi.

Pili, maandalizi ya maboresho; tatu, utekelezaji; na nne, kukua kwa mitaji. Sasa awamu ya kwanza ya kufanya utafiti umekamilika kwa kufanya tafiti katika Wilaya 34 za Tanzania Bara na Wilaya tisa za Tanzania Visiwani. Hivyo kwa sasa MKURABITA ipo katika awamu ya pili ambayo ni maandalizi ya maboresho na awamu hii inatarajia kukamilika ifikapo mwisho wa mwaka 2008. Baada ya awamu hii, MKURABITA itaanza awamu za tatu na za nne. Maelezo zaidi kuhusu MKURABITA Waheshimiwa Wabunge watapewa kwa maandishi kama nilivyosema hapo awali.

Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pia wameongelea kuhusu *TASAF* awamu ya Pili. Inavyofahamika ni kwamba awamu ya pili ya *TASAF* ilikuwa imeanza rasmi na dukuduku za Wabunge wengi ni kwamba kuna urasimu mkubwa hadi fedha kufika Halmashauri. Wengi wanauliza, kwa nini Serikali hairekebishi kwa haraka urasimu huu? Sasa tunapenda kusema kwamba utaratibu unaofuatwa na *TASAF II* unahusisha hatua zifuatazo: Kwanza, jamii kuibua miradi na kujaza fomu ya makusudio ya kuanzisha mradi.

Pili, fomu hizo huwekwa sahihi na Afisa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa au Sheiya na tatu, fomu hiyo hujadiliwa kwenye Kamati ya Fedha ya Halmashauri au Afisi ya Waziri Kiongozi. Nne, maombi huwasilishwa *TASAF* Makao Makuu kwa mapitio kwa nia ya kuthibitisha kuwa taratibu zimefuatwa. Tano, maombi huwasilishwa kwenye sekta husika ili kuhakikisha kuwa kanuni na viwango vya ubora vimezingatiwa. Sita, fedha huidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Usimamizi na Fedha hutumwa kwa jamii husika kwa utekelezaji. Utaratibu huu ulitokana na makubaliano kati ya Serikali yetu na Benki ya Dunia. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha kuwa fedha zinatumika na miradi inatekelezwa ipasavyo kwamba tunajenga uwezo wa wananchi kusimamia maendeleo yao kwa kuhakikisha ushiriki na umiliki wa jamii katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Pia kuhakikisha kuwa Serikali Kuu inaweka miradi hiyo katika mipango yake. Kwa kufuata utaratibu huu, *TASAF II* imepata mafanikio makubwa katika kipindi kifupi sana. Hata hivyo, Serikali na Benki ya Dunia watafanya mapitio ya utekelezaji wa mradi mwezi Oktoba au Novemba, 2007 kwa lengo la kuongeza ufanisi. Kwa kuzingatia mawaidha ya Waheshimiwa Wabunge Serikali kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imewasiliana na viongozi wa Halmashauri ili waimarishe mazingira ya uandaaji na uwasilishaji wa maombi ya miradi ya *TASAF* Makao Makuu yawe ya haraka zaidi. Kwa ufupi, haya ndiyo maelezo ambayo yaliombwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi na maelezo zaidi yatatolewa kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia sasa niongee kwa kifupi sana kuhusu Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Wabunge wengi waliosema na waliotoa maoni yao kwa maandishi wameipongeza sana TAKURU kwa kazi nzuri inayofanya. Mimi naomba niwashukuru pia kwa kutambua jitihada za TAKURU nitawafikishia wahusika. Lakini tukumbuke kwamba TAKURU inashughulikia vitendo vya jinai, kwa hiyo taarifa ya kazi iliyofanywa na TAKURU kama vile uchunguzi wa Richmond ni matendo ya dhahiri kati ya TAKURU na mengine na Mahakama.

Kwa hiyo, kwa utaratibu wetu isingekuwa bora kuleta taarifa hizi kwa sababu taarifa hizi ni vitendo vya jinai na Bunge haijishughulishi na masuala ya jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ajili ya muda, naomba nimalizie kwa kusema kwa mara nyingine kwamba nawapongeza na kuwashukuru sana kwa ushirikiano wa dhati katika utekelezaji wa majukumu yetu katika Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zote zilizoko chini yake, Mawaziri, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Watumishi wote. Tunaahidi tutajitahidi kwa uwezo wetu wote kutekeleza majukumu yaliyoko mbele yetu kwa mwaka 2007/2008 kwa ushirikiano huu tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mara nyingine tena kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema, tukirudi saa 11.00 Mtoa Hoja atapata muda wa dakika 45 kujibu hoja zilizobaki baada ya Mawaziri wengine kuanza kujibu hoja. Nawaomba mtumie muda huu kuviangalia vile vitabu. Mmeona kwamba kuna mafungu mbalimbali katika Ofisi hii moja. Kwa hiyo msije mkang'ang'ania mshahara wa Waziri Menejimenti ya Utumishi wa Umma, wako wengi. Mkasome vizuri tukija hapa tufanye kazi iliyo njema.

Kwa hiyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.39 mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi tulishapata sehemu ya ufafanuzi kutoka kwa Waziri wa Nchi Utawala Bora, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii na sasa tunamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi.

**WAZIRI WA NCHI MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtwara vijijini na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia na familia za Waheshimiwa Wabunge wote waliondokewa na ndugu, jamaa na familia na marafiki. Vile vile kwa familia za Marehemu waliofariki dunia katika ajali za Singida, Arusha na Mbeya, Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. *Amin*!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo za rambi rambi naomba sasa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote walichangia kwa maandishi na waliochangia kwa kuongea, nikianza na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wote.

Nichukue fursa hii pia kuwashukuru Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru na Mheshimiwa Philip Marmo kwa ushirikiano wao pamoja na majibu yao mazuri ambayo yamefafanua hoja nyingi sana za Waheshimiwa Wabunge. Pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, niwapongeze pia wataalam wote wa Ofisi ya Rais na Taasisi zake walioshirikiana nasi kufanikisha Hotuba yetu ya Bajeti wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi Bwana Philemon Luhanjo na Makatibu Wakuu Bibi Rose Rugembe, Katibu Mkuu Ikulu na Bwana George Yambesi - Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala na Waheshimiwa Wabunge na hata yale ya Kambi ya Upinzani ambayo yamelenga kuboresha utendaji wetu wa kazi yote tutayafanyia kazi ili kuboresha huduma zetu kwa wananchi. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hotuba ya Ofisi ya Rais kwa maandishi na kwa kuongea. Majina haya yanajumuisha pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Hotuba ya Waziri wa Fedha na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Majina ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Job Ndugai - Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Philip Marmo na Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Annia Chaurembo, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Salim Yusuf Mohammed, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa

Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Bahati Abeid, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Matha Umbulla, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Rajabu A. Juma, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa John Lwanji na Mheshimiwa Juma Shoka Juma. *(Makofi)*

Baada ya kuwataja Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja, naomba sasa nianze kujibu hoja zao kama ifuatavyo. Hoja ya kwanza ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani ni ya kuhusu kima cha chini cha mshahara. Kambi ya Upinzani kwanza walipendekeza kima cha chini cha mshahara kiwe Sh. 215,000/= kwa mwezi.

Baada ya kufanya uchambuzi wa kima cha chini cha mshahara kuwa Sh. 215,000/= jumla ya Sh. 2,493,981,000,000/=, hii ikiwa ni sawa na asilimia 12.7 ya pato la Taifa na ikiwa ni asilimia 71.20 ya mapato ya ndani. Lakini pia walikuja na hoja nyingine kwamba *TUCTA* ilipendekeza kima cha chini kiwe Sh. 315,000/= kwa mwezi. Baada ya kima hiki kukifanyia uchambuzi, tumeona zitahitajika Sh. 3,899,758,178,227/= kugharamia mishahara peke yake, hii ni ikiwa ni sawa na ongezeko la Sh. 2,718,942,178,227.52 ya mishahara ambayo tumeitenga mwaka huu. Hii ni sawa na asilimia 19.97 ya pato la Taifa na pia ni asilimia 111.34 ya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia kwa haraka haraka, mapendekezo yote mawili hayawezekani kwa sababu hatuwezi kuchukua mapato yetu yote ya ndani na tukachukua na pesa za wafadhili kulipia mishahara na hata tukisema tuchukue hicho kima cha Sh. 215,000/= maana yake shughuli zote za miundombinu, za elimu, maji tuzisimamishe zote twende tukalipane mishahara. Sidhani kama wananchi watatuelewa. Lakini pia hata hao watumishi wenyewe nadhani watakuwa hawana kazi ya kufanya, kwa sababu watakuwa hawana fedha hata za kutia mafuta kwenye magari yao na kuweza kuwatembelea wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunasema ni lazima kwanza uchumi ukue, ndipo kima cha chini na vima vya mshahara viweze kuongezeka. Hatuwezi kuchukua mapato yote ya ndani kulipa mishahara na hatuwezi kuchukua fedha za wafadhili kulipana na mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo Mheshimiwa Wilbrod Slaa na Mheshimiwa Janeth Massaburi walilieleza, tunaanza na suala la Mheshimiwa Wilbrod

Slaa, alisema kima cha chini kitangazwe kiwe bayana. Ni makubaliano yaliyofanyika kati ya Serikali na Wawakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi.

Wameiomba Serikali kutotangaza mishahara kwa sababu ukitangaza na gharama za maisha nazo zinapanda. Kwa hiyo, wameomba kutotangazwa, lakini pia mshahara ni siri ya mfanyakazi na Serikali. Kwa hiyo, kama mtu anataka kujua kima cha chini cha mshahara labda cha Mheshimiwa Chenge, amwombe mwenyewe, akiridhia atamwambia lakini sio mimi nije nitangaze hapa. Lakini pia katika kima cha chini, Serikali iliombwa tutangaze kima cha chini cha sekta binafsi. Nadhani suala la sekta binafsi atakapokuja Mheshimiwa John Chiligati - Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana atalitolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo liliulizwa ni kuhusu suala la kufikiria kutoa posho ya motisha hasa kwa Walimu wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu. Suala hili limeulizwa na Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Shally Raymond. Suala la motisha kwa Walimu pamoja na kada za watumishi wengine wanaofanya kazi katika mazingira magumu linafanyiwa kazi. Pia suala hili lipo katika mapendekezo ya Tume ya Rais ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma. Kinachofanyika sasa hivi ni kuainisha ni maeneo yapi na kigezo kipi kitumike katika kutoa hiyo posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililoulizwa lilikuwa ni Wafanyakazi wasikatwe mishahara kwa ajili ya michango kama vile michezo. Suala hili nadhani limeshatolewa ufafanuzi na kwamba mwajiri yeyote hapaswi kukatwa mshahara wa mtumishi bila ya ridhaa yake. Isipokuwa makato yanayofanyika kwa mujibu wa Sheria kama vile mapato ya kodi, pensheni na bima ya afya, haya hayahitaji ridhaa kwa sababu yanakatwa kisheria. Kwa hiyo, natoa wito kwa waajiri wote kuacha kukata mishahara ya watumishi bila ridhaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine liliulizwa na Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi kuhusu *employment allowance. Employment allowance* ni posho zinazoambatana na ajira kama ilivyoonyeshwa kwenye bajeti ya Serikali.

Posho hizi ni za malipo ya haki nyingine za wafanyakazi ambazo hulipwa mtumishi anapokwenda likizo, anavyoajiriwa, anavyopewa *subsistance allowance, extra duty* kama mtumishi amefanya kazi zaidi ya muda wa kazi, kwa kweli anahitaji kupata hiyo *employment allowance,* ndiyo hiyo tunayoisema. Lakini pia hata akienda safari ile, *per-diem* ni *employment allowance.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vitu vingi sana ambavyo vinaingiza *employment allowance*. Hata sisi posho zetu zile za Jimbo ni sehemu ya *employment allowance* ya kutuwezesha kufanya shughuli katika Majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa alisema mishahara midogo ya watumishi wa umma ambayo haikidhi mahitaji ndiyo kichocheo cha rushwa. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Florence Kyendesya,

Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Felister Bura.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba vitendo vya rushwa ni tabia. Hata kama tukilipa mishahara ya juu haina maana kwamba rushwa itakwisha. Wapo watumishi ambao wanapata kipato cha chini na hawapokei rushwa na wapo wanaopokea mishahara mikubwa sana na bado wanapokea rushwa. Kwa hiyo, natoa wito kwa watumishi kuacha kupokea rushwa. Mishahara sio kisingizio.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilizungumzwa suala la uhaba wa watumishi. Nadhani nimelitolea ufafanuzi kwamba katika mwaka wa Bajeti ya 2007/2008 tutaajiri watumishi wapya 41,335 na sekta ambazo zimepewa kipaumbele nimezitaja katika hotuba yangu, nadhani hakuna haja ya kulirudia tena.

Suala lingine lilikuwa kuboresha maslahi ya Walimu. Ombi la *teaching allowance* nadhani nimelitolea ufafanuzi, lakini kingine ambacho ninaweza nikaongeza ni kwamba njia sahihi na yenye manufaa kwa watumishi wote wakiwemo walimu, sio posho, ni mishahara kwa sababu mishahara ndiyo inayotumika katika kukokotoa pensheni ya mtumishi anapohitimisha kazi yake. Kwa hiyo, kama utamwongezea mshahara utamsaidia kuondoka na pensheni kubwa kwa sababu hizi posho haziingizwi kwenye makato ya pensheni.

Kuna suala lilizungumzwa na Mheshimiwa Annia Chaurembo kwamba baadhi ya wataalam wa Afya walipandishwa vyeo, lakini hawajarekebishiwa mishahara yao na alisema kwamba hili ni ombi maalum ambalo limepelekwa kwenye Vyama vya Upinzani wakiomba kwamba wale watumishi wa afya waliopandishwa vyeo muda mrefu warekebishiwe mishahara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba sasa hivi suala la kupandisha cheo na kurekebisha mshahara ni suala la mamlaka ya ajira. Kwa hiyo, kama mtumishi yupo katika Halmashauri, Halmashauri ile ndiyo inayompandisha cheo na ndiyo inayomrekebishia mshahara wake. Kama yupo Wizarani ni hivyo hivyo, kama yupo Mkoani ni hivyo hivyo.

Meshimiwa Naibu Spika, tunachofanya Ofisi ya Rais, Utumishi ni kuhakiki kama kweli huyo mtu aliyepandishwa cheo ni kweli anastahili na kama huo mshahara aliowekewa ni sahihi. Kwa sababu wengine unakuta amepandishwa cheo lakini mshahara aliowekewa labda haustahili. Anaweza akawa amewekewa cheo kikubwa, mshahara mdogo. Kwa hiyo, sisi tunachofanya ni uhakiki na hata hivyo hakuna watumishi ambao wamepandishwa vyeo hadi sasa hivi hawajarekebishiwa mshahara. Kama wapo naomba watuletee Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na suala kwamba watumishi wengi hawajapandishwa vyeo. Kama nilivyotangulia kusema katika hotuba ya bajeti yangu ni kwamba, mwaka huu tumepandisha vyeo watumishi 85,000. Kwa hiyo, Walimu wamo, watumishi wa afya, kilimo wote wamo.

Kwa hiyo, wanaostahili kupandishwa vyeo, naomba mamlaka za ajira zote ziwapandishe, kwa sababu wao tumewaweka kwenye bajeti na makisio haya yametoka kwenye taasisi zao. Naomba mara tunapowapelekea taarifa ya kuwarekebishia mishahara yao na vyeo vyao wafanye hivyo kwa haraka.

Suala lingine lilikuwa ni suala la vibali vya ajira kwamba kuna urasimu mkubwa sana katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kutoa vibali vya ajira. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Brg. Gen, Hassan Ngwilizi. Si kana kwamba naitetea Ofisi yangu, sasa hivi vibali mbadala havichukui zaidi ya wiki mbili vinakuwa vimetolewa. Labda kwa ajira mpya ndiyo ambazo inabidi lazima tupate kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi na kwa Mheshimiwa Rais. Lakini kwa ajira mpya ni ndani ya wiki mbili kibali kinatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linalojitokeza, unakuta mtumishi amefariki, ameacha kazi au mtumishi amefukuzwa kazi, waajiri wengi wanachelewa kuwatoa kwenye kompyuta na wanachelewa kutuletea sisi taarifa. Lakini wale ambao wanatuletea taarifa kwa haraka ni ndani ya wiki mbili kibali kinatolewa, kwa hiyo hakuna urasimu wowote na tunafanya hivyo kwa ajili ya kudhibiti ajira hewa.

Mhesimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la Wakuu wa Idara wa Maliasili. Nadhani katika Halmashauri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma tulishakasimu madaraka kwa TAMISEMI na kwa kiasi kikubwa hili suala wamelifanyia kazi, lakini kama kwako kuna tatizo, Mheshimiwa Pinda amekusikia na bado unaweza ukamwona.

Lakini kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma tumewaachia wenzetu wale ambao wanakaimu ambao wana sifa wathibitishe bila kutangaza nafasi hiyo na bila kufanya usaili. Kuna suala la kuweka *Database* ya watumishi wenye sifa ili wapunguze kukaimu kwa muda mrefu.

Napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala la kukaimu muda mrefu halina uhusiano na suala la kutokuwa na *database*. Mara nyingine kama alivyosema, unakuta eneo lingine hakuna mtumishi mwenye sifa na mwanzo tulikuwa tunazitangaza hizi nafasi. Kwa hiyo, kulikuwa na mlolongo mrefu kwa vile baadhi ya watumishi walikuwa wanachagua maeneo ya kufanya kazi.

Lakini sasa hivi tumeagiza waajiri wote kuwathibitisha watumishi wenye uwezo na sifa na kujaza zile nafasi zilizo wazi bila kutangaza na bila kufanya usaili. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa, tatizo hili sasa hivi hatunalo.

Suala la kuboresha kima cha chini cha pensheni za wastaafu, Serikali imekuwa ikiboresha kima cha chini cha pensheni kila wakati kulingana na hali ya uchumi wa nchi. Kama nilivyotangulia kusema, Serikali ingependa watumishi wake wapate mishahara minono, wastaafu wake wapate pensheni zao nono sana. Hata mimi ningependa niondoke na mshahara mkubwa kila mwezi, lakini tatizo ni hali ya uchumi kama nilivyosema. Uchumi ukikua, wote tutajazwa mapesa mifukoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni kuchelewa kwa malipo ya pensheni. Nadhani suala hili limejibiwa sana na wenzangu waliotangulia na hata leo asubuhi limejibiwa na Naibu Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, sina sababu ya kulirudia. Suala lingine ni suala la ununuzi wa samani za ofisi za Serikali kutoka nje kwa gharama kubwa. Suala la manunuzi kwa kweli linafanyika kwa kufuata Sheria na Ofisi yoyote inavyotaka kununua vifaa huwa inatangaza *tender* wanunuzi wanaomba. Kwa hiyo, kinachoangaliwa pale ni gharama ambayo wale wanaotaka kutuuzia samani wanazitaja lakini pia na ubora uliopo. Kwa hiyo, niwaombe wale wananchi wenzetu wazalendo na wenyewe tunavyotangaza kwamba tunahitaji samani, basi na wenyewe waje waombe na wao ili tuweze kununua samani zao, lakini pia waongeze ubora.

Mheshimiwa Job Ndugai aliulizia suala la *lifetime employment* na uzembe wa watumishi wa umma. Utaratibu wa *lifetime employment* au ajira hadi kustaafu hasa kwa viongozi ni utaratibu ambao umeshaanza kufanyiwa kazi kama ulivyofafanuliwa katika sera ya menejimenti na ajira katika utumishi wa umma. Mfano sasa hivi katika wakala ambazo ni za Serikali tunazozianzisha, kule hakuna *lifetime employement*. Kule watumishi wanaajiriwa kwa mkataba wa miaka mitano mitano. Kwa hiyo, baada ya miaka mitano ile nafasi inatangazwa tena, yule mtumishi anaomba na akionekana anafaa atachukuliwa. Kama hafai, basi ataachwa na hivyo hivyo tutauchukua huo uzoefu na mapendekezo yake kufanyia kazi kuona na katika utumishi wa umma ili utaratibu huu utumike.

Kwa hivi sasa utaratibu wa kutathmini utendaji wa kazi wa kila mwaka unasaidia kuzuia uzembe. Kwa sababu kama mtumishi tunamwona ndiyo yupo pale kazini, lakini hatimizi wajibu wake ndiyo maana unakuta tunashindwa kumpandisha cheo na wakati mwingine tunamchukua mtu sehemu nyingine na kuja kuziba ile nafasi yake. Sio kwa vile yupo pale hata kama ufanisi wake sio mzuri, tunamthibitisha kwa nafasi aliyonayo.

Mheshimiwa Shally Raymond, pia aliuliza uteuzi wa wanawake na wanaume katika ngazi za juu kufikia 50 kwa 50. Hakuona kwenye maelezo yangu kwamba kuna mikakati yoyote ambayo imewekwa kwa kufikia hilo lengo. Napenda nimfahamishe kwamba Serikali kwa kweli inafanya maandalizi hayo ya kuhakikisha kwamba wanawake na wenyewe wanachukua nafasi katika maamuzi. Ukiangalia katika taarifa yangu mwaka 2003, wanawake ambao walikuwa katika nyadhifa walikuwa asilimia 28.2, lakini kwa mwaka huu tumefikia asilimia 29.1.

Pia ili kufanya maandalizi ya kuhakikisha wanawake wengi sana wanakuwa katika nafasi za maamuzi na ikiwezekana tunafikia asilimia 50 kwa 50, Ofisi yangu inatoa nafasi za kusoma kwa shahada ya pili kwa wanawake na sasa hivi tangu mwaka 2002 hadi sasa tumeshapeleka jumla ya wanawake 190. Bado kila mwaka tunatangaza na tunapeleka wanawake kwa mafunzo zaidi ili na wenyewe wawe na sifa za kuweza kushika nafasi za maamuzi. Kwa hiyo, mikakati ipo na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Halima Mdee aliuliza, kuna mkakati gani kwa watumishi wa umma wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupewa huduma na dawa? Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Halima Mdee kwamba watumishi wa umma

wanaoishi na virusi vya UKIMWI  na wenye UKIMWI wanapatiwa huduma mbalimbali kama zilivyoorodheshwa katika waraka Na.2 wa Mwaka 2006. Huduma zinazotolewa ni pamoja na dawa za ARV's, mlo kamili wenye virutubisho, ushauri nasaha, usafiri na gharama za malazi kwa watumishi walioshauriwa kupata matibabu katika hospitali nje ya kituo chao cha kazi kwa kupewa majukumu mepesi na pia katika huo waraka tumewaelekeza waajiri kwamba wale watumishi kwa kweli kama nilivyosema, wapunguziwe kazi, wasipewe majukumu  mazito. Pia sasa hivi tunaandaa mwongozo wa kudhibiti maambuki ya UKIMWI katika utumishi wa umma. Mchakato utakapokamilika, mwongozo huo tutawapelekea waajiri na kwa sasa upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Shally Raymond - Mbunge wa Nanyumbu Mheshimiwa Mkapa, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Nyawazwa na Mheshimiwa Mwinchoum na wenyewe walielezea suala ka walimu kuripoti vituo walivyopangiwa na baada ya muda kuondoka na wakaomba tuboreshe mazingira kwa kujenga nyumba. Nadhani hili linafanyiwa kazi na atakavyokuja Waziri wa Elimu ataelezea ni mikakati gani wanayoifanya kuboresha mazingira ikiwemo pamoja na kujenga nyumba za walimu.

Kuhusu Watumishi wabadhirifu kuhamishwa badala ya kuchukuliwa hatua za nidhamu mfano madaktari ,nadhani hili alilitolea ufafanuzi sana jana Mheshimiwa Mizengo Pinda, lakini bado tutalitoa katika majibu yetu kwa maandishi.

Kuna suala ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Charles Keenja kuhusu Serikali kwamba inafanya nini kuhakikisha kuwa watumishi wake wanapata nyumba?  Je, Serikali ina utaratibu wa kuangalia endapo idadi ya watumishi waliopo ndiyo ile ile inayoidhinisha?

Kwanza, suala la nyumba ni kama nilivyolijibu kwamba Serikali inalifanyia kazi. Lakini pia kipo Kitengo cha Mikopo ya Nyumba kwa watumishi Serikalini ambacho kipo Wizara ya Ardhi.  Suala la watumishi tunafanya ukaguzi wa watumishi na sasa hivi tumeshafanya katika mwaka huu wa fedha unaoishia.  Tumefanya *audit* ya watumishi katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani na tunataka tuendelee kwa Tanzania nzima. Tumeanza na walimu wa Sekondari na watumishi wa maliasili. Lakini lengo letu tufanye kwa watumishi wote Tanzania.

Mheshimiwa Stephen Galinoma aliuliza maboresho ya Serikali za Mitaa kwamba hayana tija, ni mzigo kwa Serikali hasa Mkoani. Nadhani Mheshimiwa Pinda alielezea sana kwa urefu manufaa ya maboresho ya Serikali za Mitaa, lakini hata maboresho ya utumishi wa umma nadhani wote manufaa yake tunayaona, hakuna haja ya kuelezea sana wakati kwenye Kamati nilimpa kwa urefu sana manufaa ya maboresho. Kuna hoja iliulizwa kuhusu wahitimu wa Kidato cha Sita ambao wanapata mafunzo ya muda mfupi wanapomaliza mafunzo haya tunaowaajiri hawa Walimu wa *crash programme*. Je, wanaopewa vibali vya muda wanalipwa mishahara au wanalipwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba wale walimu wa *crash programme* tunawalipa asilimia 80 ya mshahara na wataendelea kupata asilimia 80 mpaka watakapofuzu elimu  yao  kama  ni  shahada  au  kama  ni  stashahada

kwa sababu bado tunaendelea kuwaendeleza sio kwamba tulivyowapeleka mashuleni tumewatupa; na Mheshimiwa Waziri wa Elimu atalielezea vizuri, lakini kwa maana ya mshahara tunawalipa asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Keenja pia alizungumzia tatizo la Muundo wa Sekretarieti ya Mkoa na Mawasiliano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Nadhani hili pia limeelezwa sana na Mheshimiwa Pinda, nisingependa nilirudie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Salim Mohamed ameuliza: Je, kumekuwepo na ongezeko lolote la malalamiko dhidi ya watumishi wa umma? Baada ya kubaini kuwepo kwa mapungufu katika mfumo wa kushughulikia malalamiko, Serikali imeandaa mfumo wa kushughulikia malalamiko ambao sasa hivi unafanyiwa majaribio katika taasisi saba kama nilivyosema katika hotuba yangu na baadaye utaratibu katika Wizara na Idara zote.

Mfumo huu utatuwezesha kupata takwimu kamili zitakazoonyesha ongezeko au kupungua kwa malalamiko dhidi ya watumishi wa umma. Aidha, kutokana na Serikali kuongeza uwazi katika utendaji na kuelimisha wananchi kuhusu wajibu, viwango vya utendaji na haki za wananchi kwa njia mbalimbali ikiwemo mikataba ya huduma kwa mteja, kuna mwelekeo wa ongezeko la malalamiko. Hii inatokana na kuongezeka kwa mwamko wa wananchi kudai haki zao na kujengeka kwa imani kuwa malalamiko yao yanashughulikiwa. Lakini, takwimu halisi kwa sasa hivi hatuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Galinoma pia alisema kwamba maboresho ya utumishi wa umma bado hayajafanya kazi Mikoani. Nadhani hili nimeshalijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, kama nilivyosema, sio rahisi nizijibu hoja zote, nadhani nyingine tutazitoa kwa maandishi kabla ya kufika mwezi wa Nane tutakuwa tumeshawapatia Waheshimiwa Wabunge. Baada ya hapo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 20**

Kifungu 1001 – *Administration and General*…..........................Shs. 5,891,233,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 30**

Kifungu 1001 - *Administration and General*...................................Shs. 117,637,301,500/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Programu ya 10, *Subvote* 1001, *Basic Salary* ambayo nataka kuuliza, Mheshimiwa Ngombale-Mwiru ambaye anahusika na mambo ya Siasa na kabla sijaendelea nataka ku-*declare* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha *UDP*. Kwa hiyo, nina haki ya kuuliza. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Ngombale-Mwiru, Siasa…

**NAIBU SPIKA:** Mawaziri wanatajwa kwa vyeo vyao!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siasa au Vyama vya Siasa ndiyo nguzo au inaweza kuwa chanzo cha kuwa na amani katika Taifa au machafuko katika nchi. Nimeangalia hesabu zote hizi sioni ni wapi Mheshimiwa anayeshughulikia mambo ya Siasa ametengewa fungu ambalo linaweza likasaidia kuimarisha mazungumzo *(Dialogue)* kati ya vyama vya siasa kuhakikisha kwamba vyama hivi vina uwezo wa kujenga dhana ya uvumilivu, dhana ya kuweka utaifa mbele na kufanya mambo ya kisiasa katika hali ya amani.

Kwa hiyo, naomba ufafanuzi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – SIASA NA UHUSIANO WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cheyo, akitazama ukurasa 46, Kifungu 280700 atakuta analoliulizia.

**NAIBU SPIKA:** 280700, *Transfers and Subsidy – Nonprofit Organizations*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – SIASA NA UHUSIANO WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo atakuta pesa zimetengwa Sh. 221,000,000/=. Lakini, nataka niongezee tu kwamba, unajua mtangamano wa hali katika nchi hautegemei fedha, unategemea sana uongozi wa makundi mbali mbali katika jamii pamoja na uongozi wa Vyama vya Siasa. Sasa, kwa upande wetu wa Serikali, tunajua changamoto iliyopo mbele yetu na yeye anajua kwamba kila wakati ambapo kunakuwa na matatizo tunakutana, tunashauriana na Vyama vya Siasa ili tuweze kuhakikisha kwamba nchi yetu ina utulivu, ina ushirikiano na kadhalika. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika programu hiyo hiyo, *subvote* 1001 - *Basic Salary,* napenda kuuliza swali la la kisera hapa kwa Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na masuala yanayohusu *PCB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia kwa maandishi, nilitaka kumwomba Mheshimiwa Waziri atuwezeshe katika Bunge hili kupata taarifa ya *PCB* ambayo waliitoa kwenye magazeti kuhusu uchunguzi wa Kampuni ya Richmond. *PCB* walifunga ule mjadala kwa kusema kwamba wamemaliza. Lakini, wakati wanafunga wakaeleza kwamba kuna mapungufu machache yameonekana katika taratibu zilizotumika. Sasa, kwa mtu anayesimamia shughuli za Serikali kama Mbunge, anapenda kujua haya mapungufu ni yapi.

Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu anasema, hili ni suala la kijinai jinai, kwa hiyo, taarifa ile haiwezi kuwasilishwa Bungeni. Lakini, mimi sina tatizo na hiyo sehemu ya kijinai, nadhani hata wakati tunatunga sheria ya *PCB* hilo pia tulilisema. Lakini, inapofika mahali kwamba kuna mapungufu ambayo wanasema kwenye lile tangazo walilotoa kwenye gazeti kwamba siyo tu upungufu, kuna uzembe pia ulitokea. Sasa, nadhani taarifa zile zinaacha kuwa za kijinai, kuna *element* ya kiutendaji ambayo inakwenda kwenye uzembe. Nataka Waziri atueleze taarifa ile inatolewa wapi na kwa utaratibu gani ili Bunge liweze kujadili taarifa hizo kwa sababu sehemu ya jinai tutaiachia iende kwa taratibu za jinai, lakini sehemu ya uzembe na sehemu hii nyingine ni suala ambalo Bunge linapaswa kuisimamia. Sasa, nataka ufafanuzi kwamba taarifa ile tunaipataje.

Lakini ya pili, je, kama taarifa hizo ni za siri, ni kweli kwamba *PCB* inaweza ikachapisha kwenye magazeti, ikaacha kuwaamini Wabunge, ikaamini zaidi vyombo vya habari! Kwa sababu naona hapa sasa kuna tatizo kwamba *PCB* inaweza ikakwepa kutoa taarifa yake kwa vyombo vinavyosimamia Serikali, lakini ikaitoa taarifa ile kwa magazeti na Bunge halitakuwa tena na namna ya kuhoji. Nilitaka ufafanuzi katika haya mawili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mbunge anaulizia taarifa ya uchunguzi uliofanywa na TAKURU kuhusiana na shughuli ya Kampuni ya Richimond. Kama alivyosema yeye mwenyewe ni kwamba *PCB* muda wote inashughulikia masuala ya rushwa na rushwa ni vitendo vya jinai na mkondo wa matendo ya jinai hatimaye hufika katika hatua ya aidha mashtaka au uchunguzi kufungwa na kuelekea Mahakamani na hata siku moja sio Bungeni. Narudia tena, taarifa za *PCB* kwa asilimia mia moja zinahusiana na masuala au matendo ya jinai na mkondo wa matendo ya jinai. Kwa maana hiyo basi, hata siku moja haiwezi kuwa Bungeni isipokuwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Mbunge au raia yeyote ana ushahidi ambao anafikiri utaisaidia TAKURU au TAKURU haikufuatilia kwa makini, basi raia hazuiwi hata kufungua mashtaka binafsi *(private prosecution),* sheria zetu ziko wazi.

Pili, taarifa kwa kweli sio ya siri kwa maana ya siri ya Serikali. Taarifa hii inaweza kujadiliwa mahali popote lakini ni taarifa ya uchunguzi ambao umefungwa na

uchunguzi huu unahusu masuala ya jinai na kama kuna dosari zozote katika uchunguzi mwelekeo ni kwenye Mahakama na hata siku moja sio Bungeni.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimeuliza na mimi mwenyewe nimesema sina tatizo na mwelekeo wa jinai kwa sababu wote tunajua mwelekeo wa jinai unakwenda Mahakamani. Nimeuliza kwenye ile taarifa inazungumzia mapungufu na inazungumzia uzembe. Sasa Serikali ni moja. Baada ya taarifa ile kutamka kuna uzembe na kuna mapungufu yalielekezwa wapi hayo ili sehemu ya Serikali inayohusika iweze kuchukua hatua za kinidhamu? Nilifikiri Wizara hii ikiwemo Wizara ya Ofisi ya Menejementi ndio sehemu ambayo inastahili. Sasa Serikali ni vyema ikatuambia, kinapotokea kitu cha namna hii katika taarifa ya namna hiyo linaachwa linafungwa? Kama ikifungwa ni chombo gani kinachukua kutoka pale ili yale yaliyojitokeza pale ambayo sio ya kijinai yaweze kufanyiwa kazi au ndio tunaacha? Iwapo hivi ndivyo, kwamba inaachwa, je, dhamira ya Serikali ya kufuatilia uzembe, hata hii dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuita watendaji ili pale panapotokea uzembe hatua zichukuliwe, tunachukuaje hatua iwapo taarifa ya namna hiyo inafungwa haipelekwi kwenye chombo kinachohusika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ufafanuzi zaidi kuhusu suala hili. Ikumbukwe kwamba kwa mujibu wa sheria ya Kupambana na Rushwa, uzembe pia ni kosa la jinai. Lakini iwapo Mheshimiwa Mbunge anafikiri kuna uzembe kwa jinsi suala la Richmond lilivyoshughulikiwa, kwa utaratibu wake anaweza kulileta Bungeni lakini sio kutumia taarifa ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Taarifa ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa malengo yake ni kufungua kesi shauri la jinai.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* …………Sh.516,489,400/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Division* ….Sh.582,224,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ……………...Sh.313,212,000/=
Kif. 2001 – *Cabinet Secretariat* …………..Sh.1,082,319,000/=
Kif. 2002 – *Communication Division* ………Sh.346,040,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Good Governance* ………………Sh.433,963,000/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2003, kinachohusu utawala bora, kifungu kidogo 250100, nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na utawala bora, jambo linalohusiana na dhana nzima ya utawala bora ambayo imebainishwa pia katika Katiba ambapo inaonyesha wazi kazi ya Bunge ni kuidhibiti Serikali *oversight function*. Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anaeleza juu ya

jambo la *BoT* ametumia maneno kwamba Serikali imemwagiza *CAG*, sizungumzii juu ya *BoT,* hapa nazungumzia juu ya dhana nzima ya utawala bora. *CAG* (Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali), yeye analeta ripoti yake Bungeni. Anapoagizwa na Serikali anapeleka ripoti yake wapi? Mimi nafikiri dhana nzima ya *check* and *balance* kwamba Serikali na Bunge na likitumia Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ni kuikagua Serikali na kwa hili kwa kukagua *BoT* tunakagua Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Serikali kusema itaagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaliondeshea madaraka Bunge la Tanzania. Nataka maelezo. Hii ni dhana kweli ya utawala bora ambapo madaraka ambayo yamewekwa kwenye Bunge sasa yanachukuliwa na Serikali na yule atakayetoa ripoti yake atapeleka kwa Serikali au Bungeni? Hii inaelezwa namna gani katika Katiba ya Tanzania? Naomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimsahihishe kidogo Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali akimaliza ukaguzi wa mahesabu na taarifa yake ikikamilika huwa anamkabidhi Mheshimiwa Rais ama Mheshimiwa Rais anampeleka Waziri Mkuu ndio huwasilisha Mezani hapa Bungeni. Huu ndio utaratibu uliopo na utaratibu wa Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la Benki Kuu, nafikiri ni suala la lugha. Ni wajibu wake. Nani angepewa kazi hii? Benki Kuu ni chombo kizito sana katika nchi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ndio *Auditor* wake na ndio anayeaminika ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, suala hapa mimi nafikiri ni kumpa kazi au kumwagiza. Lakini mimi ninavyoona, kwa vyovyote vile hii bado haiathiri ile dhana ya kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anawajibika kufuatilia mwenendo wa Benki Kuu. Ndio Mkaguzi wake na ni kazi yake kufanya hivyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika. Kama ni kusahihisha maneno kwamba tumemwagiza Mkaguzi na Mdhibiti wa Serikali kama ndivyo anavyotaka kufanya naweza nikakubali lakini dhana nzima ingekuwa jambo hili lisingetolewa kwenye Bunge likapelekwa Serikalini. Hoja hii iko kwenye Bunge ni mali ya Bunge, inakuwaje inachukuliwa na Serikali? Kama ni *Select Commitee* ingetengenezwa *Select Committee* na Bunge na ikasaidiwa na *CAG* na ripoti ikaletwa Bungeni. Sasa ananiponiambia kwamba ripoti itapelekwa kwa Waziri Mkuu halafu atalileta, Waziri Mkuu asipopenda hiyo ripoti, Sisi tuna mamlaka gani ya kumuomba *CAG* alete ripoti hiyo? Lakini kama *terms of reference* zingekuwa zimetolewa na Bunge, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anapaswa kuleta hiyo ripoti Bungeni ambapo ni mali ya Bunge. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge hawezi akapata taarifa zote za utendaji wa shughuli za Serikalini za kila siku. Lakini, mimi naamini anasoma magazeti ya hapa nchini mara kwa mara. Taarifa kuhusu uchunguzi wa Benki Kuu ulianza mwishoni mwa mwaka jana.

Makaratasi haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaleta hapa, Serikali ilishakuwa na taarifa na makaratasi hayo toka Novemba mwaka jana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha alishatangaza dhamira yake ya kuchunguza Benki Kuu toka mwishoni mwa mwaka jana. Kwa hiyo, ajenda hii ilishakuwa inafanyiwa kazi na Serikali kabla haijaanza kujadiliwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MH. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**NAIBU SPIKA:** Siyo juu ya suala la Benki Kuu hapa!

**MHE. DR. WIBORD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana! Mimi suala la Benki Kuu nilishasema nitaleta hoja ya *select committee*, kwa hiyo siongelei hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia kifungu 2003 - *Basic Salary,* tena nikiamini kwamba hapa ndio Waziri wa Utawala Bora alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuelewa kwangu na nitaomba Waziri anieleze kama sivyo, Utawala Bora ni pamoja na mambo yote yanayohusu Utawala Bora wa Fedha za Nchi, Taratibu za *Accountability*, *Transparency,* yaani uwazi, kupiga vita mambo yote yanayohusu ubadhirifu na kupiga vita mambo yote yanayohusu uzembe. Waziri katika kujibu swali langu la awali hapa sasa hivi anasema kwamba taarifa ile imefungwa na Mbunge akitaka ailete kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza sasa kwamba iwapo hivi ndivyo, ni nini wajibu wa Ofisi hii ya Waziri wa Utawala Bora? Tulifikiri kwamba mambo haya yanapotokea Waziri wa Utawala Bora ndiye anayekuwa wa kwanza kuyaleta kwenye Ofisi inayohusu kama ni Maadili ama ni Nidhamu yeye ndiye anakuwa wa kwanza kwa sababu taarifa imeanzia ofisini kwake. Lakini Waziri anasema imefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka pia kupata maelezo ya kina kwa taarifa iliyotolewa kwenye Kamati nadhani ya Mheshimiwa John M. Cheyo ya *PAC* pamoja na taarifa tuliyoletewa hapa Bungeni, matumizi yaliyotumika kwa ajili ya vifaa hivi ambavyo *PCB* imevileta nchini ni zaidi ya bilioni 172 na kwamba tutaendelea sasa kuvilipia hata kama hatutumii kwa kipindi chote cha miaka miwili kwa sababu katika taratibu ndivyo zilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuingia kwenye suala la Mkataba. Nataka kurudia pale ambapo chombo cha Serikali kinachotumia kodi ya wananchi, kinathibitisha kwamba kuna mapungufu na uzembe, Ofisi yetu ambayo tulitegemea ndiyo ya Utawala Bora inasema tumefunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka Waziri aniambie ni kwa sasa ataendelea kulipwa mshahara, kama yeye katika Ofisi yake kunatokea tukio kama hili na Watanzania wanaendelea kulipia, Ofisi yake inasema tumefunga, Mbunge alete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tunatoa mshahara kwa Waziri ambaye tunategemea Utawala Bora yeye ndiye anaulezea, anaupigania na Ofisi yake inataka sisi pia tumsaidie kuendeleza Utawala Bora kule kwenye Wilaya zetu? Ninapenda nipate maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ngoja kwanza nielewe swali. Upande wa TAKURU wamesema wao wamefunga, kwa maana hiyo upande wa Serikali wanasema wamefunga lakini Waziri amesema kama kuna mtu ana ushahidi wa kutosha haimzuii yeye kufungua hili suala, nafikiri nimeelewa hivyo.

Sasa tukiwa tunarudia palepale ni kwamba kama Mbunge yeyote ana ushahidi na sio lazima Mbunge, hata mwananchi kama ana ushahidi wa kutosha haizuii kufungua hili suala, nadhani ndivyo nilivyoelewa mimi. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yako ni sahihi. Serikali imesema imefunga msingi wa hoja yangu, ni kwamba hata kama ile sheria ya *PCB* inavyosema na nadhani tunafikiri tutarudi kwenye ile sheria kwa wakati muafaka. Sheria inasema, taarifa ile inakuwa *tabled* Bungeni, sheria ya *PCB* na Mheshimiwa Waziri tuling'ang'ania pale, tulieleza wakati tunatunga ile sheria kwamba *PCB* inatakiwa iwe chombo huru ili Wabunge kwa kupata taarifa mbalimbali zilizofanyiwa utafiti tuweze pia kuchukua hatua. Serikali iling'ang'ania ikaseme *PCB* itabaki Ikulu. Sisi tukasema tumeifanya kuwa chombo kisicho huru. Sasa Wabunge hawana chombo cha uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya uchunguzi ni vyombo vya dola, ndiyo tunavilipia kodi yetu. Chombo cha dola kinapofungwa vilitegemea yale ambayo siyo ya kijinai yatahamishwa kwa idara ya Serikali ambayo haishughulikii na jinai mathalani madai sasa kama hivi. Ndivyo mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri anipe maelezo, lakini kama sivyo katika hatua ya mbele tutachukua utaratibu mwingine wa kudai hiyo taarifa kwa njia ya kanuni zetu. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mimi swali langu litakuwa ni hapo hapo kwa *good governance and support* 2003 *basic salaries.* Nilikuwa napenda kupewa ufafanuzi kwamba masuala ambayo tumekubaliana kikatiba, *a good governance* yanaeleweka na yameandikwa. Lakini katika Wilaya ya Tarime kwa muda mrefu sasa kumekuwa na mfumo mwingine wa utawala ambao unaitwa mabaraza ya jadi au sungusungu ambao una uwezo wa kukamata, kusikiliza kesi, kuhukumu kupita faini na hata kufanya uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu ambao hauko kisheria. Wakati ambapo katika Wilaya ile kuna Mahakama, kuna Polisi, lakini unatumika mtindo wa kusema kwamba wanafumbia macho.

Kwa hiyo, wale wanakuwa na ruksa ya kufanya shughuli zao katika vijiji 77 vya Jimbo langu na nikitoa mfano wa kijiji kimoja cha Nyakungulu ambako kwa mwaka mmoja waliweza kuchukua mbuzi, ng'ombe, sufuria na vitu vya aina hiyo ambavyo vina

thamani ya zaidi shilingi milioni mbili ambao uki-*multiply* kwa vijiji 77 utaona ile *magnitude* ya kazi ambayo wanaifanya.

Sasa ningependa kutoa ufafanuzi ya kwamba hii kazi inayofanywa ni sehemu ya *good governance* kama siyo sehemu ya utawala bora niliwahi kuzungumza mbele ya Waziri Mkuu, akaagiza kwamba kama nina ushahidi nipeleke, nikaandika, nikakusanya ushahidi wote kitabu chenye ukurasa 97 na hata wewe Mheshimiwa wa Waziri wa Wizara hiyo ulipata nakala ambayo inaonyesha aina ya uvunjaji wa haki za binadamu unaofanyika Tarime na kuvuruga utawala bora. Sasa ningependa kujua kwamba wale wanafanya kazi kwa misingi ipi kwa sababu kufanya kazi mwaka mzima bila mshahara lakini wanaishi, hawalimi, kwa hiyo, inabidi waishi kwa kuwala wananchi wengine. Ningependa kupewa ufafanuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tuko kwenye kamati ya matumizi kwa hiyo usitupige hatua sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Chacha Wangwe kuhusu matatizo yaliyoko kule Tarime. Matatizo yaliyoko Tarime siyo mageni, yalikuwepo hata kuanzia enzi za Wakoloni. Tanzania huru tuliwahi kujitahidi sana kupambana na vitendo vya uhalifu, wizi wa mifugo, mauaji na kadhalika.

Naweza kusema kwamba kwa kweli ukiangalia kwa undani kabisa kuna tatizo la utawala bora katika maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Tarime. Lakini kiini hasa ni uhalifu. Uhalifu huu lazima wote tuungane tupambane nao. Kama kwa miaka zaidi ya 50 matatizo ya Tarime yamekuwa yakishughulikiwa kwa njia moja au nyingine, leo isingekuwa rahisi kwa sisi kutatua tatizo lile kwa mara moja.

Mimi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Usalama wa Raia na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, tulifika Tarime kujadiliana namna ya kutatua tatizo la uhalifu kule. Tukakubaliana hatua kwa hatua matatizo yale yaweze kumalizwa kimila kwa sababu chanzo pia ni mila za wananchi wa kule. Tukumbuke pia sheria za nchi hii pia zinatambua baadhi ya mila ikiwa ni pamoja na mila ambayo inawaweka walinzi wa amani. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika vizuri na hilo jibu kwa sababu tukiangalia takwimu za uhalifu katika nchi hii tunaona kwamba tukichukulia kwa *rating* ya Mikoa, Mkoa wa Mara unakuja wa saba, ukitanguliwa na Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na sehemu nyingine. Lakini kumekuwa na dhana ambayo imeelezwa Kiserikali kwamba watu wa Mkoa wa Mara hususan Wilaya ya Tarime ni wahalifu sana, wakati ambapo naona ya kwamba ni kauli ambayo ni ya kuwatenga na kuwabagua kwamba wao ni watu wenye mila tofauti na watu wengine hapa Tanzania ambao wameshiriki ulinzi na uongozi wa nchi hii na miaka mingi wamewekeza katika usalama wa nchi mnafahamu. Kama wangekuwa watu wabaya kiasi hicho, waliwezaje kufanya kazi katika majeshi?

Kwa hiyo, mimi nafikiri hii *stigma* ya kuweka utawala tofauti ambao haupo katika maeneo mengine ya Tanzania hasa katika Wilaya ya Tarime na Serengeti inaonyesha kuna namna fulani ambayo inatumika kinyume na utawala ya kuwaona na kuwabagua na kuwa-*marginalize* wale watu wa Tarime kwamba pengine wao ni watu tofauti na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndiyo ambalo nilikuwa napenda anipe ufafanuzi kwamba je, ni lini sasa tutaanza kutumia Katiba na sheria katika utawala bora pale Tarime badala ya kutumia hizo mbinu za mila na desturi ambazo pengine siyo za Tarime? Kwa sababu kama sungusungu imetokea Usukumani, Wakurya wenyewe wana mila zao na desturi ambazo zinaheshimu wazee na vijana, *worriers* kutatua mambo yao. Lakini hii mila ya sungusungu imetokea Usukumani na ndiyo inayoua watu pale. Sasa ningependa kujua kwamba basi kama ni hivyo tutumie za Kikurya sasa. *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Waziri, hakuwabagua watu wa Mara wala watu wa Tarime. Lakini ni ukweli kwamba Tarime ndiyo pekee kumebaki Tanzania ambako ukoo huu unagombana na ukoo huu, kabila hii inagombana na kabila hili, mambo ambayo ni ya zamani sana katika nchi yetu.

Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tumekwenda kule, tumezungumza na viongozi ukweli mmoja ambao Mheshimiwa Wangwe anaukataa hapa. Ni kwamba yale mabaraza ya jadi yana nguvu kweli kweli, yanasikilizwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunasema, sungusungu na Mabaraza ya jadi yanasaidia kuleta amani na ndio kazi yetu kuleta amani. Tunawaunga mkono na tutaendelea kushirikiana nao kuhakikisha katika nchi watu hawagombani koo kwa koo kwa mambo ambayo hayana maana yoyote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wangwe, unataka kufanyaje sasa?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka siku Waziri Mkuu alipokuja...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wangwe naomba ukae kwanza. Sasa tunataka kufanya *dialogue* humu ndani. Tumeshamaliza, umeshafafanuliwa ulichotaka kuuliza, tuko kwenye Kamati ya Matumizi, hatuko kwenye Kamati ya kuanza *dialogue*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2004…………………………….. Shs. 339,204,700/=

**FUNGU 32 – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA.**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, katika kifungu hiki kulitokea mabishano ya Katiba inasema nini kuhusu taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katiba kifungu 143 (4) kinasema: "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hiyo." Ibara ya pili inazungumzia majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge au Naibu Spika ikiwa Kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yoyote ile Spika hawezi kutekeleza shughuli za kazi zake ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilitajwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1001 *Administration and General*...Sh. 6,565,878,000/=

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Mojawapo ya kero kubwa ambazo...

**MWENYEKITI:** Naomba kifungu kwanza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** *Program* ya 10, *Sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100. Mojawapo ya kero kubwa ambazo watumishi wa umma wanakutana nazo ni kutokupandishwa vyeo kulingana na kanuni za utumishi, yaani *Standing Order.* Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Utumishi amelitambua tatizo hilo, sasa mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hapa kwamba kulingana na mkakati wake, ni lini anategemea kwamba hili tatizo la kupandishwa vyeo watumishi wa umma litakuwa limekwisha?

Swali langu la pili, katika watumishi wa umma hao hao ukiangalia *intake* moja katika Wizara/Idara moja ya Serikali na nyingine baada ya muda utakuta kwamba baadhi ya watumishi kwenye baadhi ya Idara wanapandishwa kwa haraka zaidi au wanafikia vyeo vya juu zaidi kuliko katika Idara nyingine. Sasa mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, labda kuna tofauti ya madaraja kutoka daraja, uwingi wa madaraja au katika miaka inayochukua kwa mtumishi kutoka katika ngazi moja hadi ngazi nyingine katika kila idara ya Serikali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi wa suala alilouliza Mheshimiwa Kajege. Kuhusu suala la watumishi ambao hawajapandishwa vyeo, napenda kumpa taarifa kwamba suala la kuwapandisha vyeo watumishi ambao walirundikana na ambao walikaa muda mrefu hawajapandishwa vyeo tulilianza mwaka jana katika bajeti ya mwaka 2006/2007 ambapo tulipandisha watumishi zaidi ya 9,000 na walimu ambao kwa wingi tumewapandisha safari hii ni kwamba uchambuzi wao ulichukua muda mrefu kwa

sababu tuliletewa malalamiko zaidi ya 75,000 na ilibidi lazima tuhakiki na baada ya kumaliza kuhakiki ikiwa kifungu ambacho tulitenga shilingi bilioni 10 zilikuwa zimekwisha, tulishatumia shilingi bilioni 12.

Kwa hiyo, tukasogeza mwaka huu. Sio walimu peke yake, kama mlivyoona katika kitabu cha Bajeti tumeweka watumishi wengi tu. Kwa hiyo, sasa hivi sitegemei. Naweza nikamwambia, kama tumemaliza sitegemei kama kuna watumishi ambao walikuwa hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu ambao hawajapandishwa labda kama mwajiri wake amefanya uzembe.

Suala la pili alilosema, kuna watumishi wengine anaona wanapandishwa haraka haraka vyeo wakati wengine wanachelewa. Je, kuna taratibu gani? Ningependa kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba inategemea kada na kada. Mfano kama Wahasibu, kama wewe labda ni Mhasibu Msaidizi au Karani wa hesabu ili kuwa Mhasibu ni lazima ukasome. Sio kukaa peke yake kwamba uko mtumishi kwa miaka 10 utakwenda nafasi nyingine ya juu, haiwezekani. Ni lazima ukasome!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna kada ambazo ukishakuwa na *degree* ya kwanza au ukishakuwa na *diploma* unaweza vyeo vyake vikawa vinakwenda. Lakini kuna vyeo vingine vya taaluma ni lazima ukasome. Ukishafika *bar*, kwenye *bar* yako hata ukae miaka 30 kama hujakwenda kusoma huwezi kupandishwa. Kwa hiyo, ndiyo hiyo tofauti iliyokuwepo.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tuchukue mfano wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na ushirikiano wa kimataifa, ambayo watumishi wake wengi wana *degree* za *masters* na wanafanya kazi vizuri sana. Lakini mpaka muda huu kuna baadhi ya wafanyakazi miaka mingi hawajapandishwa vyeo. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu kutatua tatizo la watumishi wa Wizara za Mambo ya Nchi za Nje?

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, safari hii ameona tumepandisha vyeo zaidi ya watumishi 85,000. Kwa hiyo, kama ni kweli, hao wana sifa. Kwa maana hiyo, taaluma yao lakini pia na utendaji mzuri wa kazi kwa sababu hatuangalii elimu na muda wa kukaa kazini, pia tunaangalia utendaji wako. Kama ni wale wazembe ambao Mheshimiwa Ndugai ametuambia, hiyo *life time employment* uko tu umekaa kwa kweli hawatapandishwa, lakini kama kweli wana sifa na wanafanya kazi vizuri. Nina imani kabisa wamo katika watumishi waliopandishwa vyeo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002……………………..............Shs. 152,079,000/=
Kifungu 2001……………………………. ..Shs. 351,671,100/=
Kifungu 2002…………………………...... Shs. 263,466,000/=
Kifungu 2003…………………………...... Shs. 418,475,600/=
Kifungu 2004 ……………………….....… Shs. 142,836,000/=

Kifungu 3001 …………………………...... Shs. 443,911,000/=
Kifungu 3002 ………………………. ......Shs. 674,643,000/=
Kifungu 3003 …………………………...... Shs. 73,044,000/=
Kifungu 3004 …………………………..... Shs. 69,090,000/=
Kifungu 4002 ………………………….... Shs. 219,243,000/=
Kifungu 4003 ………………………….... Shs. 483,176,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 33 – SEKRETARIET YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

Kifungu 1001 - *Administration and General............................ Shs. 1,500,009,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 94 - TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

Kifungu 1001 …….……………………. Shs. 2,012,498,300/=
Kifungu 2001 ……………………………Shs. 396,059,100/=
Kifungu 2002 ……………………………Shs. 449,739,800/=
Kifungu 2003 …………………………...Shs. 4,280,731,100/=
Kifungu 2004 ……………………………Shs. 330,200,300/=
Kifungu 2005 ……………………………Shs. 348,892,400/=

**KITABU CHA NNE MATUMIZI YA MAENDELEO**

**FUNGU 30 – OFISI YA RAIS NA SEKRETARIETI YA BARAZA YA MAWAZIRI**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division*……................... Shs. 69,590,206,000/=

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka ufafanuzi, niko kwenye *sub-vote* 1003 *item* 6220 - *TASAF*. Hizi fedha ni msaada wa *ADA* ni msaada wa maendeleo kwa wananchi. Lakini zinapokuja kwetu, nakusudia kwetu hasa Pemba, fedha hizi huwa ni za kisiasa au kiitikadi. Nafikiri nimeandika kwa Mheshimiwa Waziri. Vijiji vyetu vinaambiwa viibue miradi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeandika kuna kijiji cha Makangale kwenye Jimbo langu, Konde wameibua mradi wao, ni wavuvi wanataka *fishing gears* na fomu hizo zikapelekwa kwa wahusika na wakaambiwa zinafanyiwa kazi. Lakini kumbe baadaye zikatiwa kapuni akaambiwa Sheha aandike fomu nyingine na msaada ule ulipokuja

wakapewa wanaCCM peke yao. Sasa nataka ufafanuzi: Je, fedha hizi za maendeleo za *TASAF* zinakuja kwa itikadi kwa chama fulani tu? Tujue!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha za *TASAF* hazitolewi kwa misingi ya itikadi hata kidogo. Kama kuna maeneo ambayo miradi hii imefanikiwa ni Visiwa vya Unguja na Pemba. Sisi kwenye Wilaya zetu tunapenda kuwatuma Maafisa wanaohusika na *TASAF* kwenda Pemba na Unguja ili kuangalia jinsi ambavyo miradi hii imefanikiwa sana. Mashahidi wetu ni Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala ambao mara kwa mara wamekuwa wakitembelea miradi hii.

Sasa kama kuna tatizo la pekee kama hili analoongelea Mheshimiwa Mbunge la Kijiji cha Makangale basi alilete kwa utaratibu unaofaa kwa kupitia kama ya Waziri Kiongozi na baadaye Makao Makuu ya *TASAF*. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mbona sijakuita?

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Ahsante sana. Kamati ya uvuvi inahusika, wamenipigia simu na wameletea barua. Kwa hiyo, nafikiri labda kama ulivyopendekeza nafikiri tukutane baadaye ili tuone kwamba…..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, endelea kusema. Mimi ndiyo Mwenyekiti, hapa. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri baadaye tutafute utaratibu ambao labda msaada huu ambao tayari umetoka ili uwafaidishe wote sio kundi moja tu au Chama kimoja tu.

**MWENYEKITI:** Alichokwambia Mheshimiwa Waziri wa Nchi ni kwamba, kama ni kweli unayoyasema, basi watumie utaratibu wa Ofisi ya Waziri Kiongozi, halafu itajulikana ni mazingira gani kijiji hicho kilinyimwa msaada huo na hasa kama kilitimiza masharti ya *TASAF*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 32 – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

*Kifungu 1001 - Administration and General... …………………. Shs.4,720,144,300/=*
*Kifungu 2001 – Policy Development... ... Shs. 1,292,943,000/=*
*Kifungu 2002 – Management Service... ... Shs. 7,032,175,000/=*
*Kifungu 2003 – Establishment ... ... ... Shs. 955,300,000/=*

*Kifungu 2004 -Ethics Division ... …… ...Shs. 713,900,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kifungu 3001- Human Resource Development…………….Shs. 1,733,790,000/=*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikilinganisha fedha ambazo zimetengewa kifungu...

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 3001 *sub-vote* 6254, yaani shilingi bilioni 1.7. Naona kama ni kidogo sana kulinganisha na kazi iliyopo kuliko ukiangalia *sub-vote* 2002 kifungu 6254 nilifikiria kwamba labda hizi shilingi bilioni saba ndiyo zingekuja kwenye *human resource development* badala ya kuja kwenye *management services*. Labda tupate maelezo ambayo yataridhisha kwamba kweli fedha hizo zinastahili kuwa hapo.

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha zimewekwa kiidara. Kwa hiyo, pale zilipokaa, shilingi bilioni saba zinastahili pale kutokana na kazi zilizopangwa katika idara hiyo na huko kwenye *human resource development* pia zinatosha hizo hizo zilizowekwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Yaani pale ni Sh. 1,700,000,000/= na pale pengine ni Sh. 706,000,000/= siyo!

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri alikubali kabisa kwamba tuna tatizo la *capacity* katika watumishi wa umma. Sasa mimi nilifikiria kwamba sehemu kubwa ya fedha zingekwenda katika *human resource development,* yaani kujenga *capacity* ya watumishi wa umma na wala siyo katika *management services.*

**MWENYEKITI:** Sasa Serikali inayofanya kazi hiyo ndivyo ilivyosema kwamba ndivyo imeweka siyo kwamba wamekosea. Kwa hiyo, nadhani hatuwezi kufanya zaidi ya hapo, wamesema walivyopanga ndiyo hivyo hawajakosea. Maana yake tulifikiri wamepitiwa, lakini wanasema ndivyo walivyopanga.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kifungu 3002 – Civil Service Training Centre... ... ... ... ... ... ... Shs. 776,703,000/=*

*Kifungu 3004 – Gender ... ... ... ... ... ...Shs. 1,055,252,000/=*

*Kifungu 4002 – Management Information*
*System ………………… Shs. 7,446,840,000/=*

*Kifungu 4003 – National Archives …… Shs. 1,897,800,000/=*
*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imepitia Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, ikijumuisha Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makisio ya bajeti ya Ofisi ya Rais kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mchana Kamati ya Uongozi, imekaa na kuangalia tena ratiba yetu kutokana na matatizo tuliyopata hapa katikati. Kwa hiyo, tumeona ni vizuri kadri inavyowezekana Wizara zote ziwe zinasomwa nyakati za asubuhi, kusudi wananchi wengi waweze kufuatilia kinachoendelea Bungeni. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12. 36 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 4 Julai, 2007 saa tatu asubuhi)*